

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Mbili - Tarehe 12 Juni, 2014

(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. MCHEMBA):

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa Mwaka 2014/2015 [*The Monetary Policy Statement for the Financial Year 2014/2015*].

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya Alhamisi tunaanza na Maswali kwa Waziri Mkuu, lakini leo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hayupo, hivyo naanza kumwita Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi nyingi ambazo zimekabiliwa na tatizo kubwa la ajira kwa Vijana. Kila mwaka vijana wanamaliza mafunzo yao lakini ni wachache sana wanaopata ajira na kwa maana hiyo kundi kubwa kubakia halina ajira.

Je, Waziri Mkuu una mpango gani, mkakati gani au mazingira gani ya kuwatumia vijana hawa mara tu baada ya kumaliza mafunzo yao.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu, swali limekuwa *precise*.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah swali lake, mimi nafikiri zuri sana kwa sababu Watanzania wote ndiyo jambo ambalo tunalizungumza sana. *(Makofi)*

Kwanza, nilitaka nianze kwa kusema kwamba tatizo la ajira siyo jambo la Tanzania tu ni tatizo kubwa kwa kweli Afrika na Duniani kote. Lakini kila nchi inajitahidi kuona ni namna gani wanaweza kupunguza hilo tatizo. Kwa nchi changa zenye uchumi mdogo kama zetu nadhani changamoto hiyo inakuwa ni kubwa zaidi, matumaini yangu ni kwamba kwa juhudi ninazoziona zinafanywa na Serikali chini ya Chama cha Mapinduzi (CCM) nina hakika kabisa tatizo hili baada ya muda si mrefu tutakuwa tumelikabili vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, mategemeo yetu makubwa kwenye ajira kwanza ni sekta ya umma yenyewe kwa maana ya Serikali, Mashirika yake, na vyombo vyake vingine ndiyo maana unaona kila mwaka walimu kadhaa tunawachukua, watalaam kadhaa. Kwa hiyo, kuna *element* hiyo ya sekta ya umma ambayo ndiyo eneo la kwanza tunalolitegemea, lakini siyo kubwa la kuweza kuchukua watoto wote wanaomaliza Vyuo na Elimu ya Juu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo ndilo tegemeo letu ni sekta binafsi. Ninaposema sekta binafsi hapa ina sura mbili. Sekta binafsi kwa maana kwamba yeye mwenyewe mtu mmoja mmoja kujajiri kutegemea na fursa anazoziona.

Lakini sekta binafsi kwa maana ya kuajiriwa katika vile vyombo au makampuni ambayo tayari yanahitaji ajira. Hivyo, vyote viwili tunajaribu kuvipa msukumo mkubwa sana. Kwa hivyo, kwa upande wa Tanzania ndiyo maana unaona tumekuja na sera za namna mbalimbali za kutuwezesha kuongeza idadi ya Viwanda. Tume-*open up* sana suala la uwekezaji hapa nchini, tunajitahidi sana kwenye maeneo maalum kama EPZ pamoja na ZES zote hizi ni katika jitihada za kujaribu kuona namna ya kukabiliana na jambo hili. Lakini nilazima nikubaliane na wewe, ni jambo kubwa, ni jambo linatukera lakini nadhani hatua kwa hatua tunaweza tukaendelea kulikabili wote kwa pamoja. *(Makofi)*

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake mazuri, nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania inatumia fedha nyingi sana kuwafundisha vijana wetu ndani na nje ya nchi. Lakini matokeo ya mafunzo haya na matumizi ya fedha hizi vijana hawa wanaondoka na kwenda kutumikia nchi nyingine jambo ambalo ni hasara kubwa sana kwa Taifa.

Je, kama Waziri Mkuu unasemaje kuhusu suala hili, ni hatua gani utazichukua ili watalaam hawa waweze kubakia ndani ya nchi na kuweza kutumia Taifa hili.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka niseme tu kwamba si dhambi kwa Mtanzania kwenda kufanya kazi nje kama fursa hiyo ipo. Ni jambo ambalo tunapaswa tuwatie moyo, ni namna tu ya watu kutumia muda na fursa walizonazo kuona namna wanavyoweza kujiendeleza.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa hiyo mimi nadhani tusione kama ni jambo baya sana, Hapana! Mimi nadhani tuwatie moyo, waende popote na nchi nyingi ndivyo walivyofanya. Wamewa-encourage vijana wao kwenda popote pale kufanya kazi lakini kwa matarajio kwamba baada ya muda siyo mrefu watarudi, watakuwa wamepanua uelewa wanaweza vilevile wakatuhudumia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nadhani jambo la msingi ni kwamba hizi sera ambazo tunakwenda nazo, polepole zitapunguza hata hiyo kasi ya watu kutaka kwenda kufanyakazi nje. Kubwa kwani hapa *brother* ni nini? Kubwa hapa ni je, kuna mahali nitapata vihela hivi niweze kuishi? Kama tutaendelea na sera ya kuongeza mishahara yetu wakati uchumi unapanuka, wengi hawa tunaweza kabisa kuwa-retain kwa sababu watakuwa hawana sababu ya kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini nakubaliana bado na swali la msingi lipo pale pale ni lazima juhudi za kuendelea kutafuta mbinu mbalimbali za kuongeza uwezekano wa kuwa na ajira pana liwe ndiyo hasa lengo kubwa la kila mmoja wetu. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana, tuendelee na Mheshimiwa Haji Khatib Kai.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, Taifa lolote Duniani linategemea wasomi na kwa kuwa kuna taarifa za wanafunzi wa UDOM wapatao 500 watazuiliwa kufanya mitihani yao kwa kushindwa kulipa ada za mitihani hiyo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nini kauli yako juu ya Wanafunzi hawa, watoto wa maskini? (Makofi)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, imani yangu mimi kwanza ni kwamba sidhani kama tutaweza kuruhusu wasifanye mitihani, sidhani. Pengine mimi nikushukuru tu kwa sababu umeliuliza, kwa sababu mimi nilikuwa sina taarifa hizo. Nina vijana wangu wa UDOM mara nyingi ni wepesi sana kunifuata wanapokuwa na jambo lolote linalowakabili.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninachoweza kuahidi ni kwamba tutalifuatilia kwa karibu sana na tutahakikisha wote wanafanya mitihani, kwa sababu tumewasomesha, tumewapeleka pale, suala la kwamba hana ada leo au nusu ada amelipa haliwezi kuwa ndiyo sababu ya kumfanya mtu ambaye amekaa miaka mitatu, minne asitumie nafasi yake ya mwisho kuweza kufanya mitihani. Hapana! Hilo tutahakikisha wanafanya. (Makofi)

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, nimeridhika na majibu ya Waziri Mkuu. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana, afadhali umetumia busara. Mheshimiwa Suleiman Said Bungara, hawa wote ni CUF leo walijipanga.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Mkoa wa Lindi na Mtwara kwa muda mrefu sasa hivi imezuiliwa mikutano ya hadhara ya kisiasa na ya kidini. Je, ni sababu zipi ambazo zimesababisha mikutano hiyo izuiliwe.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ilichukua hatua ya kusitisha mikutano ambayo inaweka watu wengi kwa pamoja tangu zilipotokea vurugu pale Mtwara miaka miwili hivi nafikiri na zaidi kidogo iliyopita. Kazi ya Serikali imekuwa ni kuendelea kuhakikisha tunarejesha ile hali ya utulivu kwa Mkoa ule lakini Lindi kutokana na ujirani wake na Mtwara nao walikumbwa na uamuzi huo.

Nataka nikuhakikishie tu kwamba jambo hili tunaendelea kulifanyia tathmini na hata juzi nilikuwa nazungumza na Wakuu wa Mikoa yote miwili ili tuweze kufika mahali na kuruhusu tena shughuli fulani ziweze kuendelea kama ambavyo tulikuwa tunafanya kabla.

Mheshimiwa Spika, rai yangu tu kwa wana Lindi na Mtwara kutambua tu kwamba sisi kama Serikali tunao wajibu wa kuendelea kuhakikisha watu wanaishi kwa amani, kwa utulivu bila vurugu na kadiri tutakavyopata ushirikiano wa karibu kutoka kwao hatuna sababu yeyote ya kuendelea kushikilia uamuzi huo kwa sababu ulifanywa kwa maksudi maalum, sababu ile ikishatoka hatuna haja ya kuendelea nalo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Selemani bado una swali la nyongeza?

MHE. SULEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa, sasa hivi kuna utulivu wa hali ya juu, huoni sasa utoe kauli rasmi kwamba mikutano hiyo iruhusiwe, hususani ukizingatia kwamba uchaguzi wa Serikali za Mitaa unanza hivi karibuni?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni vigumu kwangu Mheshimiwa Bungara kusema hivyo hapa, kwa sababu kwa sehemu kubwa ndiyo maana mimi nafuatilia muda wowote. Ile tathmini inayotoka kwenye Mikoa inayohusika ndiyo inaweza kunipa mimi nafasi ya kutoa kauli.

Lakini nataka nikuahidi tu kwamba hili jambo halitachukua muda mrefu sana kwa sababu kwa upande wa Lindi kwa mfano nilikuwa karibu tayari nikubali kwamba tufanye hivyo, lakini baadaye wakaniletea tatizo dogo hivi nikaona basi walimalize kwanza halafu tuone kama tunaweza tukawapa muendeleo na shughuli kama kawaida.

Usione hivi hata sisi kinatuuma, maana na sisi vilevile ni wadau na tungependa na sisi tufanye mikutano hiyo kwa sababu mwaka kesho siyo mbali. Sisi tungependa tuanze

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuonekana pale kwa nguvu kama ambavyo na ninyi mnavyopenda, lakini nina uhakika tutalimaliza mapema sana kabla hatujafika karibu sana na chaguzi hizo.

SPIKA: Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa Assumpter Mshama.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninatambua kabisa kwamba ardhi ni mali ya umma na pia mwenye mamlaka nayo ya juu ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna taratibu na miongozo inayotumika katika maamuzi ya kuchukua ardhi na kuigawa kwa mtu mwingine. Niseme tu kumekuwapo na utaratibu ambao Serikali inachukua ardhi lakini inashindwa kuwalipa fidia watu kwa wakati na hata ikiwalipa inawalipa hela kidogo.

Katika Jimbo la Nkenge, ni juzi tu Waziri wa Mifugo na Uvuvi ameamrisha wananchi wangu wanaokaa katika Kata ya Kakunyu kwamba waondoke mara moja katika maeneo yao, wakati imegawa hayo maeneo kwa JKT.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, jana usiku watu hawajalala, naomba kuuliza. Je, Serikali iko tayari kuwafidia kabla hawajaondoka katika maeneo yao ya makazi?

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu labda jaribu, maana yake ni *very specific*.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera ni kweli liko tatizo ambalo linagusa sana ardhi na maisha ya watu. Lakini pengine kwa hili ambalo Mheshimiwa Mshama ameuliza labda nieleze kwanza kidogo ili Bunge liweze kufahamu msingi wake ni nini.

Mheshimiwa Spika, maeneo anayoyazungumza Mheshimiwa Mshama ni maeneo ambayo yalikuwa chini ya NARCO ambalo ni shirika letu la umma. Ni eneo hili ambalo Serikali ilifanya uamuzi wa kugawa baadhi ya maeneo ya NARCO kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania wengine waweze kuendeleza sekta ya ufugaji kwa maksudi tu. Wapo ambao wamefanya vizuri na wapo wengine ambao bado wanasuasua.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nkenge anachokizungumza pale ni kweli, vipo vitalu vitatu, moja, saba na kumi na moja, ambavyo Serikali kwa maksudi tumeamua tuwape SUMA JKT. Uamuzi huu ulitokana na ukweli kwamba pale ni mpakani na kumekuwa na maneno mengi sana juu ya mpaka ule. Kwa hiyo tukaona namna moja ya kujihakikishia hali ya amani pale na utulivu kiulinzi tuweke vilevile chombo hiki katika eneo hilo. Watafanya mambo ya uzalishaji lakini vilevile wanaweza kuwa ni jicho la Serikali kutokana na mpaka ule tunavyokaribiana na nchi nyingine za jirani ndiyo maana tukafanya uamuzi ule.

Mheshimiwa Spika, JKT wapo pale kwenye kitalu Na. 7 wameshaweka na ng'ombe kidogo pale na polepole wanaendelea kuongeza idadi ya ng'ombe. Lakini wakati tumefanya uamuzi ule, mimi nina hakika Mheshimiwa Mshama jaribu ku-check. Mimi maelezo niliyopewa ni kwamba wapo tuliokwisha kuwaondoa, wapo wachache wamebaki pale, lakini kauli ya Serikali ni kwamba mara tu JKT watakapokuwa wame-settle na kupata lile eneo lao lote, wale wengine

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wote ambao tutakuwa tumewaondoa kwa yale maendeleo waliyokuwa wameyafanya watafidiwa.

Hakuna ambaye ataondolewa pale kwa mfano kama alikuwa amejenga banda lake pale, tutamfidia kutokana na kile alichokuwa ameendeleza, hatutamfidia kwa thamani ya ardhi kwa sababu ni ya NARCO, lakini kwa kile alichokiendeleza tutafanya. Ndiyo maana nadhani pengine cha kufanya tu ni kushirikiana na Mheshimiwa Mshama kujaribu kuzungumza na Mkoa nipate maelezo ya zaidi kuweza kuelewa mpaka sasa wapo katika hatua gani kwenye zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, pili wakati ule uamuzi unafanyika tulikubali vilevile kwamba Mkoa utazame mahali pa kuwapeleka hawa wengine, kuwa-*settle* katika maeneo mengine ili wasipate taabu ya mahali pa kwenda.

Kwa hiyo, mimi nadhani kilichotokea inawezekana pengine ni maelezo tu, nikipata picha kamili nitajaribu kushirikiana naye tuone hasa kimetokea nini kwa sababu sikutegemea kwamba linaweza kuwa ni tatizo kubwa kwa sasa, maana ni jambo tuliamua kwa maksudi tu.

SPIKA: Mheshimiwa Mshama, swali fupi la nyongeza.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimwombe kwamba ile kauli iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri isimame kwanza tuangalie wale watu kaya 650 tunawapeleka wapi na hatimaye muweze kuchukua eneo hilo, ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ningeweza nikatoa hilo tamko, lakini kufamya hivyo kabla sijawasiliana na Waziri mwenyewe nione msingi wake ulikuwa ni nini haitakuwa jambo la busara sana. Kwa hiyo, mimi nafikiri nikubalie tu kwamba baadaye nitazungumza na Waziri wa Mifugo na Uvuvi tuone msingi na maelekezo aliyoyatoa ni ya namna gani halafu nadhani tutalimaliza vizuri tu sidhani kama lina tatizo. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika ziara zako za kuhimiza na kukagua miradi ya maendeleo ulifika Mkoa wa Ruvuma na ulifika katika Wilaya ya Namtumbo.

Ulikutana na malalamiko ya Wakulima wa zao la tumbaku ambao walikuwa wanadhulumiwa fedha zao kwa njia ya mkopo. Serikali ilitamka pale kwamba itaunda Tume ya Ukaguzi kwenda kukagua na iliunda Tume ile, ripoti ya Tume ile ilitolewa ikakabidhiwa Serikali Kuu.

Wananchi wa Wilaya ya Namtumbo hususan Wakulima wa Tumbaku wanaotegemea uchumi wa tumbaku wanauliza, Serikali ripoti hiyo itawaeleza nini na hatua gani zitachukuliwa.

SPIKA: Kwamba hawajapokea taarifa ya ripoti hiyo?

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, karibu miezi minane sasa.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ni kweli nilipofanya ziara Ruvuma nilipofika Namtumbo suala hili lilijitokeza na nilichowaeleza wananchi pale ni kwamba Serikali italichunguza hilo jambo halafu tukishapata matokeo ya uchunguzi basi hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Sasa ni bahati mbaya tu kwamba jambo lenyewe kwa sababu limekuja katika mfumo huu nilikuwa sijafanya mawasiliano na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika lakini vile vile na Mkoa ili tuweze kujua tumekwama wapi na limemalizika namna gani.

Lakini nataka nikuahidi Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba nipe tu nafasi kidogo nimemwona Mheshimiwa Chiza yupo, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika pengine hata baada ya maswali haya tuone kama tunaweza tukakaa, tukapata maelezo ya kina ili hatua ziweze kuchukuliwa haraka kama ambavyo tulikuwa tumeahidi kwa ajili ya wale wakulima wa tumbaku.

SPIKA: Mheshimiwa Vita, bado una swali la nyongeza?

MHE. VITA R. M. KAWAWA: Nimeridhika Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimeamua kuendesha shughuli zake za Serikali kwa uwazi, kwa maana ya *OGP*. Yaani *Open Government Partnership* mpango ambao ulizinduliwa mwaka 2011 kule New York nchini Marekani ulijumuisha nchi za Marekani, Uingereza, Mexico na hata Afrika Kusini.

Na kwa kuwa mpango huu wa awamu ya kwanza sasa hivi umefikia mwisho wake 2014 na tunataka kuingia katika awamu ya pili ya kuendeleza mpango huu. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu unaweza kulieleza Bunge hili tathmini ya kiumla ambayo Serikali yako imeweza kufanya kufuatia mpango huu?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu maelezo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kipindi hiki sikipendi sana. Swali la Mheshimiwa Rajab ni zuri sana. Lakini kunitegemea kwamba naweza kuwa na kila jibu kwa kila swali ni ngumu. Angeniuma sikio jambo hili, swali zuri, ningekufanyia kazi nzuri na ningekupa jibu zuri sana. Sasa labda nikuahidi tu kwa sababu *Open Government Partnership* ni moja tu kati ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

njia mbalimbali ambazo nchi yetu imeamua kuzitumia katika kujaribu kufanya shughuli za Serikali ziweze kuendeshwa kwa uwazi.

Lakini utakumbuka vile vile kwamba sisi vile vile ni sehemu ya maamuzi ya msingi juu ya kitu tunaita APRM ambayo nayo ni namna nyingine ya kufanya Taifa letu tuendeleo kuangaliwa na mtu yoyote anayetaka kutuangualia aone tunaendeshaje shughuli zetu ili Watanzania waweze kuridhika na utendaji na uendeshaji wa shughuli za Serikali. (Makofi)

Ninachoweza kukuambia tu kwa ufupi ni kwamba chini ya mpango huo umeshirikiana sana na nchi mbalimbali wadau wa maendeleo. Tulichokuwa tunafanya katika awamu ile ya kwanza, ni kuweka misingi ya namna tutakavyokuwa tunashirikiana na kuendesha shughuli juu ya mpango huu. Mpaka sasa tunachofanya ni kujaribu kuona kwamba mambo gani lazima tuyafanye wazi wazi. Ndiyo maana utaona tulifika mahali hata Bajeti hii sasa tunaiweka kwenye mitandao tu ili kila mmoja aweze kujua kinachoendelea ni nini.

Tumeamua vile vile katika Serikali yetu Wizara zote kila moja iwe na utaratibu wa kutoa taarifa kwenye mtandao ili mtu yoyote anayetaka kujua kinaendelea nini aweze kufanya hivyo na hili jambo tunaendelea nalo kwa nguvu sana na ndiyo maana tunajaribu kuomba hata Bunge hili katika maeneo mengine utakuta hatuna ugomvi nalo ninaposema ni sehemu ya *Open Government Partnership* tunataka na hiki nikiweze wazi na hiki nikiweze wazi, tunakubali.

Kwa hiyo, ningekuwa nimejiandaa vizuri pengine kwa maana ya tathmini Mheshimiwa Rajab ningekuletea hata pengine na takwimu na maeneo mengine lakini ni swali zuri sana. Lakini nitaomba tu wenzangu kwa sababu na wenyewe wapo hapa pengine tuje tutoe Kauli ya Serikali Kwa ajili ya jambo hili na hata ile APRM ili muweze kuona kiasi gani Serikali tumejitahidi katika kujaribu kuweka mambo yetu kuwa wazi. Nadhani itasaidia zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Rajab bado una swali lingine la nyongeza?

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu kwa kweli kajibu vizuri na ameonyesha namna gani ambavyo Serikali itataka kufanya shughuli zake kwa uwazi. Nikiri kabisa kwamba moja ya maeneo ambayo Serikali inafanya shughuli zake kwa uwazi ni suala la Taarifa za CAG kwamba sasa hivi linajadiliwa katika Bunge, katika Mabaraza ya Madiwani na hata katika maeneo mengine.

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu moja ya kati ya tatizo ambalo linaonekana ni Serikali kutokujibu taarifa au mapendekezo ya Ukaguzi ama kwa wakati ama kutokujibu kabisa. Huoni kwamba kutokujibu au kutetereka kwa Serikali yako kutoa maelezo ama majibu ya mapendekezo yale ya ukaguzi kwamba kutaweza kuifanya hii dhana ya uwazi kutetereka katika uso wa dunia kuonekana kana kwamba hamfanyi kazi kisawa sawa?

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwa namna Sheria ile ilivyo hakuna uwezekano wa sisi kutokujibu hoja yoyote ya CAG, hakuna. Nataka nikuhakikishie tu kwamba ndiyo maana tuliwahi kuja hapa na mapendekezo mbele ya Bunge kuomba kwamba ili Wabunge muweze kujua kwamba hatukaidi maagizo ya CAG, hebu tuweke katika Sheria ile kipengele kinachoonyesha Serikali na ninyi mmeshughulikia vipi hoja zote za CAG.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Maana tumekuwa tukiandaa tunayapeleka kimya kimya huko Wabunge wanakuwa hawajui kwamba na sisi tumeshajibu zile hoja. Sasa bahati nzuri naona kamakimsingi lilikubaliwa na Mheshimiwa Lukuvi ameshaanza hiyo kazi vizuri.

Pengine tunachoweza kufanya kukazania sasa na sisi tuwe tunatoa kijitabu, wakati yeye anaandaa na kukamilisha lile zoezi lake na sisi tuweke kijitabu cha kila jibu kwa kila hoja ili muone namna tulivyojitahidi.

Lakini nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Rajab ndiyo maana leo hatuna hati chafu hata moja. Ndiyo, ni kwa sababu ya jitihada hizo. Lakini nakubaliana na wewe kabisa kwamba lazima tufike mahali na nyinyi muone kwamba sisi si watovu wa nidhamu.

Kwa hiyo, nitamwambia Mheshimiwa Lukuvi pengine tulikazanie hilo ili mpate vijitabu vile muweze kuona tunavyojitahidi.

SPIKA: Huwa vinagawiwa, lakini nadhani wengi hawavilili maanani. Labda tuangalie utaratibu mwingine wa kuwasilisha. Nadhani hiyo itasaidia. Tunao, mwaka janatulipewa, na mwaka juzi tulipewa. Tuligawa. Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kipindi cha miaka ya 1990 mpaka kufikia miaka hii ya elfu mbili, Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuweza kuchochea uwekezaji ili kuweza kukuza uchumi na kutoa matokeo ambayo yanaweza yakasaidia pia hali za jamii zetu. Matokeo ya uwekezaji huu hivi sasa yanaelekea kuwa ni chungu kwa Watanzania.

Kwa mfano, kuna malalamiko makubwa sana kwamba misamaha ya kodi imekuwa ikitumika vibaya matokeo yake Serikali inakuwa inapoteza mapato na hainuifai na uwekezaji uliotokea. Nini kauli ya Serikali katika kuondoa changamoto hizi ambazo zinaonyesha sasa zinaweza zikaathiri uchumi wetu?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Mangungu linaweza kuwa na ukweli kiasi fulani. Lakini mimi nadhani kazi yangu iwe zaidi kueleza ni maeneo yapi ambayo na sisi tunafikiri ni vizuri kwa pamoja tukaona namna ya kuyafanyia kazi na kuyarekebisha. Msingi wa msamaha, ambao kwetu ni wa msingi kabisa ni pale unapotoa msamaha kwa mwekezaji kwa kuwa unajua ndani ya miaka 10 ijayo matokeo yake yatakuwa na *impact* kubwa zaidi kwa jamii katika maendeleo ya watu.

Kwa hiyo, unasamehe leo ili baadaye uje unufaike zaidi. Hilo ndiyo jambo kubwa katika uwekezaji. Sasa ni kweli inawezekana kabisa katika msamaha huo usimamizi wake ukawa si makini sana na wakati mwingine mtu akapewa msamaha akautumia vibaya. Hilo linawezekana.

Lakini jitihada ambazo tumefanya hasa kwa wawekezaji wengi ambao tumekuwa tukiwapa msamaha ni kuhakikisha kwamba TRA pamoja na vyombo vingine vinakuwa na utaratibu wa kufuatilia kwa karibu sana namna wanavyotumia ile misamaha. Lakini misamaha kwa ajili ya wawekezaji lengo ni zuri na ni vizuri tukaendeleza namna ya kuimarisha.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Lakini uko msamaha mwingine ambao unakuta unatokana na mazingira ya muda mfupi na hasa inapotokea kwamba bei za vitu zimepanda sana. Mara nyingine Serikali inalazimika kuruhusu ili bei zile ziwe za kuteremka ili *inflation* ile isitusumbue.

Lakini hii kwa kweli inapaswa kuwa ni kitu cha muda mfupi sana baada ya pale mnaendelea na utaratibu kama kawaida. Lakini na sisi upande wa Serikali Mheshimiwa Spika, eneo hili tumelitazama kwa upana sana na ndiyo maana utaona katika sheria ambayo mtatusaidia hapa kutuongoza tumejaribu vile vile kuja na mawazo ya baadhi ya maeneo ambayo tunafikiri si lazima yakapewa msamaha.

Kwa hiyo tumekuja na mapendekezo hayo kwenye hiyo Sheria nadhani kwenye mjadala utakaofanyika hapa mwisho wa Bunge, Wabunge watapata nafasi ya kushauri vizuri zaidi maeneo yapi tuweze kuendelea nayo. Yapi pengine tusamehe kidogo na kadhalika na kadhalika.

Lakini mwisho niseme tu kwamba hofu niliyonayo mimi kwenye misamaha mingine ambayo tunaitoa sasa ni pale ambapo inaua jitihada za ndani za watu wanaotaka kuwekeza katika viwanda. Maana viwanda ndiyo vitatupa ajira. Viwanda ndiyo vitatupa bidhaa.

Sasa msamaha wowote ambao unaua kabisa jitihada hizi ni lazima wote kwa pamoja tuone kwamba msamaha huu hauna tija. Ndiyo maana umeona tumekuwa tukija na mapendekezo juu ya ngozi, viwanda vya ndani. Nguo kwa mfano, viwanda vya nguo, tutaagiza kanga mpaka lini? Kwa nini tusiwe na utaratibu wa vitu vingine kuvikataa kuvipiga ushuru mkubwa ili viwanda vya ndani viweze kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Tuna viwanda vya sukari. Tungalipenda viendeleo kuzalisha sukari hapa nchini. Lakini kwa nini tuendeleo kuagiza sukari kutoka nje kama tunaweza kujenga uwezo wa ndani. Hali kadhalika saruji tungependa tuwe na viwanda vyetu hapa. Kwa sababu heshima ya nchi kwa kweli ni kuwa na viwanda vyenu ninyi wenyewe.

Kwa hiyo, misamaha hii ni dhahiri kwamba tuiangalie kwa upana katika kulinda viwanda vyetu vya ndani na kama si lazima kuwa nao bora maana yake nini? Ili mradi tuweze kuianisha kati ya uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa zenyewe. Kwa hiyo ni suala la msingi na mimi nakubaliana naye lakini Sheria ikija mtatungalia vizuri zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Mangungu, swali moja fupi.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Nashukurisana. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mmoja kati ya watu makini sana nilioweza kuwafahamu duniani. Ningependa nikuulize moja kati ya matokeo ambayo tulitarajia baada ya uwekezaji huu ni kukuza ajira na kutoa matokeo mengine ya kusaidia Sekta nyingine za kiuchumi.

Hivi sasa kumekuwa na wimbi kubwa la watu kutoka nje kuvamia hapa kupata ajira katika hao wawekezaji ambao tunawapa kwa sababu tunawapa na fursa ya kuingiza watumishi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Watanzania wanakosa ajira na Serikali inatumia pesa nyingi kusomesha Watanzania. Vile vile utoaji wa leseni kwa biashara ambazo Watanzania wanaweza kufanya hata maduka wanapewa watu wa nje. Sasa hili unalichukuliaje Mheshimiwa Waziri Mkuu? Na unatoa tamko gani la Serikali. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu maelezo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, biashara. Ni kweli katika baadhi ya maeneo wako walioruhusiwa kufanya biashara. Lakini nataka niseme kwamba hiyo yote inatokana na mwanya. Unajua mkiwa na Taifa ambalo linaelekea kufanya uchuuzi zaidi hawa hamtawakwepa. Lazima watakuja tu. Kwa hiyo, dawa hapa ni sisi kujikita katika uzalishaji wetu wa ndani ambao utakuwa sasa unamilikiwa na Watanzania wenyewe na biashara itafanywa na wao wenyewe.

Sasa hivi *tendency* za wengi ni hizo bidhaa kuagiza kutoka China, kutoka sijui India. Sijui kutoka wapi? Sasa wale wanajua kumbe huku hamna hivi vitu. Kwa hiyo, na wenyewe wanajichomekea hapo. Kwa hiyo, mnakuwa na biashara za maua, biashara sijui za nini.

Sasa mimi nadhani kubwa hapa tujikite zaidi katika jambo la msingi la viwanda kuzalisha bidhaa hapa ndani na ndiyo maana mimi rai yangu bado kwa wenzangu wote hata wale wanaotaka kuja kufanya biashara hapa ni kuwabana tu kama unataka biashara, jenga viwanda, zalisha hapa. Hapo tutaelewana. Hapo tutaelewana, lakini vinginevyo hapana.

La pili ambalo Mheshimiwa Mangungu, amelisema ni pale ambapo mnakuwa na watu kutoka nje kuja kufanya kazi hapa nchini kwa wingi kwa vingizio mbalimbali. Ninachoweza kusema tu Mheshimiwa Spika, tunajitahidi sana hili jambo kwa sababu na mimi ni mdau mkubwa nalifuatilia sana. Wakati mwingine inatokana tu na ukweli wa aina ya uwekezaji wenyewe ulivyo. Ndiyo maana tunaruhusu kiasi fulani cha watu kutoka nje. Lakini vile vilena Watanzania wawepo.

Kwa hiyo, katika mifano michache niliyoiona ni kwa mfano mradi niliokwenda kutembelea kiwanda cha Dangote Mtwara, ni lazima tukubali kwamba turuhusu *component* fulani ya utaalum kwenye maeneo fulani fulani. Lakini nilichofarijika pale nimekuta Watanzania vile vile wako wengi sasa. Nimeangalia lile bomba la Mtwara linalojengwa, nimekuta kuna *component* ya Wachina pale. Lakini walio wengi ni Watanzania.

Kwa hiyo, tukienda na mtazamo huu kwangu mimi ndiyo mzuri zaidi kuliko pale ambapo tunaruhusu watu kiholela kuja kufanya kazi. Lakini naamini Wizara ya Kazi kwa sababu ndiyo wenye kazi hii na Idara ya Uhamiaji wataendelea kuwa makini ili tuhakikishe tunaruhusu watu wale tu ambao mahitaji yao ni ya lazima sana. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha na walioomba kuzungumza wameisha. Tukushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu ya maswali ya *all weather*. Lazima tukubali kabisa inakuwa kama ni *interview* hivi ya kupata kazi, maana yake, lakini tunakushukuru umejibu vizuri na maswali ya leo yamekuwa mazuri sana. Kwa hiyo, tunataka

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kujibu vizuri. Katibu tunaendelea. (Makofi)

MASWALI YA KAWAIDA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali ya kawaida tunaenda Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, atauliza swali la kwanza.

Na. 236

Mzozo Kuhusu Maeneo ya Wakulima na Wafugaji

MHE. RASHID ALI ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kipindi kirefu sana kumejitokeza mizozo baina ya Wakulima na Wafugaji kuhusu maeneo ya kulima na ufugaji:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kuondoa tatizo hili kwa Wakulima na Wafugaji?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa kutokutatua tatizo hili kunaweza kudhoofisha uchumi wa Taifa letu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika kipindi kirefu sasa kumekuwako na mizozo baina ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mpango uliopo wa uhakika wa Serikali wa kuondoa tatizo la wakulima na wafugaji ni kuhakikisha kuwa kila Halmashauri inakuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi yaani *Land Use Plan*. Mpango ambayo unacinisha maeneo kwa ajili ya wafugaji, wakulima, wawekezaji na shughuli nyingine.

Hivyo, Serikali imeendelea imehimiza Halmashauri zote nchini kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kutenga maeneo ya ufugaji kwa ajili ya kuendeleza malisho ya mifugo katika Halmashauri zote.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba migogoro ya aina hii isipodhibitiwa inaweza kudhoofisha uchumi wa Taifa letu. Hata hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI imekusanya na kuunganisha taarifa za migogoro ya ardhi kutoka kwenye Mikoa yote ili kuitafutia ufumbuzi.

Vile vile Mheshimiwa Waziri Mkuu ameagiza Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kukutana na kujadiliana namna nzuri ya kuzuia migogoro ya aina hii.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mkutano huu umepangwa kufanyika mwezi Julai mwaka 2014. Hatua hii itasaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi kuhusiana na utatuzi wa migogoro iliyopo na hivyo kuzuia kudhoofika kwa uchumi wa Taifa letu. (Makofi)

MHE. RASHID ALLI ABDALLAH: Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Baada ya majibu hayo nina maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi, yamesababisha mauaji ya wakulima na wafugaji katika sehemu mbalimbali za nchi hii. Kwa mfano kule Singida, Iringa, Arusha, Dodoma na Morogoro hasa maeneo ya Kiteto na Mvomero.

Mheshimiwa Spika, kwa vyanzo vya habari na maelezo mbalimbali inaonekana kwamba mauaji haya yaliyotokea kule Mvomero na Kiteto yamesababishwa kwa kiasi kikubwa na uongozi wa Wilaya kule Kiteto.

Je, Serikali hadi sasa imechukua hatua gani za kisheria dhidi ya uongozi huu ambao wamesababisha mauaji ya wakulima na wafugaji?

Je, Mheshimiwa huoni kwamba kuibuka kwa vitendo hivi katika sehemu mbalimbali ni aibu kwa Taifa hili, hasa linalofuata utawala bora katika hatua ile ya uwajibikaji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa tumejieleza hapa na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anajibu maswali hapa, mmesikia jitihada ambazo tunazifanya kwa maana ya kuhakikisha kwamba, tunaondoa migogoro hii ambayo imekuwa inajitokeza katika Taifa letu. Sisi kwa upande wetu tumepokea maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yanayotutaka Wizara hizo nilizotaja hapa tuweze kukutana na kuweza kuona matatizo haya yaliyopo yanaondoka na hayatakuwepo tena.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anazungumza kuhusu matukio mbalimbali ambayo yametokea katika Taifa letu na watu wamepoteza maisha, jambo ambalo sisi wote hatuwezi kufurahi kwamba, jambo hilo linatokea, tunajisikia vibaya kwamba, limetokea.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie, na nimejibu tena hapa, tulichofanya sisi sasahivi ni kwamba, tumeigiza mikoa yote Tanzania nzima na Wilaya zetu na Halmashauri zetu zituletee matatizo yote ambayo yamekuwa yanatokea katika Halmashauri zetu na katika Mikoa yetu, ili tuweze kuchambua na kuangalia kwamba, kiini cha matatizo haya yanatokana na nini. Kwa hiyo, katika zoezi hili ndipo tunaweza tukabaini hata hili analozungumza la Mvomero, ili kuweza kujua kwamba, tatizo limekuwa wapi? Hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Spika, tumefanya hiyo kazi Mkoa kwa Mkoa, Halmashauri kwa Halmashauri. Kwa hiyo, siwezi kusema hapa sasa kwamba, ni kweli, limekuwa hivyo, katika uchambuzi huo ndio tunaweza tukajua.

Mheshimiwa Spika, pili. Anazungumza habari ya *Good Governance*; utawala bora ni utawala ambao unafuata Sheria na taratibu za nchi, ndivyo ninavyoelewa mimi. Na ukienda kinyume cha hivyo, utakuwa na matatizo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, anasema weka mpango wa Matumizi Bora ya ardhi. Ukisema hapa pawe ni kwa ajili ya kilimo, ni kwa ajili ya kilimo. Ukisema hapa ni kwa ajili ya mifugo, basi pawe ni kwa ajili ya mifugo. Hapa ni kwa ajili ya watoto kubemba, hapa pawe ni mahali pa kubemba *that is the bottom line.* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivyo tutapata matatizo. Ndio maana ukisoma Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ukiangalia mle ndani, Waziri anaeleza maeneo ambayo sasa tunaanza. Amezungumzia habari ya Wilaya tisa (9) ambazo zitaanza kufanyiwa huo utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya mifugo na kadhalika, ametaja humu ndani. Ukimsikiliza Profesa Anna Tibaijuka, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na yeye anazungumza habari hiyo hiyo.

Kwa hiyo, kwa jitihada hizi nategemea kwamba, matatizo haya yatakuwa yameondoka. (Makofi)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, maeneo ya wafugaji wakulima wanaona kwamba, ni maeneo ya wazi ambayo hayana matumizi.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kuweka Hatimiliki maeneo yote ya wafugaji ya malisho, ili wakulima wasiyavamie tena?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Kaka yangu Michael Lekule Laizer na jirani yangu katika Wilaya ya Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ardhi hii tunayozungumza hapa, tunazungumzia matumizi bora, ikipimwa ukisema hapa ni kwa ajili ya wafugaji, unawapa na Hatimiliki kabisa wanakuwa na Hati yao kwamba, hapa ndipo watakapokuwa wanachunga ng'ombe na ndipo watakapokuwa wanapatumia. Na hivyo hivyo kwa ajili ya wakulima na hivyohivyo kwa ajili ya *activities* nyingine zote ambazo tumeeleza hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nikubaliane naye Ndugu yangu Mheshimiwa Michael Lekule Laizer kwamba, wafugaji ni lazima useme eneo la kwenu ni hili hapa. Tukishasema eneo hili ni kwa ajili ya wafugaji asitoke tena mtu kule mkulima kwenda kulima katika lile eneo pale, ndicho kinachozungumzwa hapo. Tusipofanya hivyo ugomvi huu hautakwisha kule Kilosa, mchezo ni huo huo unasikiliza sasa akina Asumpter Mshama nao wanazungumza ni habari hiyo hiyo, nchi nzima ni hivyo hivyo.

Kwa hiyo mimi nadhani nakubaliana na wewe kabisa kwamba, iko haja ya kuweka Hatimiliki kwa ajili ya wafugaji, ili wasije wakasumbuliwa. (Makofi)

Na. 237

**Kujaa Tope Eneo la Malindi Wharf Katika
Bandari ya Dar es Salaam**

Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JAKU HASHIM AYOUB aliuliza:-

Kumekuwa na kero ya muda mrefu inayotokana na hali ya kujaa tope kwenye eneo la *Malindi Wharf* katika Bandari ya Dar es Salaam licha ya kodi nyingi zinazokusanywa Bandarini hapo:-

(a) Je, Serikali inatoa Kauli gani juu ya kasoro hiyo?

(b) Je, malipo yanayotozwa watumiaji wa Bandari yanatumikaje, ikiwa hali ya Bandari inazidi kuwa mbaya, hasa nyakati za mvua?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inalitambua tatizo hilo la maji kutuama na tope kujaa katika eneo la *Malindi Wharf* nyakati za mvua. Tatizo hili linatokana na miundombinu chakavu ya kuelekeza na kudhibiti maji ya mvua yasituame na kutawanyika hovyo eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kukarabati miundombinu ya maji na eneo lote la *Malindi Wharf* kwa ujumla tumeusitisha kufwatia uamuzi wa TPA kujenga Gati 2 mpya maalum za kisasa kwa njia ya PPP ambazo zitachukua eneo kubwa la *Malindi Wharf* Shughuli zinazofanyika *Malindi Wharf* kwa sasa zitahamishiwa eneo lingine muafaka ndani ya Bandari.

(b) Mheshimiwa Spika, eneo la *Malindi Wharf* ni moja tu ya maeneo kadhaa yanayosimamiwa na TPA na ambayo, kwa sehemu kubwa, yameboreshwa na yanaendelea kuboreshwa kulingana na maendeleo ya sasa ya uchukuzi kwa kutumia mapato ya Bandari.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. pamoja na majibu mazuri sana na ya kutia moyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Charles Tizeba, naomba kuuliza maswai madogo mawili ya ziada:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hivi sasa eneo hilo linaendelea kutumika na linakusanya kodi karibu tatu (3) na huduma nyingine pale wanachangishwa wananchi wakati huduma hizo wakiwa hawazipati, ingawa kuna mpango wa kuendelea na eneo la ujenzi, kuna hatua gani ya dharura ya kutatua tatizo hilo kwa wananchi haraka?

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaonaje au inatathmini vipi afya za walipa kodi katika eneo hilo?

Ukizingatia wakati wa jua pana mavumbi yanaruka vibaya na kazi kusimama kwa muda?

Wakati wa mvua huwa kiama kabisa, hutoa matope na maji na kusababisha hata hatari ya kutokea homa ile ya dengue?

SPIKA: Aah, unataka kututisha sisi na homa ya dengue? (Makofi/Kicheko)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hashim Jaku, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, baada ya tatizo hilo kuwa limekwishaonekana pale *Malindi Wharf*, Serikali ilikwishaigiza Mamlaka ya Bandari kuchukua hatua za haraka, ili kuhakikisha kwamba, watumiaji wa sasa wa eneo hilo hawapati adha hiyo wanayoisema ya tope na maji kutuama pale wakati mvua zinanyesha.

Maelekezo yaliyotolewa ni kwamba, *TPA* kwanza wakatie mifereji ya kuinga maji yale yanayoteremkia pale, inaitwa mifereji ya kuinga maji, lakini pia wapeleke *moram* na juu yake waweke kokoto ndogo sana zinazotokana na mawe yaliyosagwa, ili kuhakikisha kwamba, mvua zinaponyesha sehemu hiyo haijai maji na haiwi na tope kama ilivyo sasa. (*Makofi*)

Na. 238

Kulifufua Shirika la Ndege la ATCL Nchini

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA aliuliza:-

Shirika la Ndege la *ATCL* ni kitendawili na imeonekana hakujawa na mpango kabambe wa kulifufua; na hivi karibuni tulisikia yupo Mwarabu kutoka Oman ambaye yuko tayari kuwekeza kiasi cha dola milioni mia moja (*100,000,000 USD*) kwa ajili ya kulifufua Shirika hilo.

Je, suala la mwekezaji huyo kutaka kuwekeza katika Shirika hilo la Ndege limefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, naomba kutoa maelezo yafwatayo:-

Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu Swali la Msingi tarehe 17 June, mwaka jana kwenye Mkutano wa 8 wa Bunge la Bajeti, kuhusu Mwekezaji kutoka Oman, nilieleza kuwa, Serikali ilikuwa imefanya mazungumzo ya awali na Mwekezaji huyo wa Oman. Nilitieleza kuwa, Mwekezaji huyo alionyesha nia ya kuwekeza ndaninya Kampuni ya Ndege ya *ATCL* kiasi cha Dola milioni mia mpoja za Marekani na kwamba, majadiliano kati ya Serikali na Mwekezaji yalikuwa hayajakamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mazungumzo kati ya Serikali na Wawekezaji mbalimbali, akiwemo Mwekezaji huyo kutoka Oman, yatakamilika mara baada ya mchakato wa kusafisha mizania ya *ATCL* utakapoisha kwa madeni ya *ATCL* yanayofikia shilingi bilioni 133 kuchukuliwa na Serikali na kuyaweke utaratibu maalum wa kuyahakiki, kuyajadili na wadai na kuyalipa, huku *ATCL*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ikianza upya shughuli zake bila mzigo wa madeni. Wizara ilishawasilisha Serikalini Mpango Mkakati (*Business Plan*) wa kuifufua ATCL ambao uko hatua za mwisho kuridhiwa na vyombo husika vya Serikali.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, kumekuwa na tabia hii ya upembuzi yakinifu, mchakato unaendelea, mchakato upo katika hatua za mwisho. Tunachotaka kujua hapa ni lini deni hili la bilioni 133 litabebwa na Serikali, ili Mheshimiwa Waziri kama alivyotutamkia hapa katika Hotuba yake ya Bajeti kwamba, ana uwezo wa kuleta ndege 4 hadi 5 kuongezea nguvu ya shirika hili, lakini kilichokuwepo ni kulipwa kwa deni hili; ni lini deni hili litalipwa, tupewe *particular time* baada ya mwezi, mwaka, miaka?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; tulikuwa na ndege mbili za *Boeing 737* na hizi zilikuwa zina-*operate* mpaka *regional* na zilisaidia sana na bado zinaonekana hazijachakaa. Ndege hizi *Boeing 737* ziko wapi au zimepotea kama ile ndege ya Malaysia? (*Makofi*)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana kwa maswali ya Mheshimiwa Sanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshaeleza kwamba, tumetengeneza *Business Plan*. Hiyo *Business Plan* tumeiwasilisha Serikalini na vyombo husika vya Serikali viko hatua za mwisho kujadili na kuweza kupitisha, hatuwezi kutumia njia nyingine hii dunia leo ni ya Sayansi na Teknolojia. Nina uhakika mapema iwezekanavyo tutafikia hatua hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu ndege *Boeing 737*, naona toka jana unaniulizia hizo ndege, sijui unazipenda kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, hizo ndege zimepitwa na muda wake. Tukiingia sisi tukisafishiwa hiyo mizania yetu tutakuja na ndege mpya, sio hiyo unayozungumzia. (*Makofi*)

MHE. RACHEL R. MASHISHANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru; kuna ndege *Boeing 737* iko Mwanza ilipata ajali. Sijajua hatma ya ile ndege mpaka sasa, naomba kujua?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mashishanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba, ile ndege baada ya kupata ajali iliyotokea, shirika lililokuwa limeiwekea bima ndege hiyo lililipa bima kwa wamiliki wa ndege na ndege hiyo sasa inamilikiwa na shirika hilo la bima ambalo walilipia bima ambayo walikuwa wameiwekea ndege hiyo. Kwa hivyo, ni suala la wenye bima wale ambao ndio wamiliki wake wa sasa kujua wanataka kufanya nini na ndege hiyo.

SPIKA: Eeh, niwafuate ambao huwa hawasimami. Mheshimiwa Riziki?

MHE. RIZIKI O. LULIDA: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru; naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, swali moja:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, mashirika haya ya nje, kama vile *Emirates, Qatar Air, Oman Air*, huwa zinavuna, zinapata abiria wengi na kukusanya fedha nyingi.

Je, kati ya hizo ndege ambazo Mheshimiwa Waziri anatarajia kuzileta pindi yatakapomaliza kulipwa hayo madeni, kuna ndege ambazo zitakuwa zikisafirisha abiria kwenda Oman na Dubai? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, hatusomi maswali. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Riziki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hapa swali la nyongeza amesema kwamba, imeandaliwa *Business Plan* ambayo hiyo ikisharidhiwa *then* litafwatia suala la kuondokana na hilo deni na wabia mbalimbali wanaotaka kujiunga na *ATCL* hapo ndipo watapata nafasi nzuri ya ku-join na *ATCL* kuifufua kama tunavyotarajia. Ndege hizi zitakapopatikana zitakwenda mahali kote ambako kutakuwa na biashara yenye tija. Sasa itakuwa Dubai, itakuwa Oman, itakuwa London, itakuwa Johannesburg, kote kule zitakwenda *as long as* safari hizo zitakuwa na manufaa kwa Shirika lenyewe. (*Makofi*)

Na. 239

Wakulima wa Kakao Kupatiwa Wataalamu na Kiwanda cha Zao Hilo

MHE. CYNTHIA H. NGOYE aliuliza:-

Zao la kakao ni malighafi muhimu kwa utengenezaji wa *Chocolate* na hulimwa kama zao la biashara katika Wilaya za Kyela na Rungwe:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wakulima wa zao hilo Wataalamu wa Ushauri, ili kuongeza uzalishaji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha ujenzi wa Kiwanda cha *Chocolate* katika maeneo hayo, ili kuleta soko la zao hilo na kukuza Sekta ya Viwanda nchini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, Mbeya, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa zao la kakao katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu na imeendelea kuajiri Maafisa Ugani, ili kufikisha utaalumu na teknolojia mbalimbali za kilimo bora kwa wakulima nchini, wakiwemo wakulima wa zao hilo la kakao katika Wilaya za Rungwe na Kyela.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *TECHNO-SERVE* imetoa mafunzo maalum kuhusu uzalishaji, usindikaji na masoko ya zao la kakao kwa wakulima 7,634 katika Wilaya za Kyela, Rungwe na Kilombero. Mafunzo maalum pia, yametolewa kwa Wataalamu 65

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutoka Wilaya hizo ili kuwasaidia wakulima mbinu za uzalishaji bora, usindikaji pamoja na kuwaunganisha na masoko ya zao la kakao.

Aidha, Halmashauri za Wilaya zinazolima kakao zimehamasishwa kutenga fedha kupitia mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya (DADPS) kwa ajili ya kuwapatia Wataalamu wake mafunzo rejea kuhusu uzalishaji wa kakao, ili kuimarisha uwezo wa Maafisa Ugani waliopo katika kuhudumia wakulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa zao la kakao inaandaa mkakati wa kuendeleza zao la kakao nchini, wenye lengo la kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 8,000 kwa sasa hadi kufikia tani 30,000 mwaka 2023. Maeneo ya kipaumbele ni kuongeza tija, uzalishaji na ubora wa kokoa, kuhamasisha masoko ya ndani na nje ya nchi na kuhamasisha ulaji wa bidhaa za kakao. Kuimarisha utafiti na uenezaji wa teknolojia za kakao na kuhamasisha wadau kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa zao la kakao.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuandaa mazingira ya soko la uhakika kwa zao la kakao na kuzingatia ukweli kuwa kakao inayozalishwa Wilayani Kyela na Rungwe ina ubora mkubwa na inazalishwa bila kutumia kemikali kama mbolea na madawa (Organic) Serikali kwa kushirikiana na wadau, likiwemo Shirika la *TECHNO-SERVE* itaendelea kuhamasisha wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza *chocolate*.

Katika utekelezaji wa mkakati huo Kampuni ya *Mamas Chocolate Ltd.* ya Jijini Dar-es-Salaam imeanza kununua kokoa kutoka Kyela na kuanza kutengeneza *choklate*.

Aidha, mkakati wa Serikali ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo nchini, ikiwemo zao la kokoa, kabla ya kuuzwa nje, ili kuongeza thamani na hivyo, kuwapatia wakulima mapato mazuri. (Makofi)

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Spika, asante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; katika Swali langu la Msingi niliomba kujengewa kiwanda cha kusindika kakao katika Wilaya zalishaji maarufu kwa zao la kakao katika Wilaya za Rungwe na Kyela; lakini katika jibu lake anaonesha kwamba, kiwanda hiki cha *Mamas Chocolate Ltd.* kinafanya mkakati wa kujenga kiwanda hicho Dar-es-Salaam.

Je, Waziri au Serikali kwa ujumla haiwezi ikaishawishi kampuni hii kuwekeza na kujenga kiwanda hicho katika Wilaya hizi mbili nilizozitaja? Ili kupunguza gharama na vilevile kuongeza ajira kwa vijana wa Wilaya hizo nilizozitaja? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Makampuni yanayonunua kakao katika Wilaya hizi yanafanya hivyo kiholela kabisa na bei zao ni za chini kabisa kwa madai kwamba, zao hilo lina thamani ndogo; lakini tatizo ninaloliona mimi ni kwamba, hakuna Bodi maalum inayosimamia zao hili.

Je, Serikali sasa iko tayari kuunda Bodi Maalum ambayo itasimamia utaratibu mzuri wa kuendesha uzalishaji na mauzo ya zao hili?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa viti Maalum Mbeya, kama ifuatavyo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mmiliki wa kiwanda cha Mamas anatarajia kujenga kiwanda cha Kakao kule Dar es Salaam lakini nikubaliane na rai ya Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawashauri wawekezaji waone umuhimu wa kuwekeza au kuweka viwanda katika maeneo ambako zile bidhaa zinazalishwa ili pia kuweza kuwapatia ajira wananchi wa maeneo hayo na kwa maana hiyo waone pia umuhimu wa kulima mazao hayo. Hili ni suala la ushauri ingawa kimsingi pia hatuwezi kuwalazimisha sana. Lakini tutaendelea na kazi ya kuwashauri waone umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Mbunge nataka nikubaliane naye kwamba ununuzi wa zao la kakao na kwa sababu pia mimi natoka Mbeya nafahamu zao lile. Pia hivi karibuni nilitembelea Kyela, ni kweli soko lake haliko vizuri sana.

Ni kweli pia, tukiri kwamba mazao mengi katika nchi yetu bado ununuzi wake hauko sawasawa. Mara nyingi wanunuzi wamekuwa wakiwadhulumu wakulima kwa sehemu kubwa sana. Hili Serikali imelitambua na ndiyo sababu sasa tumeshaanzisha utaratibu wa stakabadhi ya mazao ghalani.

Pia Waheshimiwa Wabunge wanajua utaratibu huu umesaidia sana kwa maana ya wakulima kuwa na nguvu ya pamoja, wanapokusanya mazao yao sehemu moja wakisubiri bei ya mazao kuwa nzuri. Lakini tumeenda hatua mbele zaidi kwamba tunaanzia sasa utaratibu wa kuanzisha soko la mazao na bidhaa yaani *Commodity Exchange* na tukishafanya hivyo kwa mazao mengi maana yake wakulima watakuwa na nguvu kubwa zaidi na mazao yale yatauzwa kwa utaratibu kama vile yako mnadani.

Kwa hiyo, tukifika hapo tunafikiri hatutakuwa hata pengine na sababu ya kuwa na Bodi nyingi kwa sababu tukishakuwa na chombo hiki nadhani kinaweza kikasaidia sana kuhakikisha kwamba wakulima wanauza mazao yao kwa bei iliyo nzuri na bora zaidi. *(Makofi)*

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kakao ni malighafi kama walivyo samaki na kwa kuwa Ziwa Nyasa lina samaki wengi na kwa kuwa Rais aliyeingia madarakani sasa hivi huko Malawi ametangaza msimamo wake bayana kwamba yeye mgogoro wake na Tanzania uko pale pale na gazeti la Mwananchi la wiki iliyopita limemnukuu kwa kauli hiyo.

Naomba kupata kauli ya Serikali itakayowapa faraja wananchi wa Ludewa, kule Manda, Lupingu na Ziwa Nyasa kote namna gani tunamaliza kwa amani mgogoro huu wa Ziwa Nyasa na Tanzania. *(Makofi)*

SPIKA: Yaani linakataa ku-*fit* hilo swali, linakataa kabisa ku-*fit* yaani limekataa hata kama ni kutudanganya. Waheshimiwa Wabunge basi na muda umeisha msije mkaniuliza mengine yasiyo-*fit* in. Ahsanteni sana wamesikia wanaohusika watakujibu baadaye lakini kwa hapa hai-*fit*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge niwatambue wageni, baadhi ya wageni ambao wako humu ndani. Waheshimiwa Wabunge tunao wageni, tunao mabalozi ambao wapo kwa ajili ya kutusikiliza mpango *I will introduce you in the afternoon, I think we will have a better organized list of your participation so I will introduce you in the afternoon.*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge kuna wageni 85 wa Mheshimiwa Deo Filikunjombe wakiongozwa na Wenyeviti wa CCM Kata 25 Ludewa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stanley Kolimba, naomba Mwenyekiti Stanley Kolimba asimame alipo. Mheshimiwa Kolimba alishakuwa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mbunge hapa kwa vipindi zaidi ya viwili. Halafu wako Makatibu kata 25 wasimame walipo, halafu Makatibu wa CCM wote kutoka Ludewa wakiongozwa na Katibu wa Wilaya hiyo wasimame Makatibu wote hao, kuna Makatibu waenezi na wenyewe wasimame.

Sasa yuko Katibu mwenezi wa MKoa Bwana Honoratus Mgaya asimame na yuko Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Njombe Mheshimiwa Rosemary Lwiva na wako waandishi wa Habari na Wauguzi wote wapo hapo. Kwa hiyo, Mbunge wenu ameuliza swali silo lakini lilikuwa la maana lakini halikuwa lenyewe.

Tuna wageni 26 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji na Uwezeshaji ni Wachungaji wa Makanisa ya PAG kutoka Wilaya ya Hanang, naomba Wachungaji hawa wasimame walipo wako kule nyuma.

Tuna wageni tisa (9) wa Mheshimiwa Stephen Wassira Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu ambao ni viongozi wakuu na hawa ni viongozi wote wakiongozwa na Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Rais Tume ya Mipango Dkt. Philip Isidori Mpango naomba Dkt. Philip Isidori Mpango asimame ahsante sana na wale wengine ni siku yao.

Kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Stephen Wassira ni wanafunzi 38 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, naomba wasimame kama wamepata nafasi, watakuja nafasi ilikosekana wamekosa nafasi.

Kuna wageni 74 wa Mheshimiwa Mwigulu Mchemba ambao ni wana kwaya ya Mtakatifu Thomas More Baraza Katoliki Chuo Kikuu - Mzumbe na viongozi wa wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe. Naomba hawa wasimame, kwaya kubwa kabisa na sisi tunajumuiya yetu inaitwa hivyo hivyo Thomas More hapa tunasali siku ya Jumatano tu.

Tuna wageni wanane (8) kutoka Ofisi ya Mkaguzi na Mdhidhi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) wakiongozwa na Ndugu Salome Mollel, hawa wako wapi kama wamepata nafasi, wako pale juu ahsanteni sana na karibuni.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, yupo Mwenyekiti Kenny Salvatory Festo na Katibu wake Meshack Jumanne Ngwesa, ahsante. Tunao wageni wa Mheshimiwa Haji Mponda, ambao ni wanafunzi 32 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na vijana kutoka jimbo la Ulanga na wenyewe wasimame kama wapo nafikiri nafasi haitoshi.

Kuna wageni kumi na tisa (19) wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, hawa ni Madiwani nao nasikia wataingia baadaye. Kuna wageni wa Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, ambao ni Ndugu Virginia Silayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya *Action for Justice in Society* na Ndugu Bernadeta Daniel Afisa Miradi wa Asasi ya *Action for Justice in Society* wako kule nyuma.

Kuna wageni 40 wa Mheshimiwa Devotha Likokola ambao ni Wanachama wa VICOBA kutoka Dar es Salaam tunamwona mmoja nadhani nafasi haiyo. Kuna wageni wa Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina ambao ni Ndugu Damian Mtihinda Katibu Mwenezi CCM Ngara na Ndugu Selemani Bunzia Mjumbe wa Halmashauri ya Wilaya CCM Ngara karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Aliko Kibona kutoka Mbeya wakiongozwa na Ndugu Obeid Cheyo wasimame hao kama wapo humu ndani halafu na wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 45 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma wasimame walipo kama wamepata nafasi, hawakupata nadhani wataingia mchana.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kuna wanafunzi 60 kutoka shule ya Sekondari Wailes Temeke - Dar es Salaam, kama wapo wasimame ahsante sana. Ahsanteni sana tunawatakiwa masomo mema karibuni sana Bungeni Dodoma. Tuna wanafunzi 70 na walimu sita (6) kutoka shule ya msingi Buigiri Mission na wenyewe wasimame walipo ahsanteni sana, karibuni sana. (Makofi)

Nasikia wageni wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba wapo, wako wapi wasimame, asanteni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge tumetumia muda mwingi sana kwa ajili ya kutangaza wageni siyo vizuri sana kwa niaba ya Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* Mheshimiwa Ritha Kabati anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba mazoezi ya mchezo wa mpira wa kikapu *Basketball* yatafanyika katika viwanja vya michezo vya chuo cha Elimu ya Biashara *CBE Campus* ya Dodoma kila siku kuanzia saa kumi na moja na nusu asubuhi hadi saa moja kamili asubuhi. Waheshimiwa Wabunge ambao wangependa kushiriki katika mazoezi hayo wnaombwa kufika katika viwanja hivyo kila siku asubuhi kwa muda uliotajwa. Waheshimiwa mnaombwa kushiriki hapo kama mnavyojua mkakati wa kupambana na matatizo ya *obesity* yanatakiwa yaendeleo, Katibu tunaendelea.

MHE. MCHUNGAJI PETER S. MSIGWA: Mwongozo wa Spika

SPIKA: Muda hautoshi, mwongozo baadaye.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili Kupokea na Kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015. Pamoja na Hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kushiriki mkutano wa kumi na tano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha ninashukuru wewe kwa kunipa fursa hii niweze kuwasilisha taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa kwa mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tume ya Mipango pamoja na Mheshimiwa Dokta Mohamed Gharib Bilal Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa uongozi wao mahiri chini ya uongozi wao taifa limepigwa hatua kubwa kimaendeleo kutokana na kusimamia kwa dhati utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM, mipango na *program* mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pongezi kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum mjumbe wa Bunge wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika wadhifa huo. Ninawapongeza pia Mawaziri na Naibu Mawaziri wengine wa Wizara mbalimbali.

SPIKA: Naomba utulivu Waheshimiwa Wabunge wanaotoka, mtoke kwa utulivu.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maalim Hussein Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa kalenga na Mheshimiwa Ridhiwan Jakaya Kikwete, Mbunge wa Chalinze waliojiunga na Bunge lako Tukufu kufuatia ushindi waliopata katika chaguzi ndogo zilizofanyika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Andrew John Chenge Mbunge wa Bariadi Magharibi kwa maoni na ushauri waliotupatia ambayo yametusaidia kuboresha taarifa ninazoziwasilisha hivi leo. Tunaahidi kuendelea kuipatia Kamati hiyo ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake. Tutazingatia maelekezo yanayotolewa na Kamati hii katika hatua mbalimbali za uandaaji na utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya Taifa.

Vile vile nitumie nafasi hii kutoa shukurani kwa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uongozi wa Mheshimiwa William Mganga Ngeleja Mbunge wa Serengerema kwa ushauri na maoni wanayotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya tume ya mipango.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia fursa hii kutoa salamu za pole kwako na kwa Wabunge wote kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu marehemu Dkt. William Augusto Mgimwa aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mbunge wa Kalenda na marehemu Said Ramadhan Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Chalinze.

SPIKA: Waheshimiwa wanaotaka kutoka waondoke na walioko ndani wakae kimya.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Vile vile natoa salamu za pole kwa Wabunge na wananchi wote waliopatwa na maafa mbalimbali nchini katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hotuba ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Kwanza ni maelezo mafupi kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2013. Pili ni muhtasari wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa taifa 2013/2014 na sehemu ya tatu ni mpango wa maendeleo wa taifa 2014/2015 unaobainisha miradi iliyopo chini ya mfumo wa matokeo makubwa sasa, miradi ya kitaifa ya kimkakati na miradi mingine ambayo Serikali inatarajia kutekeleza mwaka 2014/2015, gharama za utekelezaji wa mpango na mfumo wa uratibu ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kueleza Hali ya Uchumi wa taifa kwa mwaka 2013 na mpango wa maendeleo wa taifa 2014/2015 naomba kuainisha kwa muhtasari maeneo muhimu ambayo Kamati ya Bunge ya Bajeti ilishauri kuzingatiwa katika mpango. Maeneo hayo ni pamoja na kuongeza uwekezaji katika kilimo, kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa maji na umeme vijijini, kuanza ujenzi wa reli mpya kwa kiwango cha kimataifa na ukarabati reli iliyopo, kuboresha huduma za bandari, kuboresha mazingira ya biashara na kuimarisha uvuvi wa bahari kuu.

Aidha kamati ilishauri tume kufanya mapitio ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano 2011/2012 hadi 2015/2016 kwa kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa maeneo haya yote yamezingatiwa kikamilifu katika mpango wa maendeleo wa taifa wa mwaka 2014/2015 kama Kamati ilivyoshauri.

Vile vile Ofisi ya Rais Tume ya Mipango imeanza kufanya mapitio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano yaani 2011/2012 hadi 2015/2016.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, tangu kutokea kwa msukosuko mkubwa wa fedha na uchumi duniani mwaka 2008 ukuaji wa uchumi wa dunia umekuwa chini ya kiwango kilichokuwa kimefikiwa awali. Mwaka 2013 kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia iliendelea kupungua na kuwa asilimia tatu ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.3 mwaka 2012.

Miongoni mwa mambo yanayoendelea kuchangia kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ni pamoja na wasiwasi uliotokana na baadhi ya nchi za jumuiya ya Ulaya kushoindwa kulipa madeni yao na utekelezaji wa sera za kubana matumizi ya Serikali hizo pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea ilipungua kutoka asilimia 1.4 mwaka 2012 hadi asilimia 1.3 mwaka 2013.

Kwa upande wa nchi zinazoendelea kasi ya ukuaji wa uchumi pia ilipungua kutoka asilimia 5 mwaka 2012 hadi asilimia 4.7 mwaka 2013. Kupungua kwa ukuaji huu wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ulichangiwa na kupungua kwa ukuaji wa shughuli za kiuchumi hususan huko Urusi, Amerika ya Kusini na Caribbean.

Aidha kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Asia zinazoendelea hususan China na India ilipungua na kuwa asilimia 6.7 mwaka 2013 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha muongo mmoja takribani theluthi mbili za nchi za Kiafrika zimekuwa na ukuaji mzuri wa uchumi kutokana na ukuaji huo fursa na kiwango cha elimu kimeongezeka, vifo vya watoto wachanga vimepungua na Bara la Afrika linaendelea kuvutia wawekezaji katika nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi.

Mwaka 2013 ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara ulikuwa asilimia 4.9 kama ilivyokuwa mwaka uliotangulia 2012. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na uwekezaji hususan katika uchimbaji wa madini, miundombinu ya usafiri na mawasiliano, kilimo, uzalishaji na nishati na upanuzi wa shughuli za biashara.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Bara la Afrika katika mwaka 2013 ulizidi kuimarika na kuongezeka uwezo wake wa kuhimili misukosuko ya kiuchumi na kukabili changamoto zinazojitokeza.

Wachambuzi wa masuala ya uchumi na maendeleo Duniani na pia sekta binafsi wanakiri kwamba, Afrika hivi sasa inainukia, (*Africa is rising*). Takwimu za Benki ya Dunia zinaonesha kuwa, Tanzania ni miongoni mwa nchi 20 Duniani, ambazo uchumi wake unakua kwa kasi kubwa, *20 fastest growing economies in the world*. Wastani wa ukuaji wa Uchumi wa Tanzania kati ya mwaka 2005 mpaka 2013 ni asilimia 6.9. Nchini nyingine za Kiafrika katika orodha hii na wastani wa ukuaji wake kwa kipindi hicho ni Ethiopia asilimia 10.8, Angola asilimia 10.8, Sierra Leone asilimia 8.2, Rwanda asilimia 8.2, Ghana asilimia 7.4, Msumbiji asilimia 7.3, Uganda asilimia 6.7, Zambia asilimia 6.4 na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo asilimia 6.4.

Ukuaji wa uchumi wa Nchi Wanachama wa Jamuiya ya Afrika Mashariki kati ya 2012 na 2013, unaonesha kuimarika kwa nchi zote wanachama isipokuwa Rwanda. Uchumi wa Kenya, uliongezeka kutoka asilimia 4.6 mwaka 2012 hadi asilimia 5.6 mwaka 2013, Uganda asilimia 2.8 hadi 6.0, Burundi asilimia 4.0 hadi asilimia 4.5 na Tanzania asilimia 6.9 hadi asilimia 7.0 katika kipindi hicho. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Rwanda imepungua kutoka asilimia 8.0 mwaka 2012 hadi asilimia 5.0 mwaka 2013. Kuimarika kwa uchumi wa Nchi Wanachama wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni matokeo ya utekelezaji wa sera madhubuti za usimamizi wa uchumi na mifumo taasisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 7.0, ikilinganishwa na kukuaji wa asilimia 6.9 mwaka 2012. Shughuli ndogo ambazo zilikuwa kwa kasi kubwa katika mwaka 2013 ni mawasiliano asilimia 22.8, fedha asilimia 12.2, ujenzi asilimia 8.6; Biashara ya jumla na reja reja asilimia 8.3 na hoteli na migahawa asilimia 6.9. Licha ya viwango vikubwa vya ukuaji, shughuli ndogo za mawasiliano na fedha kila moja ilichangia chini ya asilimia 2.5 ya Pato la Taifa. Kwa upande mwingine, kasi ya ukuaji wa shughuli za kilimo ilibakia asilimia 4.3 kama ilivyokuwa mwaka 2012, hasa kutokana kupungua kwa ukuaji wa shughuli ndogo za mazao ambapo ilipungua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2012 hadi asilimia 4.5 mwaka 2013. Hata hivyo, katika eneo hili la kilimo, kasi ya ukuaji wa shughuli ndogo za mifugo na uwindaji iliongozeka kutoka asilimia 3.1 hadi asilimia 3.8 na misitu kutoka asilimia 2.4 hadi 3.3 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji katika baadhi ya shughuli ndogo ilipungua katika mwaka 2013, ikilinganisha na mwaka 2012. Maeneo husika yanayojumuisha bidhaa za viwandani yalipungua kutoka asilimia 8.2 hadi 7.7 kutokana na kupungua kwa uzalishaji katika baadhi ya viwanda; umeme na gesi asilimia 6 ilikwenda mpaka asilimia 4.4 kutokana na uchakavu wa mitambo ya kufua umeme wa maji; uchukuzi asilimia 7.1 hadi 6.2 kutokana na kupungua kwa usafirishaji wa shehena za mizigo katika njia ya anga; na uvuvi asilimia 2.9 hadi 2.2 kwa sababu ya kupungua kwa uzalishaji wa samaki, kutokana na uharibifu wa mazingira ya mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa, mwaka 2013 lilikuwa shilingi trilioni 53.17, sawa na Dola za Kimarekani bilioni 33.26 ikilinganishwa na shilingi trilioni 44.72 mwaka uliotangulia 2012, sawa na Dola za Kimarekani bilioni 25.24. Hivyo, wastani wa pato la mwananchi kwa mwaka 2013 lilikuwa shilingi 1,186,200, sawa na Dola za Kimarekani 742, ikilinganisha na shilingi 1,025,038, sawa na dola 652.1 mwaka 2012, ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.7.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013, thamani ya uwekezaji nchini, *total investment*, ilikuwa takribani Dola za Kimarekani bilioni 11.37 ikilinganishwa na dola bilioni 8.75 mwaka 2012. Ongezeko hili linatokana hasa na uwekezaji katika miundombinu ya usafiri, ujenzi, nishati, maji na kilimo. Aidha, uwekezaji wa mitaji ya kigeni na moja kwa moja *foreign direct investment* ilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 1.88 mwaka 2013, ikilinganishwa na dola bilioni 1.80 mwaka 2012. Ongezeko hili kwa kiasi kikubwa linatokana na uwekezaji katika sekta ndogo ya gesi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchumi kukua, umaskini haujapungua kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa kiasi kikubwa hali hii inatokana na tija ndogo katika sekta mama ya kilimo, ambayo inaajiri Wananchi wengi. Kilimo kimeendelea kuendeshwa katika mfumo usio rasmi hususan kwa kujikimu pamoja na kutumia zana, mbinu na teknolojia duni na hivyo kuchelewesha Mapinduzi ya Kijani. Vilevile sekta hii imeendelea kuvutia kiasi kidogo cha mitaji na mikopo kutoka katika mabenki.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya 2011/2013, yaani *household budget survey*, kwa Tanzania Bara yaliyoonesha kuwa idadi ya Watanzania wanaoishi chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi, yaani *basic needs poverty line*, ilipungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2007 hadi asilimia 28.2 mwaka 2011/2012. Katika Jiji la Dar es Salaam idadi ya kaya maskini ilipungua kutoka asilimia 14.1 mwaka 2007 hadi asilimia 4.1 mwaka 2011/2012. Kwa maeneo mengine ya mijini kiwango hicho kilipungua kutoka asilimia 22.7 hadi asilimia 21.7 katika kipindi hicho. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa, asilimia 9.7 ya watu wote

Nakala ya Mtandao (Online Document)

waishio Tanzania Bara, wapo chini ya mstari wa umaskini wa chakula, yaani *food poverty line*, ikilinganishwa na asilimia 16.6 kwa kigezo hicho mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo pia umeonesha kuwepo na mafanikio katika maendeleo ya makazi na umiliki wa rasilimali. Hivi sasa takribani asilimia 73 ya kaya zinaishi katika nyumba zilizojengwa kwa matofali ya saruji au kuchomwa au mawe ikilinganishwa na asilimia 33 mwaka 2007. Aidha, asilimia 66 ya Watanzania wanaishi kwenye nyumba zinazoezekwa kwa bati ikilinganishwa na asilimia 55 na mwaka 2007. Vilevile utafiti unaonesha kuwa idadi za kaya zinazomiliki vyombo vya usafiri na mawasiliano iliongezeka kati ya mwaka 2007 na 2012. Kwa mfano, idadi ya kaya zinazomiliki pikipiki imeongezeka kutoka asilimia 1.5 mwaka 2007 hadi asilimia 4 mwaka 2011/2014 na takribani asilimia 57 ya kaya zina mtu mmoja anayemiliki simu ya mkononi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mafanikio katika kudhibiti mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei kwa mwaka 2013 ulipungua kufikia wastani wa asilimia 7.9 ikilinganishwa na asilimia 16 mwaka 2012. Hali hiyo ilichangiwa na kushuka kwa bei za chakula hususan mchele na aina nyingine za nafaka, kufuatia kuimarika kwa upatikanaji na usambazaji wa chakula katika masoko. Mfumuko wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Aprili, 2014 ulifikia wastani wa asilimia 6.3. Kwa upande wa nchi nyingine za Afrika Mashariki mfumuko wa bei kwa mwezi Aprili nchini Burundi ulikuwa asilimia 3.8, Kenya asilimia 6.4, Rwanda asilimia 2.8, na Uganda asilimia 6.7.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013, Serikali inaendelea na sera ya kudhibiti ujazi wa fedha ili uende sambamba na ukuaji wa uchumi. Ujazi wa fedha kwa tafasiri pana zaidi, yaani M3, ulikuwa shilingi bilioni 16,106.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 14,647.1 mwaka 2012, sawa na aongezeko la asilimia 10.0. Hata hivyo, ukuaji huu ulikuwa chini ya lengo lililowekwa kwa mwaka 2013 la asilimia 15. Hii ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa rasilimali halisi za ndani katika benki, *net domestic assets*, ikiwa imeongezeka kwa asilimia 15.8 mwaka 2013 ikilinganisha na asilimia 22.3 mwaka 2012. Aidha, katika kipindi hicho kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi nayo ilipungua na kuwa asilimia 15.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 18.2 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013, ujazi wa fedha kwa tafasiri pana, M2, uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 11,890.6 kutoka shilingi bilioni 10,724.5 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Aidha, mikopo nchini iliongezeka kwa asilimia 18.8 kutoka shilingi bilioni 13,719.4 mwaka 2012 hadi shilingi bilioni 16 mwaka 2013. Kati ya hizo, shilingi bilioni 5,900.4 zilikuwa mikopo kwa Serikali Kuu na shilingi bilioni 10,386.9 zilikuwa mikopo kwa sekta binafsi. Udhhibiti wa ujazi wa fedha ni nyenzo ya Serikali kudhibiti mfumuko wa bei hususan usiokuwa wa chakula. Aidha, kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi ni kielelezo cha kuongezeka kwa uwezekaji, ajira na kuimarika kwa kipato cha mwananchi.

Mheshimiwa Spika, viwango vya riba; mwenendo wa riba za amana mbalimbali na za mikopo kwa mwaka 2013 uliimarika ikilinganishwa na mwaka 2012. Kiwango cha riba ya mikopo kwa mwaka mmoja kilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.09 Desemba, 2012 hadi asilimia 13.78 Desemba, 2013. Riba za amana za mwaka mmoja ziliongezeka kufikia wastani wa asilimia 11.12 Desemba, 2013 kutoka asilimia 11.06 mwaka 2012. Kutokana na mwenendo huo, tofauti kati ya riba za amana na mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kutoka wastani wa asilimia 3.03 Desemba, 2013 kufikia asilimia 2.66 Desemba, 2013. Kupungua riba kwa mikopo na kuongezeka kwa riba za amana za mwaka mmoja ni dhahiri kuwa Wananchi wengi wameanza kunufaika na mikopo kwa ajili ya kuendeshea shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, riba zinazotazwa katika soko la fedha za kigeni baina ya mabanki, yaani *interbank foreign exchange market* ziliongezeka kufikia wastani wa asilimia 8.58 Desemba,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

2013 ikilinganisha na asilimia 5.8 Desemba, 2012 kutokana na kupungua kwa ukwasi wa mabenzi. Aidha, riba kwa dhamana za Serikali ziliongezeka kufikia wastani wa asilimia 16.20 mwaka 2013 ikilinganishwa na asilimia 12.8 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola za Marekani ilishuka kwa wastani 1.7 mwaka 2013, ikilinganishwa na asilimia 0.9 mwaka 2012. Dola ya Kimarekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi za Tanzania 1,598 mwaka 2013 ikilinganishwa na shilingi 1571.70 mwaka 2012. Vilevile Dola ya Marekani iliuzwa kwa shilingi 1,578.57 Desemba, 2013 ikilinganishwa na shilingi 1,571.62 Desemba 2012. Kushuka kwa thamani ya shilingi kunatokana na kuongezeka mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa mbalimbali kutoka nje, ambayo yalikuwa zaidi ya mauzo ya bidhaa za Tanzania. Aidha, thamani ya Shilingi ya Tanzania iliendelea kushuka ambapo kufikia Aprili, 2014 Dola ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 1,637.38.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nje; katika mwaka 2013, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilipungua kwa asilimia 1.7 kutoka Dola za Kimarekani milioni 8,675.6 mwaka 2012 hadi dola milioni 8,532. Upungufu huu ulichangiwa zaidi na kushuka kwa mauzo ya dhahabu na bidhaa nyingine asilia ikiwa ni pamoja na tumbaku, kahawa, pamba, katani, kushuka kwa bei za uzalishaji wa baadhi ya mazao katika Soko la Dunia. Aidha, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 6.6 kutoka Dola za Kimarekani milioni 13,517.6 kutoka Dola milioni 12,678 mwaka uliotangulia. Ongezeko hili lilitokana na uagizaji wa mafuta ambapo kiwango cha uagizaji kiliongezeka kwa asilimia 27.4.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo Tanzania ilifanya vizuri katika biashara ya nje kwa mwaka 2013 ni yafuatayo; huduma za utalii ambayo mapato yake yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani bilioni 1.37 mwaka 2012 hadi dola bilioni 1.81 mwaka 2013; huduma za usafirishaji bidhaa kupitia Tanzania kwenda nchi jirani, yaani *transit trade*, ambapo mapato yake yalikadiriwa kuongezeka kutoka dola milioni 497.3 mwaka 2012 hadi dola milioni 576.8, mwaka 2013. Aidha, mizigo iliyopitishwa nchini kwenda nchi jirani iliongezeka kutoka tani 1,175,484 hadi tani 1,386,705 katika kipindi hicho. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani pia iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,037.3 mwaka 2012 hadi dola milioni 1,072.1 mwaka 2013. Serikali inaipongeza sana juhudi za Wananchi na wadau waliochangia ongezeko hili katika sekta nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuimraika. Katika kipindi kinachoishia Desemba, 2013, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 4,676.2 ikilinganishwa na dola milioni 4,069.1 mwaka 2012. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kinatosheleza uagizaji bidhaa kutoka nje kwa zaidi ya miezi 4.5 ikilinganisha na miezi 3.9 mwaka 2012. Aidha, akiba ya fedha za kigeni katika benki za biashara ilipungua kwa asilimia 2.2 kufikia Dola za Marekani milioni 876.3 kutoka dola milioni 887 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, mapato na matumizi ya Serikali: Mapato ya ndani kwa mwaka 2012, yalikuwa ni shilingi bilioni 8,586, sawa na asilimia 17.6 ya Pato la Taifa. Aidha, matumizi yalikuwa shilingi bilioni 12,817 sawa na asilimia 26.3 ya pato la Taifa. Hivyo, nakisi ya bajeti, ikijumuisha na misaada ilikuwa asilimia 6.5 ya Pato la Taifa katika mwaka 2012/2013. Mwaka 2013/2014 Serikali ilikadiriwa kukusanya mapato ya ndani jumla ya shilingi bilioni 11,174.07, sawa na asilimia 18.3 ya Pato la Taifa. Matumizi yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 18,248.9 sawa na asilimia 27 ya Pato la Taifa. Kufuatia hali hii, nakisi ya bajeti, ikijumulisha misaada, inakadiriwa kuwa asilimia 5.5 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2013, Deni la Taifa lilifikia Dola za Marekani bilioni 17.10, sawa na shilingi trilioni 27.04 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22 katika kipindi kama hicho

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mwaka 2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 19.1. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya hasa ya masharti nafuu na ya kibiashara pamoja na kukua kwa malimbikizo ya riba kwa madeni ya nje hususan kwa nchi zizizo wanachama wa kundi la Paris, ambazo hazitoi misamaha. Mikopo hii ilitumika katika kugharimia miradi mbalimbali kuhusu maendeleo ya Taifa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, ujenzi na ukarabati wa barabara, ujenzi wa miundombinu ya umeme na ujenzi wa miundombinu ya maji kwa Miradi ya Ruvu Juu na Chini. Pamoja na ongezeko hilo, Deni la Taifa linahimilika.

Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha 15 cha Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kilichofanyika Uganda Novemba, 2013, pamoja na mambo mengine Itifaki ya kuanzisha sarafu moja kwa nchi za Afrika Mashariki ilisainiwa. Masuala ya msingi yanayotakiwa kutekelezwa ni kuwa na sarafu moja, ni kufikia vigezo vya muunganiko wa uchumi mpana, *Micro Economic Convergence Criteria* na kuanzisha Taasisi muhimu ya kusimamia utekelezaji wa sarafu moja kwa nchi husika, ambazo ni Taasisi za Fedha za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Takwimu ya Afrika Mashariki na Kamisheni ya Huduma ya Fedha ya Afrika Mashariki ili kufikia hatua hiyo Nchi Wanachama wanatakiwa kukamilisha hatua za awali za mtengamano za umoja wa forodha na soko la pamoja ikijumuisha kurekebisha sheria na kuweka mfumo wa pamoja wa kielektroniki wa kufuatilia usafirishaji wa mizigo ndani ya Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na hatua za kuridhisha katika utekelezaji wa Miradi na Programu za pamoja za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika uendelezaji wa barabara na reli zinazounganisha Tanzania na Nchi Wanachama, usanifu wa kina wa barabara za Arusha, Holili - Taveta, Voi ulikamilika na mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo ulitiwa sahihi kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika na nchi za Kenya na Tanzania. Aidha, katika kutekeleza mpango kambambe wa kuendeleza reli ya Dar es Salaam, Isaka, Kigali/Keza, Gitegi, Musongati inayojumuisha nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania, upembuzi wa kina umekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za utekelezaji wa utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI nchini, mwaka 2013 Serikali ilianzisha mpango unaoitwa *Option B plus*, unaolenga kuwapatia wajawazito wenye maambukizi ya VVU, dawa ya kupunguza makali ya VVU kwa wakati. Hii ni katika kutekeleza mpango wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, mafunzo na warsha zilizotolewa kwa watoa huduma na viongozi wa ngazi ya Mikoa na Wilaya kwa lengo la kuwawezesha kuandaa mpango endelevu wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013 Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Mazingira ya Mwaka, 1977 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ili kuleta maendeleo endelevu. Katika kipindi hiki miongozo mitatu kwa ajili ya kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 iliandaliwa na hivyo kufanya Sheria iwe na miongozo saba kati ya 19 inayohitajika kulinganisha na miongozo minne iliyoandaliwa mwaka 2012. Miongozo hiyo ni mwongozo wa kuandaa tathmini ya kimkakati ya mazingira, mwongozo wa kuhusisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika Sera na Mipango na muongozo wa maandalizi ya mipango ya mizingira ya kisekta na Serikali za Mitaa. Hii ni rai ya Serikali kuwa, miongozo hii itumike ipasavyo ili isaidie katika jitihada za kunusuru nchi yetu kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali iliendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mkakati huo unatoa mwongozo wa hatua ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, zinazotakiwa kuchukuliwa na sekta mbalimbali na kutoa mwongozo wa kuziwezesha sekta kuandaa mpango wake

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Sekta za mtaji za maji na kilimo zimeanza utekelezaji wa mkakati huu kwa kuandaa mipango yake ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, upangaji na uendelezaji wa maji na vijiji. Katika mwaka 2013 Serikali iliendelea kuandaa mpango wa kusimamia uendelezaji na udhibiti wa ukuaji wa maji nchini. Mipango hiyo ya aina mbili, mipango kabambe ambayo hutoa mwongozo na uendelezaji maji kwa muda mrefu wa miaka 20 na mipango ya muda wa kati na matumizi ya ardhi ambayo hutoa mwongozo kwa uendelezaji wa maji kwa muda wa miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam ziliendelea kuandaa Mpango Kabambe wa Jiji la Dar es Salaam, ambapo rasimu ya mwisho iliwasilishwa kwa wadau na mtaalam mwelekezi anayeendeleza kuboresha kwa kutumia maoni na mapendekezo yanayotolewa na wadau. Aidha, Halmashauri ya Mji Mdogo wa Bagamoyo ilikamilisha maandalizi ya rasimu ya awali ya Mpango Kabambe ya Mji huo. Pia, Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, ilikamilisha maandalizi ya rasimu ya mpango wa muda wa kati na matumizi ya ardhi kwa Mji wa Kilindoni. Vilevile Serikali inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Manispaa ya Sumbawanga na Mji wa Bariadi kuandaa mpango kabambe wa maji hiyo.

Mheshimiwa Spika, hali ya usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali hapa nchini imeendelea kuimarika. Kwa upande wa ushiriki wa wanawake katika ngazi za siasa na maamuzi, idadi ya Mawaziri Wanawake imeongezeka kutoka asilimia 15 mwaka 2005 hadi asilimia 30 mwaka 2013. Wakuu wa Mikoa Wanawake kutoka asilimia 10 mwaka 2005 hadi asilimia 24 mwaka 2013. Majaji Wanawake pia wameongezeka kutoka asilimia 33 hadi asilimia 61 kwa kipindi hicho. Uwakilishi wa Wanawake Bungeni umeongezeka kutoka asilimia 30.3 mwaka 2005 na kufikia asilimia 36 ya Wabunge wote mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuwawezesha wanawake kiuchumi, mwaka 2013/2014, Serikali ilitenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Katika kipindi hicho, Julai mpaka Desemba, Mfuko huo ulikuwa umepatiwa shilingi 515,000,000. Aidha, taasisi za kifedha zimeendelea kutoa mikopo ya fedha na mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake. Baadhi ya Taasisi hizo ni Benki ya Wanawake Tanzania, *Women Covenant Bank*, SACCOS na VICOBA.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa MKUKUTA na Malengo ya Milenia. Utekelezaji wa MKUKUTA umekuwa na mafaniko ya kuridhisha licha ya changamoto mbalimbali. Katika kupunguza umaskini wa kipato, Serikali iliendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuongeza fursa za ajira nchini na kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana kuwawezesha kujijiri wenyewe. Kutokana na hatua hizo, jumla ya nafasi za ajira 274,030 zilipatikana mwaka 2012/2013, ikilinganisha na ajira 250,000 mwaka 2011/2012. Aidha, Serikali ilibaini na kuhakiki vikundi 502 vikiwa na jumla ya wanachama 5,385; wanawake 2,519 na wanaume 2,866, katika Mikoa 17 kwa ajili ya kuviendeleza na kuvipatia mitaji na mfunzo ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, utafiti wa mapato na matumizi ya kaya, *Household Budget Survey*, uliofanyika mwaka 2011/2012, umeonesha kuwa idadi ya kaya maskini zilizo chini ya kiwango cha mahitaji, yaani *basic needs poverty*, kimepungua kwa asilimia 6.2 kati ya mwaka 2007 na 2012. Utafiti huo pia umeonesha mafanikio katika upatikanaji wa huduma za Afya, Elimu na Maji. Kwa upande wa Afya, Tanzania imefanikiwa kufikia Lengo la Milenia Namba Nne ikiwa imepunguza vifo vya watoto wachanga toka 191 mwaka 2000 mpaka vifo 51 kati ya watoto 1000 mwaka 2013. Aidha, vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vilipungua kutoka 115 mwaka 2000 hadi vifo 54 kati ya watoto 1000 mwaka 2013.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jitihada zake za kipekee katika eneo hili hapa nchini na nje ya nchi. Katika hili ameonesha ukereketwa na utumishi uliotukuka, ambapo yeye pamoja na Mwenyekiti mweza Mheshimwa Stephen Harper, Waziri Mkuu wa Canada, imebidi wapewe pongezi za kipekee na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Ban Ki-Moon, kwa ufanisi mkubwa waliouonesha tangu walipoteuliwa kuongoza Tume ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia masuala la afya ya mama na mtoto Duniani. Pongezi hizo zilitolewa tarehe 29 Mei, 2014 huko Toronto Canada. Hii ni heshima kubwa kwake na kwa Taifa ketu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, utafiti kuhusu Malaria na Ukimwi (*HIV and Malaria Indicator Survey*) wa mwaka 2012, umeonesha kuwa kasi ya maambukizi ya malaria ilipungua kutoka asilimia 18 mwaka 2007 hadi asilimia 9 mwaka 2011/2012. Maambukizi ya UKIMWI katika kundi la watu wenye umri kati ya miaka 15 na 49 kutoka asilimia 7.7 mwaka 2007 na 2008 hadi asilimia 5 mwaka 2011/12. Haya ni mafanikio ya kutia moyo. Hata hivyo, naomba nisisitize kwa Watanzania wote kuwa, janga hili la Ukimwi na Ugonjwa wa Malaria bado ni changamoto kubwa. Hivyo, tunapaswa kuongeza jitihada zaidi ili hatimaye tuweze kufikia azma yetu kuwa, Tanzania bila UKIMWI na Malaria inawezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sekta ya Elimu na Maji ni sehemu ya maeneo yaliyo chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa; mafanikio yaliyopatikana katika sekta hizo yameelezwa katika sehemu ya utekelezaji wa Miradi hiyo ya BRN.

Mheshimiwa Spika, sasa nijikite katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mawaziri wa Sekta wameshaeleza kwa kina utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa sekta zao kwa kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, naomba nieleze kwa kifupi sana, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014. Maelezo yangu yatajikita katika maeneo ya kimkakati ambayo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulipanga kuyatekeleza. Kwa ujumla katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014 umekuwa na mfanikio ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Miradi chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, mwaka 2013/2014 Serikali ilianza kutekeleza baadhi ya miradi kwa kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Matokeo Makubwa Sasa. Katika mwaka 2013/2014 Ofisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Miradi (*President's Delivery Bureau - PDB*), ilifuatilia miradi iliyoainishwa kupitia awamu ya kwanza ya uchambuzi wa kimaabara katika Sekta ya Kilimo, Elimu, Nishati, Maji, Uchukuzi na Ukusanyaji wa Mapato.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo, baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa chini ya MNS ni pamoja na kutoa mafunzo ya kuendesha *scheme* za umwagiliaji kwa Maafisa Ugani 95 na Wakulima 95. Kupata hati miliki kwa mashamba makubwa mawili ya Bagamoyo na Mkulazi, Rufiji na Hati ya Kimila kwa Mashamba madogo 185 na kutoa mafunzo kuhusu biashara, kilimo bora na kuunda vyama vya wakulima katika Miradi ya Bagamoyo, Lukulilo na Ngalmila na maghala 50 yameendelea kufanyiwa tathmini kwa ajili ya ukarabati. Pamoja na mafanikio haya, ipo Miradi mingi ya Sekta ya Kilimo inayotekelezwa kama nitakavyoeleza katika eneo la Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Elimu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa uandikishaji katika ngazi zote za elimu, kuongezeka kwa ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne kutoka asilimia 43.08 mwaka 72 hadi 58.25 mwaka 2013. Katika ngazi ya Elimu ya Msingi kutoka asilimia 31 mwaka 2013 hadi asilimia 50.3 mwaka 2015. Kiwango cha kihitumu elemu ya msingi kiliongezeka kutoka asilimia 54.8 mwaka 2012 hadi asilimia 55.3 mwaka 2015.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine katika Sekta ya Elimu ni kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika shule 56 kati ya 264 za awamu ya kwanza na kutoa tuzo kwa shule 3,000 zilizofanya vizuri na zile zinazoonesha kupiga hatua kulingana na ufaulu katika mwaka 2012/2013. Kuongeza maabara katika shule za kata ili kuimarisha elimu ya sayansi na ufundi. Kuanza ukarabati wa shule kongwe za kitaifa na kufanyika kwa upimaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi wa darasa la pili katika sampuli ya shule 200 na kuandaa mwongozo wa kufundisha KKK. Pamoja na mafanikio hayo, napenda nikiri kuwa changamoto katika eneo hili bado zipo na ni kubwa. Kwa hiyo, ni dhahiri tunahitaji kuimarisha upatikanaji wa elimu bora katika ngazi zote. Uwezo wa Tanzania ya kesho katika ulimwengu wenye ushindani mkali kiuchumi, unategemea upatikanaji wa elimu bora, ujuzi, ubunifu na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Nishati, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kuunganishwa umeme wateja wapya 138,931 dhidi ya lengo la kuunganisha wateja 150,000 kwa mwaka 2013/2014 na kupunguza upotevu wa umeme kutoka asilimia 21 mwaka 2012 hadi asilimia 19 mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bomba la gesi lenye urefu wa kilometa 542 na kipenyo cha nchi 36 kutoka Mradi wa Mnazi Bay -Mtwara na Songosongo - Lindi hadi Dar es Salaam uliendelea kutekelezwa. Kazi zilizofanyika hadi Aprili, 2014 ni pamoja na kuwasili na kupokelewa kwa mabomba yote ya gesi, kuunganisha mabomba yenye urefu wa kilometa 362 sawa na asilimia 70, kufukia bomba la gesi kwa umbali wa kilometa 182 sawa na asilimia 34 na kujenga bomba la gesi chini ya Bahari kwa kilometa 25.6.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Uchukuzi, mafanikio ni pamoja na kuanzishwa kwa mradi wa kielektroniki wa kufuatilia usafirishaji wa mizigo, ambapo magari yenye kifaa hiki hayana haja ya kusimama katika baadhi ya vituo vya ukaguzi na hivyo kuokoa muda wao barabarani na kuongezeka kwa ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam kwa kuhudumia zaidi ya tani milioni 13, Desemba, 2013 ikilinganisha na tani milioni 12 mwezi Desemba, 2012. Vilevile katika Reli ya Kati, Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja matatu yaliyopo kilometa 293, kilometa 303 na kilometa 517 kutoka Dar es Salaam. Uundwaji upya wa vichwa vitatu vya treni katika karakana ya Morogoro na uundwaji wa vichwa vingine vitano upo katika hatua mbalimbali. Aidha, malipo ya vichwa vipya 13, mabehewa ya abiria 22 na mabehewa ya breki 34 na mabahewa ya kokoto 25 yamekamilika na malipo ya mabehewa 274 ya mizigo yamefanyika kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zilizofanyika za kurejesha ufanisi wa mtandao wa Reli, kumekuwa na matukio ya hujuma ikiwa ni pamoja na kung'oa mataluma ya njia za Reli. Matukio haya yanaturudisha nyuma. Naomba nitumie fursa hii kuwaonya na kuwataka wanaofanya hujuma hii kuacha mara moja na pia kuwaomba Wananchi kutimiza wajibu wao wa kulinda miundombinu ambayo inatutumikia sisi wote.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Maji, mafanikio yaliyopatikana ni kukamilika kwa ujenzi wa Miradi ya Maji 228 katika vijiji 243 na Halmashauri 98 na hivyo kutuwezesha jumla ya vituo vya kuchotea maji 10,560 kujengwa na kuundwa kwa Jumuiya za Watumiaji Maji 373 hadi Machi, 2014. Matokeo yake ni kuwa, Wananchi 2,640,000 waishio vijijini, wamepatiwa maji safi katika kipindi cha miezi sita, ikilinganishwa na idadi kati ya Wananchi 300,000 na 500,000 waliokuwa wanaweza kuunganishiwa huduma ya maji safi na salama kwa mwaka hapo awali. Matokeo haya yamechangiwa na kupunguza muda wa mchakato wa ununuzi wa umma, kutoka siku 265 hadi siku 90. Aidha, Miradi 538 ya miundombinu ya maji vijijini itakayohusisha vituo 9,630 vya kuchotea maji katika vijiji 587 yenye uwezo wa kuhudumia wanavijiji milioni mbili na arobaini elfu inaendelea kujengwa. Sambamba na hilo, mikataba ya Miradi 707 inayohusisha vituo 13,050 katika vijiji 725 yenye uwezo wa kuhudumia wanavijiji 3,262,000

Nakala ya Mtandao (Online Document)

imesainiwa. Naomba nitumie fursa hii kuwajulisha Wananchi kuwa ili Serikali itimize wajibu wake vizuri wa kuwafikishia Wananchi maji baada ya miradi hii kukamilika, ni wajibu wa msingi kwa kila Mwananchi kuhakikisha hifadhi endelevu ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2014 ukusanyaji wa mapato yaliyotokana na vyanzo vilivyoibuliwa chini ya Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*) ulikuwa umefikia shilingi bilioni 338, sawa na asilimia 29.14 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni moja nukta moja sita katika Mwaka wa Fedha 2013/2014. Matokeo yasiyoridhisha yanatokana na baadhi ya mapendekezo ya BRN kutotekelezwa katika mwaka 2013/2014. Mapendekezo hayo ni kubadilisha mfumo wa ushuru wa bidhaa zisizo za *petrol* kutoka *specific* kwenda *advalorem* makisio shilingi bilioni 386, kuanzisha kodi ya zuiyo ya asilimia tano kwenye bidhaa zinazotoka nje ya nchi, makisio shilingi bilioni 225.6. Kwa kuwa ukusanyaji mapato ndiyo msingi wa kufanikisha kwa BRN, Serikali inachambua vyanzo mbadala vya kufidia mapato haya ili kuhakikisha lengo kuu la kuongeza mapato kwa shilingi trilioni 3.48 linafanikiwa ifikapo mwaka 2015/2016. Aidha, katika juhudi za kuimarisha makusanyo ya kodi, Serikali inaendelea kuimarisha matumizi ya mashine za EFD ambazo mamlaka inayohusika inaendelea na zoezi la kuwasajili wafanyabiashara wote wanaostahili kuanza kutumia mashine hii.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kitaifa na Kimkakati. Katika eneo la reli, kazi zilizopangwa kubadilisha reli nyepesi na kuweka nzito ya ratili themanini kwa yadi kwa umbali wa kilometa themanini na tisa kati ya Kitaraka na Malongwe na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi mbalimbali. Kazi zilizotekelezwa hadi Aprili 14 ni pamoja na kutandikwa kwa reli yeynye uzito wa ratili themanini kwa yadi kwa urefu wa kilometa arobaini na saba na kufikisha jumla ya kilometa themanini na tisa zilizopangwa; na upembuzi yakinifu kwa Mradi wa Reli ya Isaka - Mwanza, Tanga – Arusha – Musoma, Mtwara – Mbamba Bay uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na upembuzi wa kina kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali – Keza – Msongati umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara kazi zilizofanyika ni kukamilisha ujenzi wa kilometa mia sita nukta moja saba za barabara kuu kwa kiwango cha lami, sawa na asilimia 121 ya lengo la kilometa 495 na kukamilisha ukarabati wa kilometa 193.5 za barabara kuu kwa kiwango cha lami, sawa na asilimia 102 ya lengo la kilometa 190. Kukamilisha ujenzi wa kilometa 59.25 za barabara za mkoa kwa kiwango cha lami, sawa na asilimia 90 ya lengo la kilometa 66.1; na kukamilisha ukarabati wa kilometa 424.5; kiwango cha changarawe sawa na asilimia 49 ya lengo la kilometa 867 kwa mwaka. Kwa upande wa madaraja na vivuko kazi zilizofanyika ni kukamilisha ujenzi wa madaraja ya Malagarasi Kigoma na Nanganga na Nangoo Mtwara na kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Maligusu Mwanza asilimia 90, Mbutu Tabora asilimia 96 na Kigamboni Dar es Salaam asilimia 44.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bandari kazi zilizopangwa ni kuboresha Gati Namba Moja hadi Saba na kuanza ujenzi wa Gati Namba 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam. Kukamilisha usanifu wa kina, kuandaa michoro na kuendelea kutafuta wawekezaji kwa Bandari ya Mwambani Tanga na kukamilisha uthamini wa mali na ulipaji fidia kwa Bandari ya Mbegani Bagamoyo. Kazi zilizofanyika ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa Gati Namba Moja hadi Saba na kukamilika kwa *hydrographic* na *topographic survey* katika Gati Namba 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam. Hatua iliyofikiwa katika kuendeleza Bandari ya Mwambani Tanga ni kutangazwa kwa zabuni ya kumpata mwekezaji mwenye uwezo wa kuendeleza Bandari hiyo baada ya kupatikana kwa eneo la Mradi, hekta 174, ambapo kati ya hizo hekta 92 zina hati miliki na malipo ya awali ya Shilingi bilioni moja nukta saba yamelipwa kwa Halmashauri ya Jiji la Tanga ili Wananchi walipwe fidia.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa anga, malengo ya mwaka 2013/2014 yalikuwa ni kukamilisha awamu ya kwanza ya uikarabati wa viwanja vya ndege Kigoma na Tabora na kuanza awamu ya pili; kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Songwe, Mwanza, Bukoba na Mafya; kuanza ujezi wa jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere; na kuanza ujenzi wa viwanja vya Sumbawanga na Sumbawanga, pamoja na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Mtwara na Arusha. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ukarabati wa viwanja vya Kigoma na Tabora na kuanza maandalizi ya awamu ya pili kuendelea na ujenzi wa viwanja vya Songwe, Mwanza na Bukoba; kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja cha Mafia; kuanza ujenzi wa jengo la tatu la abiria katika kiwanja cha Julius Nyerere; na kuanza kwa maandalizi ya viwanja vya ndege Sumbawanga na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la nishati, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuvutia uwekezaji katika sekta ya nishati, hususan nishati mbadala na makaa ya mawe; kufuatia jitihada mahususi za Serikali, ikiwemo punguzo la gharama za kuunganisha umeme, pamoja na uwezeshaji chini ya Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund*). Hadi mwezi Machi, 2014 kiwango cha uunganishaji wa umeme kimeongezeka na kufikia asilimia 24, ambapo kiwango cha uunganishaji umeme vijijini kimeongezeka kutoka asilimia mbili mwaka 2005 hadi asilimia saba. Lengo la Serikali ni kuwawezesha Watanzania asilimia 30 kuunganisha umeme ifikapo mwaka 2015/2016.

Katika juhudi za Serikali za kuongeza upatikanaji wa umeme, Miradi ya Ufuaji Umeme ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo ni pamoja na mitambo ya kufua umeme Kinyerezi I megawati 150 na Kinyerezi II megawati 240, itakayotumia gesi asilia. Miradi mingine itatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na mwekezaji binafsi, ambayo ni Mradi wa Gesi ya Kinyerezi megawati 300 na Kinyerezi IV megawati 500. Miradi ya Upepo (*Wind Power*) megawati 50 Singida na Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kiwira Megawati 200, Ngaka megawati 400 na Mchuchuma megawati 600.

Mheshimiwa Spika, kwa Mradi wa Maji Safi na Maji Taka malengo ya 2013/2014 yalikuwa ni kujenga na kukarabati miundombinu ya maji mijini na vijijini, hususan kuboresha upatikanaji wa maji Jijini Dar es Salaam. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji Ruvu Chini umekamilika, utandazaji wa mabomba kutoka Bagamoyo hadi Dar es Salaam uliendelea ambapo kilometa 35.16 zilikamilika kati ya kilometa 55.93 na mradi wote, sawa na asilimia 62.

Kwa upande wa Mradi wa Maji Ruvu Juu kazi zilizofanyika ni kusaini mkataba wa ujenzi na Kampuni ya VA-TECH WABAG ya India na utekelezaji umeanza. Serikali inaendelea kuboresha huduma za maji kwa kukarabati miundombinu ya kugharimia malipo ya umeme kwa ajili ya kuendesha mitambo ya maji katika Miradi ya Maji ya Kitaifa ya Makonde – Mtwara, Wanging'ombe – Njombe, Kahama – Shinyanga, Maswa – Simiyu, Chalinze – Pwani, Mgango Kiabakali – Mara na Handeni Trank Main Tanga.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kilimo malengo yalikuwa ni kutenga ardhi kwa kilimo cha miwa, kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika eneo la SAGCOT, kuanzisha kambi ya mafunzo ya kilimo ya vijana, kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini na kukamilisha ujenzi wa Ghala la Songea na kuanza ujenzi wa maghala mawili ya Songea na Mbozi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5000 za nafaka kila moja. Mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na kuhakiki jumla ya hekta 254,675, ambapo mashamba mawili yenye jumla ya hekta 85,000 yalipata hati miliki. Kukamilisha utayarishaji wa mipango na matumizi bora ya ardhi kwa vijiji katika Wilaya za Kilombero na Rufiji.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Umwagiliaji katika eneo la SAGCOT, kazi ya kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji za Sonjo na Lupiro Mkoani Morogoro inaendelea na ujenzi wa banio katika Skimu ya Umwagiliaji ya Itete umefikia asilimia 60, na ujenzi wa Ofisi ya Mradi imekamilika. Aidha, ujenzi wa ukarabati wa skimu 14 zenye jumla ya hekta 4,186 umekamilika. Katika ujenzi wa Kambi ya Vijana Mkongo Rufiji, ukarabati wa majengo umekamilika na kambi kuzinduliwa rasmi tarehe 5 Oktoba, 2013, ambapo vijana 50 wanaendelea kupatiwa mafunzo. Kwa upande wa maghala ya kuhifadhi nafaka, ujenzi wa Ghala la Songea umefikia katika hatua ya kuweka paa.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Viwanda, malengo ya mwaka 2014 yalikuwa ni kuendeleza Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZ/SEZ); kuendelea na Miradi ya Makaa ya Mawe na Chuma ya Mchuchuma na Liganga na kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza viuadudu Kibaha; na kukamilisha tafiti za kitaalam kuhusu magadi-soda katika Bonde la Engaruka na Ziwa Natron. Kazi zilizotekelezwa ni kulipa fidia ya Shilingi bilioni ishirini katika eneo la Kurasini kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Biashara na Huduma na hivyo kufanya jumla ya fidia iliyolipwa kufikia Shilingi bilioni arobaini na nne nukta saba; na kulipa fidia ya Shilingi bilioni tatu katika eneo la Bagamoyo na Shilingi bilioni tatu katika eneo la Tanga. Mafanikio mengine ni kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa miundombinu wezeshi katika kiwanda cha kuzalisha viuadudu Kibaha; kuendelea na tafiti za magadi-soda katika Ziwa Natron na kutafiti teknolojia bora ya uchimbaji wa magadi-soda katika Bonde la Engaruka na kuanza ununuzi wa mitambo kwa ajili ya ujenzi wa mgodi wa chuma katika eneo la Liganga.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta binafsi, yamekuwepo mafanikio mengi. Kwa mfano, katika Sekta ya Viwanda kwa mwaka 2013/2014, miradi inayoendelezwa na sekta binafsi ni pamoja na kiwanda cha ngozi cha Meru Tanneries Arusha, Kiwanda cha Nguo cha Dahong Shinyanga, kiwanda cha ngozi huko Shinyanga na kiwanda cha saruji cha Dangote Mtwara. Hatua zilizofikiwa ni kukamilika kwa kiwanda cha ngozi Arusha chenye uwezo wa kusindika vipande 159,000 vya ngozi ya ng'ombe na vipande 468,000 vya ngozi ya mbuzi na kondoo. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha ngozi Shinyanga chenye uwezo wa kusindika vipande 936,000 vya ngozi ya ng'ombe na vipande 2,200,000 kwa ngozi ya mbuzi na kondoo na kuajiri watu 500.

Kiwanda kingine kinachoendelea kujengwa ni kiwanda cha nguo Shinyanga ambacho kinatarajiwa kukamilika kabla ya Desemba, 2014 na kitatumia pamba tani 30,000 kwa mwaka na kuanza kwa ujenzi wa kiwanda cha Saruji cha Dangote Mtwara. Maeneo mengine yenye uwekezaji mkubwa katika sekta binafsi ni pamoja na huduma za jamii hususan elimu na mafunzo ya ufundi na afya, mabenki na huduma za afya, mawasiliano, uchukuzi na usafirishaji, kilimo, nyumba na makazi na nishati.

Naomba kutumia fursa hii kuipongeza kwa dhati sekta binafsi kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu. Serikali kwa upande wake inahidi kuongeza msukumo zaidi kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara nchini ili kuwezesha sekta binafsi ichangia zaidi ukuaji wa Uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya rasilimali watu, Serikali katika mwaka 2013/2014 ilipanga kuboresha miundombinu ya Vyuo Vikuu na ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA). Kazi zilizotekelezwa ni pamoja ukarabati wa Chuo Kikuu Huria katika Mikoa ya Mara, Simiyu na Shinyanga, ukarabati wa hosteli na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa kumbi za mihadhara katika Chuo Kikuu Mzumbe, kukamilika kwa asilimia 65 ya ujenzi wa madarasa na maabara katika Vyuo Vikuu vya Ardhi na Dodoma na kuanza kwa ujenzi wa miundombinu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wezeshi. Kupatikana kwa mkandarasi kwa ujenzi wa hospitali katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Mlonganzila.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vyuo vya ufundi stadi, kazi zilizofanyika ni kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala na karakana mbili za useremala katika Chuo cha Kihonda Morogoro na kuanza mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuweza kupata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni ishirini na tatu kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya Mkoa wa Geita, Njombe, Simiyu na Rukwa, ikiwa ni hatua ya kutekeleza azma ya kuwa na Vyuo vya VETA kila Wilaya nchini. Sambamba na hii, Serikali iliongeza fursa ya wanafunzi ambao hawajapata nafasi ya kujiunga na kidato cha sita ili kusaidia kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo 25 vya maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivyo vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi vilipatiwa vifaa vya kujifunzia na kufundishia masomo ya ufundi stadi na kwa mwaka 2013/2014 vilisajili wanafunzi 2,722 na fani mbalimbali za ufundi. Vilevile Serikali iliendelea kukarabati miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Tarime, Kilwa Masoko, Masasi na Chilala. Nitumie nafasi hii kutoa rai kwa Halmashauri za Wilaya kuwa na utaratibu wa kutenga maeneo kwa utekelezaji wa Miradi hii kama michango yao. Utaratibu huu pamoja na kupunguza muda wa maandalizi, utasaidia sana kupunguza gharama za Serikali katika kulipa fidia kwa watu kupisha ujenzi wa Miradi.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Fedha, malengo ya 2013 yalikuwa ni kuziongezea mtaji Benki za Maendeleo (TIB), Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Wanawake. Hadi kufikia Machi, TIB na Benki ya Kilimo ziliongezewa mtaji wa Shilingi bilioni kumi kila moja na Benki ya Wanawake iliongezewa Shilingi bilioni mia nne hamsini. Aidha, Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Kilimo ilizinduliwa na kuanza kufanya kazi na usaili wa Mtendaji Mkuu na Wafanyakazi wa Benki hiyo umefanyika Mwezi Machi, 2014.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za utalii, malengo yalikuwa ni kuboresha huduma za utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi na hivyo kuongeza mapato yatokanayo na utalii. Idadi ya watalii kutoka nje ya nchi iliongezeka kutoka wastani wa 930,753 mwaka 2012 hadi 1,090,905 mwaka 2013. Mapato yaliyopatikana kutokana na utalii yanakadiriwa kufikia Dola za Kimarekani bilioni moja nukta nane moja mwaka 2013 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni moja nukta tatu saba mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyoelezwa, changamoto zifuatazo zilijitokeza na kuathiri utekelezaji. Moja ni ufinyu wa rasilimali fedha kuwezesha Miradi ya maendeleo kutekelezwa kama ilivyopangwa. Pili, ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika uwekezaji unaozingatia vipaumbele vya mpango wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na kuendelea na juhudi za kuboresha upatikanaji wa mapato ya ndani na kuwahimiza wafadhili kutimiza ahadi zao na kuzingatia mzunguko wa bajeti; na kufanya uchambuzi wa kimaabara kuhusu kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015. Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015 yamezingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 hadi 2016) na Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2014/2015 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2010 - 2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, katika Ilani ya CCM kwa kipindi cha mwaka 2010 - 2015, malengo yalikuwa ni kujenga uchumi wa kisasa kwa kuboresha utoaji wa elimu, kuandaa rasilimali watu katika maarifa na mwelekeo, kufanya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi, kufanya mapinduzi ya viwanda, kuinua matumizi ya maarifa, yaani teknolojia katika uchumi wa nchi, upatikanaji wa nishati yenye uhakika na nishati mbadala na ujenzi wa miundombinu ya kisasa. Maeneo haya ya kipaumbele yalizingatiwa na kufafanuliwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 hadi 16), ambapo sasa tuko katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2014/2015 ni wa nne katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011 hadi 16). Miradi mingi imezingatia vipaumbele vya mpango wa maendeleo wa miaka mitano na hivyo ni mwendelezo wa ile iliyokuwepo katika mpango wa mwaka 2013/2014, ambayo ina uhusiano wa moja kwa moja na maeneo ya Dira ya Taifa na Maendeleo 2025. Msisitizo umewekwa katika kuhakikisha rasilimali chache zilizopo zinatumiwa katika maeneo ya kipaumbele, hususan Miradi iliyo chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa. Aidha, mfumo wa ugharimaji na utekelezaji utaimarishwa kuwezesha Miradi ya Maendeleo kutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla. Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2013/2014 umeandaliwa kwa kuzingatia shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2013/2014 mpaka 16, ambayo yameainishwa kwa kina katika Kitabu cha Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2014/2015. Kwa kifupi napenda kugusia yafuatayo:-

Shabaha, pato halisi la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2014, asilimia 7.4 mwaka 2015, asilimia 7.7 mwaka 2016 na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 8 mwaka 2017. Kuendelea kudhibiti kasi ya upandaji bei ili ibaki kwenye viwango vya tarakimu moja, ambapo mfumuko wa bei unatarajiwa kushuka zaidi kufikia asilimia 5 ifikapo Juni, 2015. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia uwiano wa Pato la Taifa kwa asilimia 18.8 kwa mwaka 2014/2015 na kuimarisha thamani ya shilingi na kuwa na kiwango imara cha ubadilishaji wa fedha kutokana na mwenendo wa soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, malengo: Kuendelea kuimarisha utengemavu wa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii, kuwepo kwa nishati ya umeme wa uhakika, kuendelea kutekeleza vipaumbele vya mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano chini ya dhana ya Matokeo Makubwa Sasa; kuendelea kuimarisha mahusiano na Washirika wa Maendeleo; kuendelea kutekeleza sera ya upelekaji madaraka kwa Wananchi; kuendelea na utekelezaji wa maboresho katika sekta ya umma; na kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele katika Mpango wa Mwaka 2014/2015: Miradi ya Maendeleo katika mwaka 2014/2015 imegawanyika katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni Miradi iliyo chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa iliyoibuliwa kupitia awamu ya kwanza ya uchambuzi wa kimaabara katika sekta za nishati, uchukuzi, kilimo, elimu, maji na utafutaji rasilimali fedha. Kundi la pili linahusisha Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati. Miradi ya Makundi haya mawili inalenga kutekeleza dhamira kuu ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa kutanzua vikwazo vikuu ili kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi. Kundi la tatu linahusisha Miradi mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kuboresha huduma za maji vijijini na mijini. Maji vijijini ambayo ni Miradi iliyo chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa; Serikali itaendelea kumaliza Miradi inayoendelea na kuanza Miradi mipya ya Maji Vijijini. Miradi ya maji mijini itakayotekelezwa ni pamoja na kumaliza kilometa 20.77 za ulazaji wa mabomba ya maji kutoka Ruvu Chini hadi Dar es Salaam na kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji katika Mradi wa Ruvu Juu; kulipa fidia ili kupisha ujenzi wa barabara yenye km 76 kutoka Ngerengere hadi eneo la Bwawa la Kidunda; kuendelea na uchimbaji wa visima 20 katika Mradi wa Kimbiji na Mpera na kuandaa miundombinu ya kusambaza maji; kuendeleza ujenzi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wa Mradi wa Kupeleka Maji Katika Miji ya Same, Mwangi na Korogwe; na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati, Miradi ya Kipaumbele ni pamoja na ile ya kusambaza umeme vijijini, ujenzi wa bomba la gesi (Mtwara – Dar es Salaam); mitambo ya kufua umeme Kinyerezi (MW 150 na MW 240) na Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma (MW 600), Ngaka (MW 400) na Kiwira (MW 200). Aidha, kwa upande wa usafirishaji wa umeme, Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi na uimarishaji wa njia za umeme wa msongo; kV 400 North – West Grid; kV 400 Iringa – Shinyanga; kV 400 Dar es Salaam – Tanga – Arusha; kV 400 Singida – Arusha – Namanga na kV 220 Makambako – Songea.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la miundombinu ya reli, Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kutandika reli na mataruma ya uzito wa ratili 80/yadi kati ya Igalula – Tabora – km 37; kujenga upya vichwa 8; kununua vichwa 11; kununua mabehewa mapya 204 ya mizigo; kutafuta wawekezaji kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa reli (Dar es Salaam – Isaka – Kigali); kukamilisha usanifu kwa Reli ya Tanga – Arusha – Musoma na kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya Reli ya Mtwara – Mbambabay na Liganga – Mchuchuma. Katika eneo la barabara, maeneo yaliyopewa kipaumbele ni barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi, zinazounganisha Tanzania na nchi jirani na zinazosaidia kupunguza msongamano mijini. Hii itajumuisha ujenzi wa km 539 na ukarabati wa km 165 wa barabara kuu kwa kiwango cha lami; ujenzi wa km 20.8 za kiwango cha lami na ukarabati wa km 914.8 za changarawe kwa barabara za mikoa; madaraja na vivuko, yakiwemo madaraja ya Mbutu – Tabora, Maligisu – Mwanza, Kilombero – Morogoro na Kigamboni – Dar es Salaam. Vivuko vitakavyopewa kipaumbele ni pamoja na kununua kivuko kipya cha Magogoni – Kigamboni na Kivuko kipya kitakachotumika kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo, ukarabati wa vivuko vya MV Mwanza (Mwanza), MV Pangani II (Pangani – Tanga), MV Kiu (Kilombero) na MV Magogoni (Dar es Salaam).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari, Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na uendelezaji wa Gati Namba Moja hadi Saba katika Bandari ya Dar es Salaam; ujenzi wa bandari kavu Kisarawe; kutafuta wawekezaji kwa ajili ya Bandari ya Mwambani – Tanga na ile ya Mtwara na Gati 13 hadi 14 Bandari ya Dar es Salaam; na kulipa fidia kupisha ujenzi wa Bandari ya Mbegani – Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, katika usafiri wa anga, maeneo ya kipaumbele ni kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria na miundobinu yake katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere na Kiwanja cha Songwe. Malengo mengine ni kuendelea kukamilisha ujenzi/ukarabati wa viwanja vya Bukoba, Shinyanga, Mwanza, Kigoma, Mpanda, Tabora, Mafia, Arusha, Mtwara na Kilimanjaro. Aidha, Serikali kwa mwaka 2014/2015 itaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa viwanja 11 vya Iringa, Musoma, Kilwa Masoko, Lake Manyara, Moshi, Lindi, Njombe, Songea, Singida, Bariadi na Tanga kwa msaada wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Kilimo, Miradi itakayopewa, kipaumbele ni pamoja na ile iliyo katika Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa, ambayo ni uanzishwaji wa mashamba makubwa 25 kwa ajili ya uwekezaji wa miwa na mpunga; usimamizi wa kitaalamu wa skimu 78 za umwagiliaji za mpunga na kuboresha mfumo wa soko katika skimu hizo; na kuanzishwa kwa maghala biashara (*commercial warehouses*) 275 ya mahindi katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa maghala ya nafaka Songea na Mbozi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja na kuanza na ujenzi wa maghala mengine katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uvuvi hususan eneo la bahari kuu, Serikali itajenga Bandari ya uvuvi ambapo kwa mwaka 2014/2015 itaendelea na utafiti wa kupata eneo kwa ajili

Nakala ya Mtandao (Online Document)

hiyo na kuanza kufanya upembuzi yakinifu. Aidha, uratibu wa shughuli za uvuvi katika eneo la bahari kuu utaimarishwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha marekebisho ya Sheria na Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la viwanda, Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na kuendeleza eneo maalum la uwekezaji Bagamoyo, ambapo kazi zikazofanyika ni kufanya tathmini ya ardhi na mali, kuendelea kulipa fidia na kufanya usanifu wa kina wa miundombinu ya msingi; kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha VIUADUDU Kibaha ukihusisha kuweka miundombinu wezeshi na kuanza uzalishaji; mradi wa chuma Liganga utakaohusisha ujenzi wa mgodi na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha chuma; na ujenzi wa Kituo cha Biashara na Huduma, Kurasini, ukihusisha ulipaji wa fidia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maendeleo ya rasilimali watu, Serikali itaendelea kuboresha ujuzi katika fani mbalimbali hususan za maeneo ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Aidha, jitihada za kuwezesha vijana kusomea fani za mafuta na gesi zitaendelea kupewa kipaumbele. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya wanafunzi 159 watadhaminiwa katika fani za mafuta na gesi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, Wanafunzi 124 watadhaminiwa na Serikali na 35 watadhaminiwa na wahisani. Miradi mingine itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vikuu, ufundi, ustawi wa jamii na ualimu; na kukamilisha mpango kabambe wa uendelezaji wa Kampasi ya Mlonganzila. Aidha, msukumo utawekwa katika mafunzo ya ufundi stadi, yanayokidhi mahitaji ya soko pamoja na mafunzo ya kuongeza ujuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kuboresha huduma za utalii na fedha; ikiwa ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kuanza kutoa huduma, kuimarisha Benki ya Rasilimali Tanzania na Benki ya Wanawake Tanzania. Aidha, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya utalii katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa na ile ya Kitaifa ya kimkakati, Miradi mingine muhimu inayochangia ukuaji wa uchumi itakayozingatwa ni pamoja na kuimarisha sekta ya elimu na mafunzo; mifugo na uvuvi; afya na maendeleo ya jamii; misitu na wanyamapori; ardhi, nyumba na makazi; usafiri wa anga na majini; hali ya hewa; madini; utawala bora ukihusisha masuala ya Bunge na Mahakama; utambulisho wa kitaifa; mchakato wa kupata Katiba Mpya; uimarishaji wa biashara na masoko; uhifadhi wa mazingira; na Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu na nafasi ya sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa biashara na uwekezaji katika sekta binafsi. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaanza utekelezaji wa mapenekezo yaliyotokana na uchambuzi wa kimaabara wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, Serikali itaelekeza rasilimali fedha zaidi katika miradi mahususi ya kufungua uwekezaji wa sekta binafsi (*last mile investments*). Aidha, Serikali itaendelea na juhudi za kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wa shughuli ndogondogo za kati (SMEs) kwa kuwezesha vikundi vya usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo; kuendelea kuboresha huduma na miundombinu ya usafirishaji, nishati na mawasiliano na kuendelea kuboresha mfumo wa usimamizi na kuvutia sekta binafsi ktika utoaji wa huduma hasa elimu na afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 Serikali imekadiria kutumia jumla ya shilingi trilioni 6.44, sawa na asilimia 32.8 ya bajeti yote kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 4.42 sawa na asilimia 68.7 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ndani na shilingi trilioni 2.02 sawa na asilimia 33.3 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje. Serikali itaendelea kugharimia Miradi ya Maendeleo kupitia vyanzo vingine vya fedha kama vile ubia katika ya sekta ya umma na binafsi pamoja na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi kuwekeza katika maeneo ya kipaumbele ya mpango.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Serikali itaendelea na utaratibu wa ufuatiliaji kama ilivyoainishwa katika mwongozo wa Mpango na Bajeti 2014/2015. Katika utaratibu huo, suala la ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya kimkakati litabaki kuwa jukumu la Tume ya Mipango na Sekta husika. Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa itafuatiliwa na PDB; na Miradi ya ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itakuwa ni jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na mikoa husika. Vilevile, Serikali itaendelea kutumia mfumo mpya wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Miradi ya Maendeleo katika mwaka 2014/2015 ili kuleta matokeo makubwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea hali ya Uchumi wa Taifa, matarajio, misingi na malengo, mwenendo wa ukuaji wa uchumi jumla kwa mwaka 2013 na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014, ni dhahiri kuwa, Serikali imepiga hatua za kuridhisha katika kutekeleza Programu/Miradi mbalimbali ya maendeleo. Changamoto kubwa iliyopo ni kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ili ukuaji wa uchumi uweze kuwiana na maendeleo kwa kumnufaisha Mwananchi wa kawaida kuondokana na umaskini.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015 umeandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kwa namna ambayo ni shirikishi ili kupunguza umaskini. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Benki ya Kilimo Tanzania inaanza kufanya kazi ili kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa mikopo kwa wakulima; kuhusisha programu na mikakati ya kinga ya jamii inayosimamiwa na TASAF, ikijumuisha uhawilishaji fedha kwa masharti maalum (*conditional cash transfers*) kwa makundi yenye umaskini uliokithiri; kutekeleza programu za kuwawezesha Wananchi kiuchumi; kuwezesha taasisi za wakulima wadogo kupitia vyama vya ushirika na kilimo cha mkataba; na kuendelea kutekeleza Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge kupitia MKUTABITA.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na utajiri wa rasilimali ya gesi asilia. Kuna haja ya kujipanga vizuri kutumia utajiri huu kwa manufaa ya Wananchi. Katika kufanikisha hili, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kutayarisha nchi kuingia katika uchumi wa gesi ikiwa ni pamoja na kukamilisha Sera ya Gesi Asilia; kuendelea na maandalizi ya Sheria ya Gesi Asilia; Mkakati Kabambe wa Matumizi ya Gesi na Sera ya Ushirikishaji Wananchi Kwenye Biashara ya Gesi (*Local Content Policy*). Aidha, Serikali inapitia Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (*Public – Private Partnership - PPP*) kwa nia ya kuweka mazingira mazuri zaidi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika Miradi ya Maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, dalili nzuri za kuwekeza katika Ukanda wa Kusini (Lindi na Mtwara) zimeanza kuonekana, ambapo ujenzi wa viwanda vya Saruji vya Dangote (Mtwara) na METS (Lindi) unaendelea. Vilevile, maandalizi ya uwekezaji katika viwanda vya mbolea, *Liquified Natural Gas (LNG)*, mitambo ya kufua umeme kutumia gesi asilia na njia za usafirishaji wa umeme katika Ukanda wa Kusini yameanza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, Serikali katika mwaka 2014/2015 itaanza kutekeleza Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana, ili kuboresha upatikanaji wa ajira kwa vijana. Programu hii ni ya miaka mitatu (2014/2015 – 2016/2017), inatarajiwa kusaidia upatikanaji wa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo kwa vijana wanaomaliza elimu katika ngazi mbalimbali. Aidha, programu hii imelenga kuainisha mikakati na hatua mbalimbali za kuchukua ikiwa ni

Nakala ya Mtandao (Online Document)

pamoja na kuweka mgawanyo wa majukumu ya kutekelezwa na sekta na tasisi mbalimbali kuwezesha vijana wengi zaidi kuajiriwa na kujijiri. Vilevile, Serikali imelenga kuendeleza vijana kwa kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, naomba kuwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais (Tume ya Mipango), wakiongozwa na Katibu Mtendaji, Dkt. Philip I. Mpango na Naibu Makatibu Watendaji, kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku za Tume ya Mipango na katika mandalizi ya Hotuba hii. Pia Waziri wa Fedha Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb), Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watenaji wote wa Wizara ya Fedha, kwa kufanya kazi kwa ushirikiano wa hali ya juu na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Gavana wa Benki Kuu, Mtendaji Mkuu wa PDB, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Watendaji wao wote, kwa ushirikiano waliotupatia. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nitoe shukrani za pekee kwa Wananchi wa Jimbo la Bunda, kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kazi za Jimbo pamoja na majukumu mengine ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika naomba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa 2013/2014 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015. Kabla sijatoa hoja, ninaomba kuwatakiwa heri washabiki wote wa mpira, kwa kazi inayoendelea kule Brazil. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, mwendelezo wa mambo haya ya Bajeti, tutakapofika jioni ndipo Waziri wa Fedha atakaposoma Hotuba yake saa 10.00 jioni. Ninawaomba saa 9.30 alasiri muwe mmeshaingia; siyo Waziri wa Fedha anasoma, wameingia watatu, wawili au mmoja, kwa sababu hilo ndiyo hitimisho la kazi yetu ya Bajeti.

Ninawaomba saa 9.30 alasiri muwe mmekaa katika nafasi zenu, saa 10.00 atakapoingia Waziri wa Fedha atukute hapa. Wabunge na Mawaziri wasichelewe. Kwa hiyo, ninaomba leo mfike mapema kwa sababu kuchelewa siyo utaratibu, isipokuwa mmeanzisha tabia ambayo haikubaliki. Tunamshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, kwa kuwasilisha Hotuba yake ya Mpango kwa ajili ya mwaka 2014/2015.

Waheshimiwa Wabunge, kesho asubuhi saa tatu, Kamati ya Uongozi itakuwa ina kikao. Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati mbalimbali.

Ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 5.36 asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali
kwa Mwaka 2014/2015**

Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: *The Gender Budget*. Mheshimiwa Mtoa hoja!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2014/2015. Pamoja na hotuba hii, nimewasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti.

Kitabu cha Kwanza ni makisio ya mapato; Kitabu cha Pili ni makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali; Kitabu cha Tatu ni makisio ya matumizi ya kawaida kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kitabu cha Nne ni makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa wizara, idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2014 ambao ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nikiwasilisha mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Fedha, Wizara ilipata pigo kwa kuondokewa na aliyekuwa Waziri wa Fedha marehemu Dkt. William Augustao Mgimwa. Marehemu Dkt. Mgimwa alikuwa ni mtaalam wa masuala ya fedha, hivyo kwa kipindi kifupi alichokaa Wizarani aliweza kutumia taaluma yake ipasavyo kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kusisitiza ukusanyaji wa mapato ya ndani na nidhamu ya matumizi kwa lengo la kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, aidha, marehemu Dkt. Mgimwa alizingatia sheria, taratibu na kanuni katika kutekeleza majukumu yake ambayo ndio msingi mkuu aliotuachia ambao tunautumia na tutaendelea kuutumia. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani kubwa aliyokuwa nayo kwangu kwa kunitiwa kuwa Waziri wa Fedha. Naahidi kuwa nitatekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa umakini, weledi na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa miongozo yao ya kila wakati katika kufanikisha majukumu ya uandaaji wa bajeti. Vile vile, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Adam Kighoma Malima na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano wake mkubwa aliotupa wakati wa matayarisho ya bajeti hii. Kadhalika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa vikao vya Bunge kwa kuongoza majadiliano vizuri Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani kwa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali kwa kushiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naishukuru Kamati ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge kwa kuchambua kwa kina bajeti za mafungu yote na kutoa mapendekezo na ushauri. Aidha, napenda kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kisekta kwa ushauri na mapendekezo waliyotoa wakati wakichambua rasimu ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha SMT; Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha SMZ; Naibu Makatibu Wakuu; Gavana wa Benki Kuu; Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Viongozi Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara; wakuu wa idara, vitengo na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa waliyoifanya katika maandalizi ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2014 na nyaraka mbalimbali za kisheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii. Vile vile namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha nyaraka zote za Bajeti kwa usahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2014/2015, imezingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Madhumuni ya mipango na mikakati hii ni kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Awamu ya pili ya MKUKUTA inafikia tamati Juni, 2015, hivyo Bajeti hii ni ya mwisho katika utekelezaji wa MKUKUTA II. Aidha, Malengo ya Maendeleo ya Milenia ambayo yametumika kama sehemu ya mikakati yetu ya kupunguza umaskini nayo yanafikia tamati mwaka 2015. Hata hivyo, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 utafikia tamati Juni 2016.

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha kwamba MKUKUTA II utafikia ukomo mwaka mmoja kabla ya ukomo wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo. Kazi iliyo mbele yetu ni kutafuta jinsi masuala ya kupunguza umaskini yatakavyoanishwa katika mikakati na mipango yetu baada ya Juni, 2015 wakati tunaelekea kuhitimisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2016. Hivyo basi, Serikali inafanya mapitio ya MKUKUTA II na kuandaa mapendekezo ya namna ya kuoanisha masuala muhimu ya kupambana na umaskini katika mipango yetu baada ya Juni, 2015. Lengo ni kuwa na Mwongozo mmoja wa kuelekeza shughuli za maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imelenga kupunguza gharama za maisha ya wananchi kwa kuendelea na jitihada za kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei, kuendelea kuboresha huduma za jamii, kuboresha miundombinu ya barabara, umeme na umwagiliaji, kuongeza mishahara ya watumishi wa umma, kuendelea kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi, kuongeza fursa za ajira na kuimarisha utawala bora. Aidha, bajeti hii imezingatia pia maandalizi ya Katiba mpya; uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014; na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Bajeti hii vile vile imelenga kupunguza misamaha ya kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imewasilisha kwenye Bunge hili Muswada wa Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Lengo la Muswada huu ni kupunguza misamaha ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kubakiza misamaha tu yenye tija kwa uchumi na ustawi wa jamii na kuleta usawa na haki katika ulipaji kodi. Aidha, Serikali imewasilisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi hapa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada wa Sheria ya Fedha 2014 tumependekeza pia mabadiliko kadhaa ya Sheria za Kodi, kama nitakavyoeleza baadaye, kwa lengo la kupunguza misamaha hiyo ya kodi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge sote kwa pamoja tuunge mkono jitihada hizi za Serikali ambazo zitasaidia kupunguza misamaha ya kodi na kurahisisha usimamizi wa kodi nchini na hivyo kutoa unafuu kwa walipa kodi, na kuongeza mapato ya Serikali. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, sambamba na kupunguza misamaha ya kodi na kuongeza haki na usawa katika kutoa misamaha hii, kuanzia mwaka 2014/2015, Serikali itachukuwa hatua kuu mbili muhimu. Kwanza, Serikali itakuwa inatoa taarifa ya misamaha ya kodi kila robo mwaka kwa kuwatangaza walionufaika na misamaha kwenye Tovuti ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa hii itajumuisha majina ya watu, taasisi, asasi na makampuni yaliyonufaika na misamaha ya kodi, thamani na sheria iliyotumika kutoa misamaha hiyo. Zoezi hili litahusisha taarifa ya misamaha ya kodi kuanzia mwaka 2010 na kuendelea. Hatua hii itasaidia kuleta uwazi na uwajibikaji katika suala la misamaha ya kodi na kuwafanya wananchi wajue ni nani anayenufaika na misamaha hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kutoa taarifa ya kina ya misamaha yote ya kodi iliyotolewa na kuiwasilisha Bungeni kila mwaka ili Waheshimiwa Wabunge mpate nafasi ya kujadili na kutoa maoni yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imelenga pia kuimarisha zaidi usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma. Ili kutekeleza azma hii, Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti na utakamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2014/2015. Sheria hii inalenga kuongeza nidhamu ya matumizi na uwajibikaji kwa wadau wote wanaotekeleza Bajeti ya Serikali wakiwemo viongozi na maafisa wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge, Mashirika ya Umma, Wakala na Taasisi za Serikali, wakandarasi na wazabuni. Katika kuandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti, wadau muhimu, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, watashirikishwa kupitia Kamati za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo la utekelezaji wa miradi chini ya viwango. Katika kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inawiana na uwekezaji katika miradi husika, Serikali imenunua vifaa vya kuhakiki ubora wa miradi ya maendeleo. Vifaa hivi vitatumika katika uhakiki wa miradi inayotekelezwa na Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, uhakiki huu utasaidia kuhakikisha kuwa, miradi ya maendeleo inayotekelezwa inakuwa ya ubora unaokidhi viwango. Aidha, matumizi ya vifaa hivi yatasaidia kuwabaini wakandarasi dhaifu katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti matumizi na kupata thamani ya fedha katika ununuzi wa bidhaa na huduma, Serikali imeamua kuzingatia ununuzi wa pamoja (*bulk procurement*) kutoka kwa wazalishaji badala ya wakala kama ilivyo sasa na hatua imeanza kuchukuliwa ili ununuzi wa magari na vyombo vya TEHAMA ufuata utaratibu huo. Aidha, kutokana na wingi wa mafuta yanayotumika kwenye magari na mitambo, Serikali itaanzisha mfumo mpya wa kielektroniki utakaotumika katika kununua, kutunza na kuuza bidhaa hiyo ili kuwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika katika ununuzi wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, vile vile, inaelekezwa kwamba vitabu vya kumbukumbu (*diaries*) na kalenda za kila mwaka, zitachapishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tu. Hii ni kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mtaa badala ya utaratibu wa sasa ambapo kila taasisi ya Serikali inachapisha kwa utaratibu wake. Pia, ili kupunguza matumizi ya umeme katika ofisi za Serikali, Serikali inakusudia kutumia vifaa vya umeme vyenye matumizi kidogo ya umeme (*Energy saving technology sensors*). *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ya kudhibiti matumizi ya umma ni kuunganisha matumizi yote ya Wizara, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala na Taasisi za Serikali chini ya mfumo mmoja wa udhibiti wa fedha za Serikali unaosimamiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa, hakuna taasisi yoyote ya umma inayokusanya maduhuli itakayoruhusiwa kutumia fedha walizokusanya kabla ya bajeti yao kupitiwa na kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa maana ya Katibu Mkuu Hazina na fedha zote zinazozidi bajeti iliyoidhinishwa zitawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu unatumiwa na nchi nyingine duniani zikiwemo nchi jirani na kwa hapa Tanzania utaratibu huu unatumika kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hivyo, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2014 una mapendekezo ya kurekebisha sheria zinazohusika ili kuwezesha utekelezaji wa utaratibu huo na naomba Waheshimiwa Wabunge muupitishie kwa kauli moja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kutoa taarifa kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Sera za Bajeti ya mwaka 2013/2014. Mipango na Bajeti ya Serikali mwaka 2013/2014 iliandaliwa kwa kuzingatia mzunguko mpya wa bajeti na sera za uchumi jumla ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato ya jumla ya sh. 18,249,000,000,000 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje na kiasi cha sh. 12,604,000,000,000 kilipangwa kutumika kwenye matumizi ya kawaida na shilingi 5,645, 000,000,000 kwenye matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2014, Serikali imekusanya mapato halisi yenye jumla ya sh. 12,882,000,000,000 sawa na asilimia 70 ya mapato yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, Sera za Mapato. Katika mwaka 2013/2014, sera za mapato zililenga kupanua wigo wa kodi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kugharamia Bajeti ya Serikali. Sera hizo zilijumuisha: marekebisha ya sheria zinazoruhusu misamaha ya kodi kwa lengo la kuipunguza; kuanzisha kituo kimoja cha kutoa huduma za forodha katika bandari ya Dar es Salaam, kuendelea kuanzisha vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mipakani (*One Stop Border Posts*); na kupitua mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo na ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mwenendo wa mapato ya ndani. Sera za mapato zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya sh. 11,154, 000,000,000. Tathmini inaonesha kuwa hadi Aprili 2014, mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 7,771.5, sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka ya shilingi trilioni 10,395.4. Sababu ya kutokufikia lengo ni kutokufanya vizuri kwa baadhi ya vyanzo vya kodi ambavyo vilitarajiwa kuchangia kiasi kikubwa cha mapato. Kutokana na mwenendo huu wa mapato, inategemewa kuwa hadi tarehe 30 Juni, 2014, makusanyo ya mapato yanayotokana na kodi yatafikia asilimia 93 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato yasiyotokana na kodi, hadi Aprili 2014, yalifikia shilingi bilioni 425.5 ikiwa ni asilimia 57 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 741.1 kwa mwaka. Inakadiriwa kuwa, hadi Juni 2014, mapato yasiyo ya kodi yatafikia asilimia 65 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 252.8 zilikusanywa, sawa na asilimia 66 ya makadirio kwa mwaka ya shilingi bilioni 383.5. Sababu ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutofikiwa kwa malengo hayo ni pamoja na kuchelewa kuanza ukusanyaji wa ada ya leseni za biashara na kuchelewa kwa zoezi la kuthamanisha majengo kwa mkupuo (*mass valuation*).

Mheshimiwa Spika, Misaada na Mikopo ya Nje yenye Masharti Nafuu. Katika mwaka 2013/2014, Serikali ilitarajia kupata shilingi trilioni 3,855.2 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2014, misaada na mikopo ya kibajeti iliyopokelewa ni shilingi bilioni 734 sawa na asilimia 63 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Mifuko ya Kisekta, shilingi bilioni 368.6 zilikuwa zimepokelewa, sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka. Aidha, kwa upande wa mikopo na misaada ya miradi ya maendeleo, sh.1,200, 000,000,000 zilipokelewa sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Kibiashara ya Ndani. Katika mwaka 2013/2014, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 1,699.9 kutoka soko la ndani kwa utaratibu wa kuuza hatifungani na dhamana za Serikali za muda mfupi kwa ajili ya kugharamia bajeti yake. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 552.3 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 1,147.6 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2013 – Aprili, 2014, Serikali ilikopa jumla ya shilingi trilioni 1,803.9. Kati ya hizo, shilingi trilioni 1,113.3 zilitumika kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zilizoiva na shilingi bilioni 690.6 zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Kibiashara kutoka Nje. Katika mwaka 2013/2014, Serikali ilipanga kukopa shilingi trilioni 1,156.4 sawa na Dola za Marekani milioni 700 kutoka kwenye masoko ya fedha ya nje ili kugharamia miradi ya maendeleo. Hadi sasa Serikali imepata jumla ya Dola za Marekani milioni 407.9, sawa na asilimia 58 ya makadirio. Dola za Marekani milioni 176.9 zimepatikana kutoka katika Benki ya *Credit Suisse* kwa ajili ya kugharamia miradi ya barabara, maji na reli na Dola za Marekani milioni 83 zimepatikana kutoka Benki ya *Citi* kwa ajili ya kugharamia miradi ya ufuaji umeme inayosimamiwa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itapata Dola za Marekani milioni 148 kutoka Benki ya *HSBC* kwa utaratibu wa *Export Credit Arrangement* kugharamia upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Majadiliano ya kupata kiasi kilichobakia cha Dola za Marekani milioni 292 kwa utaratibu huo huo yanaendelea na yako katika hatua za mwisho yakihusisha Benki za *Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC)* na *Japan Bank for International Cooperation (JBIC)*, kwa ajili ya mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi II wa Megawati 240.

Mheshimiwa Spika, Sera za Matumizi. Katika mwaka 2013/2014, Serikali ilipanga kutekeleza sera za matumizi zifuatazo:-

Kuwianisha matumizi na mapato yaliyotarajiwa, kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia tano ya Pato la Taifa, mafungu kuzingatia viwango vya matumizi vilivyoidhinishwa na Bunge, kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya vipaumbele na kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Matumizi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, Serikali imetoa ridhaa ya matumizi ya shilingi trilioni 13,034.7 sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka. Serikali iliendelea kulipa mishahara ya watumishi wa umma, ambapo hadi Aprili 2014, shilingi trilioni 3,760 zililipwa sawa na asilimia 79 ya bajeti ya mishahara ya mwaka ya shilingi trilioni 4,763.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 1,098 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu, jumla ya shilingi bilioni 92 zilitolewa kwa ajili ya watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 2,097 kwa ajili ya Halmashauri 161 za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Vile vile, Serikali ililipa mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma jumla ya shilingi bilioni 473.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga kutumia shilingi trilioni 3,319.2 kulipa Deni la Taifa na madeni mengine. Hadi kufikia Aprili 2014, malipo ya riba kwa mikopo ya ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 782.7 sawa na asilimia 78 ya makadirio ya shilingi bilioni 998 kwa mwaka. Malipo ya deni halisi la mikopo ya nje yalikuwa shilingi bilioni 139 sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mwaka. Malipo kwa madeni mengine (*CFS others*) yalikuwa shilingi bilioni 750 ikiwa ni asilimia 96 ya bajeti ya mwaka ya shilingi bilioni 783.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiasi cha shilingi trilioni 1,113.3 kilipia hatifungani na dhamana za Serikali zilizoiva sawa na asilimia 97 ya bajeti ya mwaka ya shilingi trilioni 1,148. Matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi trilioni 3,374.7 ikiwa ni asilimia 69 ya makadirio ya shilingi trilioni 4,912 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2014, jumla ya shilingi trilioni 3,115 ziliidhinishwa na kutolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya shilingi trilioni 5,645. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo zilizoidhinishwa na kutolewa, fedha za ndani zilikuwa shilingi trilioni 1,546 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 2,953, sawa na asilimia 52. Aidha, fedha za nje zilikuwa shilingi trilioni 1,569 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi trilioni 2,692 sawa na asilimia 58 ya makadirio ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa nitaelezea kidogo kuhusiana na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Serikali imeendelea kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wenye lengo la kuhakikisha kwamba Hesabu za Majumuisho za Serikali (*Consolidated Financial Statements*) zinaandaliwa kwa kuzingatia mfumo wa Viwango vya Kimataifa Vya Uhasibu (*IPSAS Accrual Basis*). Hatua hizo zinalenga kuunganisha Hesabu za Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Taasisi mbalimbali pamoja na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hii ya Serikali ya kuandaa hesabu za majumuisho, hesabu za mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 kwa Serikali kuu zimeandaliwa kwa kuzingatia mfumo wa *IPSAS Accrual Basis* kwa mara ya kwanza na kuziwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria. Lengo la kutumia mfumo huu ni kuboresha uwazi na uwajibikaji wa Serikali katika matumizi na usimamizi wa rasilimali zake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kwa kupanua mtandao wa malipo ya moja kwa moja kwenye benki – *TISS* katika mikoa 20 ya Tanzania Bara hadi kufikia Mei, 2014 na zoezi linaendelea kwenye mikoa iliyosalia ambapo hadi mwishoni mwa mwezi Juni, 2014, mikoa yote itakuwa imeunganishwa kwenye mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza nidhamu na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma, Serikali imeanza kufanya ukaguzi wa ndani kwa kuzingatia mwongozo wa ukaguzi wa ndani wenye viwango vya Kimataifa ambao ulianza kutumika Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeandaa Mwongozo wa Kamati za Ukaguzi katika Sekta ya Umma kwa lengo la kuboresha utendaji wa Kamati za Ukaguzi na hivyo kuongeza uwazi na uwajibikaji katika mapato na matumizi ya Serikali. Aidha, Serikali imeendelea kuhakiki madai ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

wakandarasi, wazabuni na watumishi, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 58 kimeokolewa katika zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini umeainisha mikakati katika nguzo kuu tatu, ambazo ni Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato, Kuboresha Maisha na Ustawi wa Jamii na Kuimarisha Utawala Bora na Uwajibikaji. Mwaka 2013/14 ulikuwa mwaka wa tatu wa utekelezaji wa MKUKUTA II. Mwenendo wa viashiria vya kupima matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA II katika nguzo kuu tatu nilizozitaja unaonesha mafanikio na changamoto. Baadhi ya matokeo ya viashiria ni kama ifuatavyo:-

Katika nguzo ya kwanza ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato, uchumi umeendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha. Ukuaji huu umeongeza pato halisi la wastani kwa kila Mtanzania hadi kufikia sh. 1,186,200 mwaka 2013 kutoka sh. 1,025,038 mwaka 2012 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 14. Kwa hiyo, pato halisi la wastani kwa kila Mtanzania limekuwa kwa asilimia 14 kutoka sh. 1,025,038 mwaka 2012 na kufikia sh. 1,186,200.

Mheshimiwa Spika, aidha, umaskini wa kipato umeendelea kupungua ambapo kwa mujibu wa takwimu mpya za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya uliofanyika Mwaka 2012, umeonesha kuwa umaskini wa kipato umepungua kwa wastani wa asilimia 6.2 kati ya mwaka 2007 na 2012 kutoka asilimia 34.4 hadi asilimia 28.2. Vile vile, umaskini wa chakula umepungua kwa asilimia 2.1 kati ya mwaka 2007 na 2012 kutoka asilimia 11.8 hadi asilimia 9.7.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utekelezaji katika eneo la kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii, unaridhisha japo umekuwa ukikumbwa na changamoto. Aidha, uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi elimu ya msingi umeimarishwa kutoka 1:47 mwaka 2012 na kufikia 1:43 mwaka 2013 ikilinganishwa na lengo la uwiano wa 1:40. Katika elimu ya sekondari uwiano wa Mwalimu kwa wanafunzi ulifikia lengo la MKUKUTA II la 1:28 mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kuboresha huduma za afya, lishe na upatikanaji wa maji safi na salama zimeendelea kuimarisha ubora wa maisha na ustawi wa jamii. Kwa mujibu wa takwimu mpya za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, vifo vya watoto wachanga vimeendelea kupungua kutoka vifo 51 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2010 hadi vifo 45 mwaka 2012. Umri wa kuishi kwa Mtanzania umeongezeka kutoka wastani wa miaka 51 mwaka 2002 hadi kufikia miaka 61 mwaka 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utawala bora na uwajibikaji, Serikali imeendelea kutekeleza programu za maboresho. Kupitia programu hizi, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuboresha mfumo wa usimamizi wa mali na fedha za umma...

SPIKA: Tulikuwa tunaishi maisha ya kukopa, eeh! Mheshimiwa endelea. *(Makofi/Kicheko)*

WAZIRI WA FEDHA: Mfumo wa sheria na usimamizi wa haki, demokrasia na utoaji huduma za umma kwa jamii. Hatua hizi zimeboresha upatikanaji wa huduma kwa umma, kupanua demokrasia na kuongeza kasi ya utoaji maamuzi ya mashauri katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tuangalie kidogo tathmini ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs). Kuhusu Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Mataifa ikiwemo Tanzania ziliahidhi kutekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia na shabaha zilizowekwa kwa viashiria mbalimbali kwamba ifikapo mwaka 2015, malengo hayo yawe yamefikwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia yanaonesha kuwa, Tanzania imefanya vizuri na inaweza kufikia malengo yafuatayo:-

Elimu ya Msingi kwa Wote, Usawa wa Kijinsia na Fursa Sawa kwa Wanawake, Kupunguza vifo vya akinamama na watoto wachanga na kupunguza maambukizi ya UKIMWI. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea na jitihada za kuhakikisha malengo yaliyobakia yanafikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwenye Sekta ya Fedha, Serikali inaendelea kutekeleza progamu ya maboresho ya sekta ya fedha ili kuhakikisha inachangia kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na hivyo kukuza Pato la Taifa. Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha (*National Financial Inclusion Framework*) ulizinduliwa na Serikali Desemba, 2013 kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanafikiwa na huduma za kifedha zilizo rasmi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ilikamilisha mwongozo wa uwakala wa huduma za kibenki ambao umeiwezesha Benki Kuu ya Tanzania kutoa leseni za uwakala kwa benki za CRDB, Posta, *Equity* na *DCB*. Utaratibu huu wa uwakala umepanua wigo wa huduma za kibenki na hivyo kuwafikia walengwa wengi zaidi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuangalia vikwazo vya upatikanaji wa huduma za fedha nchini, Serikali ilifanya utafiti mwaka 2013. Matokeo ya utafiti huo yalionesha mafanikio yafuatayo:-

Asilimia 13.9 ya wananchi wanatumia huduma za kibenki ikilinganishwa na asilimia 9.2 mwaka 2009. Aidha, asilimia 43.5 ya wananchi wanatumia huduma zisizo za kibenki (Bima, SACCOS na taasisi ndogo za huduma za kifedha na malipo kwa njia ya simu) ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha mwaka 2009 wananchi ambao walikuwa wanatumia huduma za kifedha, lakini siyo huduma za kibenki imeongezeka kutoka asilimia 6.7 hadi kufikia asilimia 43.5. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, asilimia 15.8 ya wananchi wanatumia huduma za kifedha za sekta isiyo rasmi mfano *VICOBA*, *ROSCA* (*Rotating Saving and Credit Association*), *VSLA* (*Village Saving and Lending Association*) ikiwa imepungua ikilinganishwa na asilimia 28.9 mwaka 2009. Kwa ujumla utafiti huu unaonesha kuwa asilimia 57.4 ya wananchi wanapata huduma rasmi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Serikali inatambua kuwa sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi. Ili kutimiza azma hiyo, Serikali imewasilisha Bungeni Muswada wa kurekebisha Sheria ya Ubia Na. 18 ya mwaka 2010 ili kuwezesha utekelezaji wa haraka wa miradi ya PPP. Aidha, Serikali inaazimia kuanzisha Mfuko Maalumu wa Miradi ya Ubia (*PPP Facilitation Fund*) na kuunda Kamati ya Kitaifa ya PPP (*PPP Technical Committee*) pamoja na Kituo cha Miradi ya Ubia (*PPP Centre*).

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye Deni la Taifa. Deni la Taifa linasimamiwa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 na vilevile Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Madeni. Hadi kufikia Machi, 2014, Deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na deni la nje la sekta binafsi lilifikia shilingi bilioni 30,563 ikilinganishwa na shilingi bilioni 23,673.5 la Machi 2013. Kati ya kiasi hicho, deni la Serikali ni shilingi bilioni 26,832.4 na deni la sekta binafsi la nje ni shilingi bilioni 3,730.6.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Deni la Serikali la nje linajumuisha mikopo ya nje kutoka Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, Nchi Wahisani na mabanki ya kibiashara ambapo hadi kufikia Machi, 2014 lilikuwa shilingi bilioni 18,997.6 wakati deni la ndani ni shilingi bilioni 7,834.8. Ongezeko la Deni la Taifa linatokana na kupatikana kwa mikopo mipya, kupokelewa kwa fedha za mikopo ya nyuma kwa kipindi husika vile vile kushuka kwa thamani ya shilingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuangalia deni la Taifa sasa tuangalie uhimilivu wake. Ili kuhakikisha Deni la Taifa linaendelea kuhimilika, Serikali imekuwa ikikopa na kuwekeza katika miradi ya kuchochea ukuaji wa uchumi ili kuwa na uwezo wa kuyalipa madeni hayo pindi yanapoiva. Aidha, Serikali imejiwekea utaratibu wa kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni kila mwaka kwa mujibu wa sheria ili kubainisha hali halisi ya deni na uwezo wa nchi kulipa madeni hayo katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utaratibu huo mwezi Septemba, 2013, Serikali ilifanya tathmini ya uhimilivu wa deni kwa kutumia viashiria vilivyokubalika Kimataifa. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa Deni la Taifa ilibainisha kuwa Deni la Taifa ni himilivu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tathmini hiyo, viashiria vyote vya kupima uhimilivu wa deni viko katika wigo unaokubalika Kimataifa (*debt sustainability thresholds*). Baadhi ya viashiria hivyo ni uwiano wa thamani ya sasa ya Deni la Taifa la nje (*Present Value of External Debt*) kwa uwiano wa Pato la Taifa ni asilimia 24.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 121.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 300. Uwiano wa thamani ya ulipaji wa deni la nje kwa thamani ya mapato ya mauzo nje ya nchi ni asilimia 3.34 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 25. Uwiano kati ya ulipaji wa deni kwa mapato ya ndani ni asilimia 4.32 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 22 na uwiano wa deni la Serikali likijumuisha dhamana za Serikali kwa taasisi mbalimbali kwa Pato la Taifa ni asilimia 35.58 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 74. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa deni la Taifa linaendelea kuwa himilivu kwa kuendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukopa mikopo yenye masharti nafuu na kuhakikisha kuwa fedha zitokanazo na mikopo hiyo zinaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Serikali pia inaweka ukomo wa mikopo yenye masharti ya kibiashara bila kuathiri uhimilivu wa deni. Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza uamuzi wake wa kusitisha utoaji wa dhamana kwa taasisi, mashirika, idara na Wakala wa Serikali zinazopata ruzuku kutoka Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuangalie kwa ufupi tu utekelezaji wa Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*). Katika mwaka 2013/2014, Serikali ilianzisha utaratibu madhubuti wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi hiyo katika mpango wa maendeleo ujulikanao kama Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha utaratibu huu ni kuongeza kasi katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambapo Tanzania inatarajiwa kuwa nchi ya kipato cha kati. Ili kuleta tija na ufanisi utekelezaji wa *BRN* unahusisha maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni:- Kilimo, Elimu, Maji, Nishati, Miundombinu na Utafutaji wa Rasilimali Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maamuzi yaliyofanyika kwenye maabara ya utafutaji wa rasilimali fedha, Wizara ya Fedha ilipewa lengo la kuongeza mapato mapya kwa jumla ya shilingi trilioni 1,160 kwa mwaka 2013/2014; kupunguza nakisi ya bajeti kutoka asilimia

Nakala ya Mtandao (Online Document)

6.8 hadi asilimia 5.5 ya Pato la Taifa; kudhibiti matumizi na kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi ya BRN katika sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, jumla ya shilingi trilioni 1,700 zilitengwa kwenye bajeti kupitia miradi mbalimbali ya sekta zinazotekeleza miradi ya BRN. Hadi kufikia Aprili, 2014, mafungu yanayotekeleza miradi ya BRN yamepatiwa jumla ya shilingi trilioni 1,566.7 sawa na asilimia 92 ya bajeti ya miradi ya BRN kwa mwaka 2013/2014. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya maji viijini shilingi bilioni 226.1; Elimu shilingi bilioni 48.4; Nishati shilingi bilioni 577.5; Uchukuzi ikijumuisha miundombinu ya barabara na reli shilingi bilioni 663.6; na Kilimo shilingi bilioni 51.1.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tuelezee mafanikio na changamoto katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2013/2014. Katika kipindi cha miezi kumi ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali imefanikiwa kutekeleza shughuli muhimu za bajeti licha ya kukabiliwa na changamoto kama ilivyoielezwa katika hotuba za mipango na bajeti za Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ambazo Bunge lako Tukufu limejadili kwa kina na kuzipitisha. Aidha, Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu imeelezea mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia hatua hiyo, nitaeleza kwa kifupi baadhi ya mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi. Katika mwaka 2013 Pato halisi la Taifa limekua kwa asilimia 7.0 ambayo ni sawa na lengo lililowekwa. Aidha, kwa mwaka 2012 ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 6.9 na asilimia 6.4 mwaka 2011. Mafanikio haya yanatokana na juhudi za Serikali katika kuimarisha uchumi tulivu na utawala bora ambazo ni nguzo muhimu katika kuvutia uwekezaji nchini. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya mwezi Aprili 2014, Tanzania ni nchi ya nane katika ukuaji wa uchumi katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na ya kwanza katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa ajira hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, jumla ya ajira mpya 630,616 zilikuwa zimezalishwa nchini katika sekta ya umma na sekta binafsi. Kati ya ajira hizo zilizozalishwa, sekta ya elimu ilizalisha ajira 36,073; Afya ajira 11,221; Kilimo ajira 130,974; Ujenzi wa miundombinu ajira 32,132; Nishati na Madini ajira 453; na Mawasiliano ajira 13,619. Aidha, kati ya ajira hizo, Serikali kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliajiri watu 3,055. Nafasi hizi ni nje ya nafasi zinazohusu sekta ya afya na elimu. Ajira zilizozalishwa katika sekta binafsi zilikuwa 211,970.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei nchini umeendelea kushuka kutoka asilimia 9.4 Aprili, 2013 hadi kufikia asilimia 6.3 Aprili, 2014. Lengo lililowekwa la mfumuko wa bei hadi Juni, 2014 ni asilimia sita, ambalo kuna uwezekano wa kulifikia. Kupungua kwa kasi ya upandaji bei kulitokana hasa na sera madhubuti za fedha, hali nzuri ya hewa; jitihada za Serikali kuongeza ruzuku ya pembejeo za kilimo na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao; kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika nchi jirani; pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, hali ya akiba ya fedha za kigeni mpaka mwisho wa mwezi Aprili, 2014 iliendelea kuwa ya kuridhisha. Katika kipindi kilichoishia Aprili, 2014, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 4,647.5 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 4,380.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka 2014 kinatosheleza uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi 4.6 ikilinganishwa la lengo la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma la miezi minne hadi Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na Serikali kugharamia shughuli za Tume ya Mabadiliko ya Katiba pamoja na uendeshaji wa Bunge Maalum la Katiba; kulipa mishahara ya watumishi kwa wakati; Ujenzi na utandazaji wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam umeendelea kutekelezwa kama ilivyopangwa; ujenzi na ukarabati wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

miundombinu mbalimbali unaendelea kufanyika; fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ilitolewa kwa wakati; kugharamia ununuzi wa chakula cha hifadhi ya Taifa; kuendelea kugharamia huduma za jamii; na ununuzi wa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, bajeti hii vile vile imeendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali:-

- (1) Upatikanaji kwa wakati wa mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara; kuwepo kwa mahitaji makubwa ya fedha ikilinganishwa na upatikanaji wa mapato;
- (2) ukusanyaji usioridhisha wa mapato yasiyo ya kodi;
- (3) Gharama kubwa za uendeshaji wa mitambo ya kufua umeme wa dharura; kuongezeka kwa madai ya wakandarasi, wazabuni na watumishi; na
- (4) Kutokamilika kwa urasimishaji wa sekta isiyo rasmi na hivyo kusababisha ugumu wa kutoza kodi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto nilizozieleza, Serikali itaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu na faida za kulipa kodi kwa kutumia mitandao ya kielektroniki na kusimamia ulipaji kodi kwa hiari kupitia udhibiti wa matumizi ya mfumo wa Mashine za Kielektroniki za Kutoa risiti (*Electronic Fiscal Devices*) ambao umeboreshwa zaidi na kuboresha vile vile ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kutumia TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa bajeti, Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti. Kuhusu madai ya Wakandarasi na Wazabuni, Serikali inakamilisha utaratibu wa kusimamia na kuyalipa madai yaliyohakikiwa kupitia Hazina kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zinazohusika. Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza Wizara na Taasisi kuzingatia mfumo wa malipo (*IFMS*) ambao unamtaka kila Afisa Masuuli kutoingia mikataba bila kuwa na *LPO* inayotokana na mfumo wa *IFMS*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo ya nje, Serikali itaendelea kufanya majadiliano mapema na wahisani pamoja na mabenki ili kuhakikisha kwamba fedha za misaada na mikopo zinapatikana kama ilivyopangwa na kwa wakati. Aidha, Serikali itahakikisha inazingatia na kutekeleza kwa haraka masharti ya fedha za wahisani kulingana na makubaliano.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tujielekeze kwenye bajeti ya mwaka 2014/2015. Bajeti ya mwaka 2014/2015, itaendelea kuzingatia vipaumbele vilivyodainishwa kwenye: Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010; Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015 na Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now – BRN*); Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (*MKUKUTA II*); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; na Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma. Lengo likiwa ni kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, shabaha na misingi ya Bajeti kwa mwaka 2014/2015. Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2014/15 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Pato halisi la Taifa linatarajia kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2014 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 7.7 kwa mwaka katika kipindi cha muda wa kati;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya upandaji bei ili ibaki kwenye viwango vya tarakimu moja, ambapo maoteo kwa kipindi kinachoishia Juni, 2014 ni asilimia sita na asilimia tano Juni, 2015;
- (iii) Kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano wa asilimia 18.9 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2014/2015;
- (iv) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 4.9 ya Pato la Taifa mwaka 2014/2015;
- (v) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) katika wigo wa asilimia 15.5 kwa mwaka unaoishia Juni 2015, utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei;
- (vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne kwa mwaka unaoishia Juni 2015; na
- (vii) Kuimarisha thamani ya shilingi na kuwa na kiwango imara cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia shabaha na malengo yaliyoainishwa, misingi ya Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, utulivu na utengamano nchini, kikanda na duniani kote;
- (ii) Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, biashara ya nje na huduma za kifedha;
- (iii) Mapato ya ndani yataongezeka kwa kuimarisha vyanzo vilivyopo na kubuni vyanzo vipya vya mapato na kupunguza misamaha ya kodi na kuongeza usimamizi;
- (iv) Kuimarisha mfumo wa usimamizi na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma;
- (v) Mfumo wa *IFMS* utaimarishwa na kuhakikisha unatumika kuweka mihadi ya huduma na bidhaa kabla ya malipo kuzingatia vipaumbele vilivyopo katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, MKUKUTA II pamoja na miradi itakayokuwepo katika "Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa";
- (vi) Sera za fedha zitaendelea kuimarishwa ili ziendane na sera za bajeti zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na tofauti ya riba za amana na za mikopo;
- (vii) Mtengamano wa kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC utaendelezwa na kutumia vizuri fursa zilizopo; na
- (viii) Mazingira ya biashara na uwekezaji yataendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vya utekelezaji wa Sheria ya PPP ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Sera za Mapato. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali za kiseru na kiutawala kwa kupanua wigo wa kodi, kubuni vyanzo vipya vya mapato, kuimarisha usimamizi wa kodi, kupunguza misamaha ya kodi inayotolewa kupitia sheria mbalimbali za kodi ikiwemo sheria ya VAT. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na wadau mbalimbali ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Bunge, kikosi cha wataalam (*Lab*) cha kubuni vyanzo vya mapato katika mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Spika, hatua za kiseru za kuongeza mapato zitakazozingatiwa kwenye Bajeti ya mwaka 2014/15 ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, Sera za mapato katika mwaka 2014/2015, zinalenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi trilioni 12,178.0 sawa na asilimia 19.2 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 11,318.2 na mapato yasiyo ya kodi ni shilingi trilioni 859.8. Mapato yanayotokana na vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 458.5 ambayo ni sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kupata misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ili kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Kwa mwaka 2014/2015, Serikali inatarajia kupokea misaada na mikopo ya masharti nafuu ya kiasi cha shilingi trilioni 2,941.5. Kati ya fedha hizo misaada na mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 922.1, Mifuko ya Kisekta shilingi bilioni 274.1 na miradi ya maendeleo shilingi trilioni 1,745.3

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itakamilisha na kuanza kutumia mwongozo mpya wa Ushirikiano katika Maendeleo. Mwongozo huu unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana chini ya MPAMITA na uwekaji wa misingi mipya hususan ufanisi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii (*Development Effectiveness*). Aidha, mwongozo huu unaainisha misingi ya majadiliano baina ya Serikali na wadau wa maendeleo ili misaada na mikopo inayotolewa iweze kuleta tija na matokeo yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi zao za kuchangia maendeleo yetu, naomba kuwatambua na kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kama ifuatavyo:-

Nchi za Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, India, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi, pia taasisi mbalimbali za Kimataifa ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) Benki ya Dunia (*World Bank*), Benki ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (*BADEA*), *Global Fund*, *OPEC Fund*, *Saudi Fund*, Umoja wa Ulaya, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Mbali na michango yao ya kifedha, Serikali pia inanufaika kutokana na ushauri na mawazo yao katika kutekeleza programu mbalimbali. Tunawashukuru na kuthamini mchango wao. (*Makofi*)

- (i) Kuimarisha taratibu za kukusanya mapato pamoja na kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi kwa kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo;
- (ii) Kuongeza usajili wa walipa kodi wapya na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (iii) Mamlaka ya Mapato Tanzania itaongeza siku za kufanya kazi ili kutoa muda wa ziada wa kuwahudumia walipa kodi bandarini na baadhi ya vituo vya mpakani; (*Makofi*)
- (iv) Kukamilisha utungwaji na kuanza kutekeleza Sheria Mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT);
- (v) Kukamilisha utungwaji wa Sheria ya Usimamizi wa kodi (*Tax Administration Act*);
- (vi) Kuendelea kuimarisha na kusisitiza matumizi ya mashine za elektroniki za kutoa stakabadhi za kodi (*Electronic Fiscal Devices-EFDs*) na kutoa elimu zaidi kwa walipa kodi na wafanyabiashara kuhusu matumizi ya mashine hizo;
- (vii) Kufuatia kukamilika kwa utafiti wa kuwianisha mifumo ya ukuanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, Serikali itaandaa mfumo wa usimamizi na utaratibu wa kukusanya;
- (viii) Kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iingie kwenye mfumo rasmi wa kodi;
- (ix) Taasisi, wakala na mamlaka za Serikali kuwasilisha maduhuli yote kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia mfumo wa *retention*;
- (x) Ili kukabiliana na ukwepaji kodi, Wizara ya Fedha itatoa namba maalum ya simu na anwani ya barua pepe ili kuwawezesha raia wema kutoa taarifa mbalimbali kuhusu ukwepaji kodi; na
- (xi) Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa, Manispaa, Majiji, Halmashauri, Wakala na Taasisi, Mamlaka zinazokusanya maduhuli na malipo mengine zinaagizwa kutumia mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha ukusanyaji na kupunguza upotevu wa mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Kibiashara ya Ndani na Nje. Kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya kuendeleza miradi ya miundombinu nchini, Serikali itaendelea kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo. Katika mwaka 2014/2015, Serikali inategemea kukopa katika soko la ndani jumla ya shilingi trilioni 2,955.2. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 689.56 sawa na asilimia 1.1 ya Pato la Taifa ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi trilioni 2,265.7 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva kwa utaratibu wa *rollover*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 1,320.0 kutoka masoko ya fedha ya nje kwa masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Uamuzi wa kuendelea kukopa kwa masharti nafuu na ya kibiashara umezingatia tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa na umuhimu wa kuendeleza miradi ya kipaumbele hususan miundombinu ambayo itafungua fursa za kiuchumi na kuwa kichocheo kikubwa cha ukwaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sera za Matumizi. Katika mwaka 2014/2015, Serikali imekadiria kutumia jumla ya shilingi trilioni 19,853.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Katika kipindi hiki mgawanyo wa matumizi ya Serikali utakuwa kama ifuatavyo: Matumizi ya kawaida shilingi trilioni 13,408.2 na matumizi ya maendeleo jumla ya shilingi trilioni 6,445.1, sawa na asilimia 32.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itatekeleza sera za matumizi zifuatazo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

- (i) Utoaji wa fedha kwa Mafungu utazingatia maombi na uwasilishwaji wa taarifa za matumizi (*performance based disbursement*) katika matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kila robo ya mwaka;
- (ii) Kuwianisha matumizi na mapato yanayotarajiwa;
- (iii) Kuimarisha zaidi usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, ikiwa ni pamoja na kuandaa Sheria ya Bajeti;
- (iv) Taasisi zitumie Wakala wa Serikali mtandao (*E-Government Agency*) katika kuweka mifumo ya TEHAMA kwenye Taasisi zao ili kupunguza gharama za washauri kutoka nje; (*Makofi*)
- (v) Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri, Wakala na Taasisi za Serikali zitafanya manunuzi yote kupitia Mfumo wa EFDs, hivyo kuambatisha risiti zinazotokana na mashine za kielektroniki (EFDs);
- (vi) Malipo yote ya Serikali yatalipwa kupitia akaunti moja ya Serikali iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (*Single Treasury Account*);
- (vii) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haitazidi asilimia 4.9 ya Pato la Taifa;
- (viii) Mafungu yatazingatia matumizi yaliyokusudiwa pamoja na viwango vilivyoidhinishwa na Bunge;
- (ix) Kutenga fedha za kutosha katika kutekeleza miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo;
- (x) Bajeti za Taasisi, Wakala na Mamlaka za Serikali zitawasilishwa na kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali;
- (xi) Madai ya wakandarasi, wazabuni na watumishi yatahakikiwa na kulipwa na Wizara ya Fedha kwa kuzingatia bajeti za mafungu husika;
- (xii) Serikali itazingatia ununuzi wa pamoja kutoka kwa wazalishaji badala ya Wakala; na
- (xiii) Matumizi yatazingatia Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2004 na manunuzi yatazingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, sasa twende kwenye mgawanyo wa fedha katika baadhi ya sekta. Katika mwaka 2014/2015 mgawanyo wa bajeti kwa sekta ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Nishati na Madini: jumla ya shilingi trilioni moja na milioni tisini zimetengwa. Shilingi bilioni 290.2 zimetengwa kwa Wakala wa Umeme Vijijini kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini; shilingi bilioni 151 kukamilisha ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam; na shilingi bilioni 90 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia Gesi wa Kinyerezi I.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hatua hii inalenga kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na kupunguza gharama zake na hivyo kuvutia uwekezaji na kuongeza ajira, jumla hii ya shilingi trilioni moja na milioni tisini hazijumuishi fedha zinazokwenda kwenye sekta ambazo fedha hizo ziko katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, ni bajeti hii lakini hazijumuishi fedha ambazo zitakwenda kulipia madeni ya miradi ya maendeleo ya Sekta husika ambazo zimetengwa katika Mfumo Mkuu wa Serikali. Hii Nishati na Madini kwa mwaka huu ni sawa na 7% ya bajeti, lakini kumekuwa na ongezeko ukilinganisha na mwaka jana.

Miundombinu ya usafirishaji: jumla ya shilingi bilioni 2,109.0 zimetengwa, ambapo shilingi bilioni 179.0 kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa na ukarabati wa reli ya kati na shilingi trilioni moja bilioni 1,414.8 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja. Azma hii inalenga kupunguza msongamano wa magari mijini, gharama za usafiri na usafirishaji wa bidhaa na huduma na hivyo kupunguza mfumuko wa bei. Tunaomba kusisitiza kwamba fedha hizi hazijumuishi fedha ambazo zinakwenda kwenye sekta ambazo zimo kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kilimo; jumla ya shilingi trilioni moja bilioni 1,084.7 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya SAGCOT; ujenzi wa maghala na masoko; na upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kukua uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwekeza kwenye ugani kwa kuimarisha Vyu vya Utafiti katika kilimo na kuhakikisha kunakuwa na Maafisa Ugani wa kutosha na mbegu bora. Hatua hii itaimarisha uzalishaji wa mazao, usalama wa chakula na kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika;

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Elimu kwa mwaka huu ukitoa fedha zilizoko katika Mfuko Mkuu wa Serikali sekta ya elimu imetengewa jumla ya shilingi trilioni 3,465.1 sawa na 23% ya bajeti ambapo shilingi bilioni 307.3 zimetengwa kugharamia mikopo ya elimu ya juu. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha ubora wa elimu ikijumuisha miundombinu ya elimu. Hatua hii itasaidia upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kuimarisha na kujenga madarasa na maabara. Ili kuhakikisha vijana wetu wanapata fursa za ajira, juhudi zitawekwa pia kwenye kuimarisha Vyu vya Ufundi Stadi (VETA);

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maji; jumla ya shilingi bilioni 665.1 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa visima katika Vijiji 10 kwa kila Halmashauri na kukamilisha ujenzi wa bomba la maji kutoka Ruvu Chini hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itawaondolea wananchi kero ya kufuata maji mbali na makazi yao na hivyo kupata muda wa shughuli nyingine za uzalishaji, na kuwaondolea hatari ya kupata magonjwa kwa kutumia maji yasiyo salama;

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afya; jumla ya shilingi trilioni 1,588.2 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa madawa, kuzuia magonjwa ya mlipuko, chanjo za watoto, ujenzi wa zahanati na kudhibiti UKIMWI na Malaria. Kumekuwa na ongezeko mwaka huu ambao tunamalizia kumetengwa shilingi trilioni moja bilioni mia nne tisini na saba nukta nane na mwaka

Nakala ya Mtandao (Online Document)

huu kumekuwa kuna ongezeko kwa hiyo, sasa hivi tumetenga shilingi trilioni moja, milioni mia tano themanini na nane nukta mbili kwa kujua kwa makusudi umuhimu wa afya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utawala Bora, jumla ya shilingi bilioni 579.4 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha Utawala Bora ikijumuisha kugharamia Bunge Maalum la Katiba; vitambulisho vya Taifa; uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2014; kuhuisha daftari la wapiga kura; maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015; mapambano dhidi ya rushwa na utoaji wa haki kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo huu wa kisékta kama nilivyosema awali haujumuishi madeni ya kisékta yanayolipwa kupitia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS).

Mheshimiwa Spika, masuala yanayohusu Mamlaka ya Serikali za Mitaa; katika mwaka 2014/2015, Mikoa na Halmashauri zimetengewa shilingi bilioni 4,499 ikiwa ni nyongeza ya shilingi bilioni 685.87 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2013/2014 ya shilingi trilioni 3,813. Nyongeza hii ni sawa na asilimia 18%. Aidha, mapato ya ndani ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka kwa shilingi bilioni 85.9 kutoka shilingi bilioni 372.6 mwaka 2013/2014 hadi shilingi bilioni 458.5 katika mwaka 2014/2015. Ongezeko hili la mapato ya ndani ni sawa na asilimia 23%.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, shilingi bilioni 46.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri mpya ambapo kila Halmashauri imetengewa shilingi bilioni 1.5. Aidha, shilingi bilioni 9.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Wakuu wa Wilaya katika maeneo hayo. Serikali itaendelea kuziwezesha Halmashauri hizo kupata nyenzo muhimu za utendaji kazi katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka 2014/2015, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa Halmashauri zenye mazingira magumu katika ujenzi wa nyumba za watumishi, ofisi, hospitali, hosteli, madaraja, barabara pamoja na miradi mingine maalum yenye kulenga kutoa huduma za haraka kwa wananchi ikiwemo maji, elimu na afya. Shilingi bilioni 53.99 zimetengwa katika mwaka ujao wa fedha kwa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, shilingi bilioni 8.7 zimetengwa kwa ajili ya kazi za ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Mikoa tisa nchini. Mikoa hiyo ni Katavi, Simiyu, Njombe, Geita, Arusha, Pwani, Kilimanjaro, Singida na Tabora. Ni matumaini yangu kuwa kukamilika kwa kazi hizi kutaimarisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, matumizi kwa makundi maalum; Serikali inatambua kero mbalimbali zinazowakabili Walimu hususan Walimu wa shule za msingi. Ili kukabiliana na kero hizo, Serikali imejipanga kuziondoa kero hizo kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

- (i) Ujenzi wa nyumba za Walimu: Serikali inaendelea na utaratibu wa ujenzi wa nyumba za Walimu kwa awamu. Katika mwaka 2013/2014, Halmashauri 40 zilipewa kila moja shilingi milioni 500 ili zianze ujenzi wa nyumba za Walimu na kiasi kama hicho kitatolewa kwa Halmashauri hizo kwa mwaka 2014/15. Aidha, shilingi milioni 500 zitatolewa kwa Halmashauri 80 zaidi, hivyo kufanya jumla ya Halmashauri 120 kunufaika na utaratibu huo, lengo likiwa ni kuzifikia Halmashauri zote mwaka 2015/2016. Viongozi wa Serikali katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Kata wanahimizwa kusimamia kikamilifu fedha hizo ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.
- (ii) Malipo ya madai ya Walimu: Serikali inaendelea na utaratibu wa kulipa madai ya Walimu yaliyohakikiwa, ambapo katika mwaka 2013/2014, kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kimelipwa.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Aidha, kwa mwaka 2014/2015, madai ya Walimu ambayo yatakuwa yamehakikiwa yataendelea kulipwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea kuboresha huduma kwa wanafunzi katika shule na vyuo mbalimbali ili kuhakikisha vijana wetu wanasoma katika mazingira tulivu na bora. Ili kutekeleza hili, Serikali imepanga yafuatayo:-

- (i) Kujenga maabara katika shule na vyuo na kuzipatia vifaa muhimu ikiwa ni pamoja na kutumia maabara zinazotembea ili kuwafikia wanafunzi wengi zaidi;
- (ii) Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi waliopo vyuoni na watakaojiunga na vyuo vya elimu ya juu; na
- (iii) Kujenga maktaba mpya, kukarabati na kuimarisha zilizopo kwa kuzipatia vitabu zaidi vya kiada na ziada.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazovikabili vyombo vya ulinzi na usalama, ikiwa ni pamoja na makazi na mahitaji mengine. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imepanga kutekeleza yafuatayo katika mwaka 2014/2015:

- (i) kuendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za askari katika maeneo mbalimbali nchini ambapo jumla ya shilingi bilioni 27.13 zimetengwa kwa ajili hiyo;
- (ii) Kuendelea kuwapatia vitendea kazi; na
- (iii) Kuendelea kuongeza mishahara ya askari na stahili nyingine kwa awamu kulingana na uwezo wa kibajeti katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na kuongeza mishahara. Katika kuendelea na jitihada hizo, katika mwaka 2014/2015, Serikali imepanga yafuatayo:-

- (i) Kuongeza kima cha chini cha mishahara kwa watumishi wa umma; na
- (ii) Kufanya marekebisho katika mfumo wa kodi ya mishahara (*Pay As You Earn*) kwa kupunguza kiwango cha kodi hadi kufikia kima cha chini cha kodi cha asilimia 12, kutoka asilimia 13 ambapo kiwango hicho kilikuwa asilimia 18.5 mwaka 2005/2006 na kupunguzwa hadi asilimia 13 mwaka 2013/2014. Lengo tutaendelea kupunguza taratibu hadi kufikia tarakimu moja.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wastaafu ambao walitoa mchango mkubwa kwa Taifa hili. Kwa sasa wastaafu hawa wapo katika makundi mawili ambayo ni wastaafu wa Serikali ambao hawakuchangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanaolipwa sh. 50,000 kwa mwezi na aina ya pili ni wastaafu ambao pensheni zao zinategemea michango yao katika Mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa viwango vinavyolipwa kwa sasa haviendani na uhalisia. Katika kutatua changamoto hii Serikali inapitia viwango hivyo ili kuongeza viwango kutegemeana na mapato ya Serikali na kuhakikisha malipo yanafanyika kwa wakati. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaendelea kuhuisha kanuni za ukotoaji wa mafao ili kuweka ulinganifu wa mafao katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Ununuzi wa Umma; katika mwaka 2014/2015, Serikali kupitia taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. (7) ya Mwaka, 2011 ambayo imeanza kutumika Desemba, 2013 baada ya kanuni kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo itaondoa changamoto mbalimbali zilizokuwepo katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 zikiwemo bei kubwa ya bidhaa ikilinganishwa na bei halisi ya soko pamoja na mchakato mrefu wa zabuni. Hivyo, nitoe wito kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali na Halmashauri zote na wadau wote kwa ujumla kuitumia Sheria hii kikamilifu. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuondokana na kasoro na malalamiko yaliyokuwepo hapo awali.

Mheshimiwa Spika, eneo la sekta ya fedha; katika mwaka 2014/2015, Serikali itakamilisha Sera na Mkakati wa Sekta ya Bima ili kutoa mwongozo wa kufidia hasara zinazotokana na majanga mbalimbali. Aidha, Serikali itakamilisha Sera ya Taifa ya Taasisi Ndogo za Huduma za Kifedha na kutunga Sheria ya Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali inaandaa mapendekezo ya kutunga sheria ya mifumo ya malipo ili kuboresha matumizi ya kieletroniki kufanya malipo kwa kutumia simu za mkononi, huduma za benki kwa njia ya mtandao, vituo vya mauzo na mashine za kutolea fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua athari za riba kubwa zinazotozwa na benki na taasisi za fedha kwa mikopo itolewayo ambazo zinasababisha asilimia kubwa ya Watanzania kushindwa kufaidika na huduma za kifedha. Serikali imeanza kuchukua hatua za kutatua changamoto hizo kama ifuatavyo:-

Kutekeleza programu ya kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge, kuanzisha taasisi inayotoa mikopo ya nyumba, kuendelea na zoezi la kutoa vitambulisho vya Taifa na anwani za makazi, kuchochea utumiaji wa Taasisi ya Kuhakiki Ukweli wa Taarifa za Waombaji Mikopo (*Credit Reference Bureau*), na kuimarisha mifuko ya dhamana ya mikopo inayosimamiwa na Benki Kuu. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu pamoja na wadau wengine itafanya tathmini ya viwango vya riba ili kuweza kubainisha sababu za viwango kuendelea kuwa juu na kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kikanda; Ushiriki wa nchi yetu katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika SADC unazidi kuimarika, hasa baada ya kusainiwa, kuridhiwa na kutekelezwa kwa itifaki muhimu za biashara na uchumi. Hatua hizi zitaongeza fursa za uwekezaji na hivyo kukuza uchumi na kuongeza upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, naomba kutoa taarifa kwamba mtangamano umefikia hatua ya kuanzishwa kwa Umoja wa Fedha ambapo Itifaki ya kuanzisha Umoja huo ilisainiwa na Wakuu wa nchi za Jumuiya mnamo tarehe 30 Novemba 2013. Ili kuimarisha ushirikiano katika hatua zilizofikiwa, Benki Kuu za Nchi Wanachama zimekubaliana kurahisisha taratibu za kufanya malipo kati ya nchi zetu (*cross border payments*), hivyo kuwezesha malipo kati ya nchi zetu kuwa rahisi na hivyo kuhamasisha utumaji wa fedha na biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha, naomba kutoa taarifa kwamba Serikali inakamilisha maandalizi ambapo kuanzia tarehe 1 Julai, 2014 mizigo inayokwenda nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki itakaguliwa mara moja katika

Nakala ya Mtandao (Online Document)

bandari ya Dar es Salaam na kuruhusiwa baada ya nchi husika kuthibitisha kwa Mamlaka ya Mapato kwamba kodi imelipwa.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itapunguza muda wa mizigo hiyo kukaa bandarini, hivyo kupunguza gharama kwa wafanyabiashara na kuhamasisha ukusanyaji wa mapato na ukuaji wa uchumi wa nchi zetu. Kwa upande wa Itifaki ya Soko la Pamoja, naomba kutoa taarifa kwamba utekelezaji unaendelea na Serikali imetoa tangazo la kupunguza masharti ya uwekezaji wa mitaji baina ya nchi wanachama. Kuhusu kuwianisha kodi za ndani, majadiliano ya kupata mfumo bora wa kuwianisha kodi hizo yanaendelea na yatakapokamilika Bunge lako Tukufu litajulishwa.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuhamasisha biashara sawia baina ya nchi wanachama kwa kuwa na taratibu za kodi na viwango vya kodi za ndani visivyotofautiana. Kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), naomba kutoa taarifa kwamba Serikali inaendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara. Aidha, napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuridhia Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ya nchi za SADC.

Mheshimiwa Spika, uhusiano Kati ya Tanzania na Shirika la Fedha la Kimataifa kupitia Mpango wa Ushauri wa Kiseru (*Policy Support Instrument-PSI*) Tanzania imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) kupitia mpango wa Ushauri wa Kiseru ujulikanao kama *Policy Support Instrument-PSI*. Tanzania ilifanikiwa kujiunga na Mpango huu kutokana na juhudi zinazofanyika za kuimarisha uchumi tulivu na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa kwanza wa PSI ulianza kutekelezwa Februari, 2007 hadi Juni, 2010 na mpango wa pili ulianza Julai, 2010 na kuishia Juni, 2013. Mpango huu umekuwa chanzo kikuu cha kutoa ishara kwa wawekezaji na washirika wa maendeleo duniani juu ya ubora wa sera na mikakati, mipango na uwezo wa Serikali katika kusimamia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ukuzaji uchumi na upunguzaji umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mpango huu, nchi yetu imeendelea kupokea misaada na mikopo mbalimbali ikiwemo ya kibajeti, miradi ya maendeleo pamoja na mifuko ya kisekta. Aidha, *IMF* imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukabiliana na misukosuko ya urari wa malipo ya nje kwa kuziba nakisi ya mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio hayo, Serikali imeridhia kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mpango wa *PSI* ambapo utekelezaji wake utanza Julai, 2014 kwa kipindi cha miaka mitatu. Awamu hii itaendelea kujengea nchi yetu uwezo wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia sera kwa lengo la kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika awamu mbili zilizotangulia pamoja na kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa na uchumi tulivu na endelevu na hivyo kuvutia zaidi uwekezaji na kuongeza fursa za ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni; hatua ambazo zimefikwa hadi sasa ni kwa kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi wa kuishauri Serikali ambapo Mkataba ulishasainiwa, Serikali pia imekamilisha hatua ya kumpata Mshauri wa Sheria wa Kimataifa (*International Legal Adviser*). Aidha, Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kupata Kampuni za kufanya tathimini (*Rating Agencies*). Zoezi hili lilichelewa kutokana na kampuni za tathimini kutokubaliana na aina ya fomu za mikataba zinazoandaliwa na Serikali pamoja na kuleta nyongeza ya gharama nje ya makubaliano yaliosainiwa awali ambapo imeilazimu Serikali kuanza zoezi hilo upya.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa zoezi hilo siyo tu kutawezesha Serikali kupata mikopo nafuu ya kibiashara kuliko ilivyo sasa, bali kutawezesha makampuni na taasisi binafsi za Tanzania kupata mitaji kwa urahisi kutoka Soko la Mitaji la Kimataifa na kurahisisha uwekezaji wa sekta binafsi ambao ni mhimili wa uchumi. Aidha, zoezi hili ni muhimu katika kuiweka nchi kwenye ramani ya dunia hususan kiuchumi na kutambulika zaidi kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nielezee maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya kiuchumi katika mwaka 2014/2015 napendekeza kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi na tozo ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi na tozo nyingine zisizo za kodi chini ya Sheria mbalimbali na pia taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Marekebisho hayo yanahusu Sheria zifuatazo:-

- (i) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
- (ii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
- (iii) Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura ya 220;
- (iv) Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124;
- (v) Sheria ya Ushuru wa Mauzo ya Nje, Sura ya 196;
- (vi) Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38;
- (vii) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82;
- (viii) Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972;
- (ix) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;
- (x) Marekebisho ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, miko na idara zinazojitegemea;
- (xi) Usimamizi wa kodi zinazotozwa kwenye mafuta ya petroli yanapoingizwa nchini;
- (xii) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya sheria za kodi na sheria nyingine mbalimbali;
- (xiii) Kurekebisha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348;
- (xiv) Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura ya 418; na
- (xv) Sheria ya Wakala wa Serikali Sura ya 245 kwa minajili ya kuelekeza kwenye kuunganisha fedha zote za umma chini ya Mfuko Mkuu unaodhibitiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 kama ifuatavyo: -

Kwanza, kutoa msamaha wa kodi kwenye mapato yanayotokana na mauzo ya hatifungani zitakazotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*) katika Soko la Mitaji la Tanzania.

Mheshimiwa Soika, hatua hii itawezesha Benki hiyo kuongeza uwezo wa kutoa mikopo nafuu ya uwekezaji kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile kuendeleza miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pili, kutoza kodi ya zuio ya asilimia 15 kwenye ada wanayolipwa Wakurugenzi wa Bodi kila mwaka. Ada inayolipwa kwa Wakurugenzi wa Bodi yaani *Directors fees* kila mwaka sasa itatozwa kodi ya zuio asilimia 15.

Tatu, kufuta msamaha wa kodi ya makampuni kwenye mapato ya michezo ya kubahatisha.

Nne, kufuta msamaha wa kodi ya zuio kwenye ukodishaji wa ndege kwa walipa kodi wasio wakaazi yaani *non-resident*. Hatua hii inalenga katika kupunguza misamaha ya kodi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine, nikuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha ya kutoa misamaha ya kodi kwa miradi inayohusu upanuzi na ukarabati yaani *expansion and rehabilitation* inayofanywa na wawekezaji. Msamaha huo hivi sasa unatolewa kwa utaratibu ambapo wawekezaji hupewa vyeti vya Kituo cha Uwekezaji (*TIC*).

Wawekezaji wanapofanya *expansion* kwa miradi yao, wakifanya *rehabilitation* wamekuwa wakipatiwa misamaha ya kodi. Kwa hiyo, Sheria hii inakusudia kuondosha mamlaka kwa Waziri wa Fedha kutoa misamaha hiyo yako ambayo inahusu *expansion and rehabilitation*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nyingine ni kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira yaani *PAYE* kutoka asilimia 13 ya sasa hadi asilimia 12. Hatua hii inalenga katika kutoa nafuu wa kodi kwa wafanyakazi. Aidha, Serikali itaendelea kuangalia uwezekano wa kupunguza kiwango hiki hatua kwa hatua ili kuwapa nafuu wafanyakazi.

Pia kuongeza kiwango cha kutozwa kodi kwenye mapato ghafi ya wafanyabiashara wadogo yanayozidi shilingi 4,000,000/= kwa mwaka na yasiyozidi shilingi 7,500,000/= kwa mwaka kutoka asilimia mbili hadi asilimia nne kwa mauzo kwa wanaoweka kumbukumbu za mauzo na kuongeza kutoka shilingi 100,000/= hadi shilingi 200,000/= kwa ambao wasiokuwa na kumbukumbu za mauzo. Hatua hizi kwa pamoja zitaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 31,504 (bilioni thelathini na moja na mia tano na nne).

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine ambayo tunataka kuirekebisha ni Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147. Tunapendekeza yafuatayo:-

Kwanza, kufuta ushuru wa bidhaa wa asilimia 0.15 unaotozwa kwenye uhawilishaji wa fedha yaani *money transfer* ili kuwapa nafuu watu wanaotumia fedha kwa kutumia mabanki na kwa kutumia njia za simu. Badala yake tunapendekeza kuweka ushuru wa asilimia 10 kwa mabanki na mawakala kwenye mapato wanayopata kwenye tozo na ada wanazokusanya kwenye shughuli za uhawilishaji. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati wa Sheria hii tulipoitunga zile fedha ambazo zinatumiwa ndizo zilizokuwa zinachajwa ushuru wa asilimia 0.15; sasa tumerekebisha na badala yake badala ya kumtoa mtu ile fedha ambayo anatuma, kitakachotozwa ni ile *charge* ambayo analipa ambazo zinatozwa mabenki na watu wengine. Kwa hiyo, fedha unazotuma zitakuwa ni zilezile ambazo unamtumia mtu na kitakachochojwa ni ile *charge* tu ya utumaji fedha kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunataka kulifanyia marekebisho ni kuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha ya kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa ya mafuta ya petroli, isipokuwa tu misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na washirika wa maendeleo ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kupunguza matumizi mabaya ya msamaha huu na kuelekeza misamaha ya aina hii kwenye miradi ya maendeleo na yenye manufaa kwa umma. Aidha, hatua hii ina lengo la kuifanya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 iwe sambamba na Sheria ya TIC Sura ya 38 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2013 ambazo zilifanyiwa marekebisho ili kuondoa msamaha wa kodi kwenye mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunataka kulifanyia marekebisho ni kubadilisha ukomo wa umri wa magari yasiyo ya uzalishaji (*non-utility vehicles*) ambayo sasa hivi yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilimia 25 kutoka miaka 10 na zaidi tunarekebisha na sasa kuwa miaka minane na zaidi. Lengo la hatua hii ni kulinda mazingira na kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu ambayo yanasababisha ajali, vifo na kuongeza gharama kwa kutumia fedha za kigeni kuagiza vipuri mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna takwimu za ajali zilizotokana na magari hayo yenye umri mkubwa. Mwaka 2011 ajali zilizotokea ni 23,000...

SPIKA: Mmezoea mitumba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, ajali zilizotokea kwa mwaka 2011 pekee ni ajali 23,989 ambapo vifo vilivyotokana na ajali zilizosababisha na magari chakavu vilikuwa ni 3,981 na tuna majeruhi 20,802.

Mheshimiwa Spika, pekee mwaka 2012 kumtoa ajali 23,578, vifo vilivyosababishwa na ajali hizo ni 3,969 na majeruhi ni 20,111 na pekee mwaka 2013 kumetokea ajali 23,842.

SPIKA: Basi mnaongea kidogo, halafu mnanyamaza.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, vifo vilivyosababishwa kutokana na ajali hizo ambazo zimethibitishwa zinatokana na magari chakavu zilikuwa ni 4,002, ndicho ninachokizungumza ku-*back up my information*. Tutatoa hii taarifa.

Mheshimiwa Spika, pekee kuanzia Januari mpaka Mei, 2014 kumekuwa na ajali 7,248 ambavyo vimesababisha vifo 1,423 na majeruhi pekee ni 6,334.

Kwa hiyo, tunabadilisha ukomo wa umri wa magari yasiyo ya uzalishaji (*non-utility vehicles*) yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilima 25 hivi sasa kutoka miaka 10 na zaidi kwenda miaka minane na zaidi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kulinda mazingira na kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu ambayo yanasababisha, ajali na vifo na kuongeza gharama kwa kutumia fedha za kigeni kuagizia vipuri mara kwa mara.

Eneo lingine ni kubadilisha ukomo wa umri wa magari ya uzalishaji na yasiyobeba abiria yaani *non-passenger utility vehicles* yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilimia tano hivi sasa kutoka miaka 10 na zaidi kwenda miaka nane na zaidi.

Aidha, kubadilisha ukomo wa umri wa magari ya kubebea abiria (*passengers carrying vehicles*) yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilimia tano sasa kutoka miaka 10 na zaidi kwenda miaka mitano na zaidi. Lengo la hatua hii pia ni kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu yanayoharibu mazingira, yanayosababisha ajali pamoja na vifo na kuongeza mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza vipuri mara kwa mara. Hata hivyo hatua hii haitahusisha matrekta ambayo yote yataendelea kuingizwa nchini bila kutozwa ushuru wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zinazotambulika katika *HS Code 94.01*.

Aidha, mwaka 2013/2014 Serikali ilianza kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika katika *HS Code 94.03*. Lengo la hatua hizi ni kuhamasisha matumizi ya samani zinazotengenezwa kwa kutumia mbao zinazozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira na teknolojia katika kuzalisha bidhaa hii hapa nchini na hivyo kuongeza kipato cha wananchi na Serikali.

Pia kurekebisha viwango maalum (*specific rates*) vya ushuru wa bidhaa zisizokuwa za mafuta yaani *non-petroleum products* kwa asilimia 10. Bidhaa hizo ni pamoja na vinywaji baridi, mvinyo, pombe, vinywaji vikali na kaadhalika.

Aidha, bidhaa za sigara zitatozwa ushuru wa bidhaa wa asilimia 25 ili kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Udhibiti wa Matumizi ya Tumbaku yaani *Framework Convention on Tobacco Control* wa Shirika la Afya Duniani. Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizoridhia mkataba huu kwa kuwa unalingana na azma ya Serikali ya kulinda afya za wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ninayopendekeza ni kama ifuatavyo:-

(i) Ushuru wa vinywaji baridi, kutoka shilingi 91 kwa lita hadi shilingi 100 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi tisa kwa lita;

(ii) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini kutoka shilingi tisa hadi shilingi 10 kwa lita, ikiwa ni ongezeko la shilingi moja tu kwa lita;

(iii) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda yaliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini kutoka shilingi 110 kwa lita hadi shilingi 121 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 11 kwa lita;

(iv) Ushuru wa bidhaa iliyotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, mfano kibuku kutoka shilingi 341 kwa lita hadi shilingi 375 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 34 kwa lita;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(v) Ushuru wa bia nyingine zote kutoka shilingi 578 kwa lita hadi shilingi 635 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 57 kwa lita;

(vi) Ushuru wa mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 kutoka shilingi 160 kwa lita hadi shilingi 176 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 16 kwa lita;

(vii) Ushuru wa mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka shilingi 1,775 kwa lita hadi shilingi 1,953 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 178 kwa lita;

(viii) Ushuru wa vinywaji vikali kutoka shilingi 2,631 kwa lita hadi shilingi 2,894 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 263 kwa lita; na

(ix) Ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa viwandani hautaongezeka. (Makofi)

Marekebisho ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara ni kama ifuatavyo:-

(i) Sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka shilingi 9,031 hadi shilingi 11,289 kwa sigara 1000. Hii ni sawa na ongezeko la shilingi 2,258 kwa sigara 1000 au shilingi 2.25 kwa sigara moja.

(ii) Sigara zenye kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka shilingi 21,351 hadi shilingi 26,689 kwa sigara 1000, ikiwa ni ongezeko la shilingi 5,338 au shilingi 5.30 kwa sigara moja.

(iii) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na hizo nilizoelezea kutoka shilingi 38,628 hadi shilingi 48,285 kwa sigara 1000, ikiwa ni ongezeko la shilingi 9,657 sawa na shilingi 9.65 kwa sigara moja.

(iv) Tumbaku ambayo ipo tayari kutengeneza sigara kutoka shilingi 19,510 hadi shilingi 24,388 kwa kilo ikiwa ni ongezeko la shilingi 4,878 kwa kilo; na

(v) Ushuru wa *cigar* unabaki kuwa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi katika ushuru wa bidhaa kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza Mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 124,292,000/=.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine ambayo tunayoyafanya ni Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura ya 220 na tunapendekeza kuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa ushuru wa mafuta kupitia Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura ya 220 isipokuwa misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na washirika wa maendeleo ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile miundombinu ya barabara, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine ni Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari Sura ya 124 kwa nia ya kutofautisha mfumo wa usajili wa magari na ule wa pikipiki kwa kuweka namba zinazoanzia na TZ kwa pikipiki badala ya T. Lengo la hatua hii ni kudhibiti uhalifu unaofanyika kwa kubadilisha namba za magari na kuweka kwenye pikipiki. Hatua hii haikusudii kuongeza mapato ya Serikali.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mauzo Nje, Sura ya 196. Tunapendekeza kupunguza kiwango cha Ushuru wa Mauzo ya Nje yaani *Export Levy* unaotozwa kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi kutoka asilimia 90 au shilingi 900 kwa kilo moja hadi asilimia 60 au shilingi 600 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Lengo la hatua hii ni kuzuia biashara ya magendo ya ngozi ghafi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonyesha kuwa hivi sasa hakuna ngozi ghafi zinazosafirishwa nje kupitia vituo vya forodha na badala yake hupelekwa nje ya nchi kwa magendo. Aidha, lengo la kuongeza usindikaji wa ngozi hapa nchini ili kuongeza thamani na ajira bado halijafanikiwa. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 5,778,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38. Napendekeza kufanya mabadiliko yafuatayo kuhusu kodi na uwezekaji:-

Kwanza, kuondoa saruji katika orodha ya bidhaa zinazofikiriwa kuwa ni za mtaji yaani *deemed capital goods* ambazo hupata msamaha wa kodi hivi sasa kupitia TIC. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa saruji hapa nchini na kulinda viwanda vya saruji kutokana na ushindani wa saruji inayoagizwa nje. Kwa hiyo, saruji inayoingia sasa tumeondoa msamaha hasa zile ambazo msamaha huo unapata kutokana na misamaha inayotolewa na Kituo cha TIC.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, naomba hilo lisiingie *Hansard*.

Lakini eneo lingine ambalo tunatarajia kurekebisha ni kutoa tafsiri mpya ya wawekezaji mahiri yaani *strategic investors* kwa kufanya marekebisho ya kiwango cha chini cha mtaji kinachotumika katika kuwatambua wawekezaji mahiri. Tunapendekeza kiwango cha chini cha mtaji wa wawekezaji mahiri wanaotoka nje ya nchi kiongezeke kutoka dola za Kimarekani milioni 20 hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 50.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuelekeza vivutio vya misamaha ya kodi kwa wawekezaji ambao wanaleta mitaji mikubwa. Hata hivyo, napendekeza kiwango cha mtaji kinachomtambulisha mwekezaji wa Kitanzania kuwa mahiri kibakie pale pale yaani kitabakia kuwa cha dola za Kimarekani milioni 20 ili kuwanufaisha wawekezaji wazalendo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuendelea na uchambuzi wa kubaini namna bora zaidi ya kuvutia wawekezaji wakubwa kwenye miradi mikubwa na ya kimkakati ambayo itakuwa na msukumo mkubwa na wa haraka wa ukuaji wa uchumi, upanujaji ajira na uongezaji mapato ya wananchi. Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 43,703.4.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82. Katika marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Elimu na Mafunzo Stadi Sura ya 82 kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha 2013 yaliingizwa maudhui mapya katika sheria hiyo ambapo taasisi zinazonufaika na msamaha wa tozo ya ufundi stadi zilipunguzwa na kubaki Idara za Serikali au taasisi za umma tu na ambazo zinapata fedha kwa asilimia 100 kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu wa utekelezaji wa mabadiliko haya tumeona kuwa baadhi ya taasisi ziliachwa katika msamaha huu kimakosa. Kwa mfano, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Ofisi za Kibalozi hazitozwi kodi wala tozo kama hizi kwa mujibu wa makubaliano ya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kimataifa. Hivyo basi, napendekeza kufanya marekebisho ili kuongeza taasisi zifuatazo katika msamaha wa tozo hii:-

(i) Ofisi za Kidiplomasia;

(ii) Mashirika ya Umoja wa Mataifa na taasisi za nje zinazotoa misaada ambazo hazijihusishi na biashara kwa namna yoyote;

(iii) Taasisi za kidini kwa waajiriwa wake ambao ni mahsusi kwa kuendesha ibada tu;

(iv) Mashirika yanayotoa misaada ya hiari yasiyohusisha na biashara kwa namna yoyote ile;

(v) Serikali za Mitaa; na

(vi) Taasisi za elimu na mafunzo zinazotoa huduma bure na hazijihusishi na biashara katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tunataka kufanya marekebisho ni Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara wamewasilisha mapendekezo ya kutoza viwango mbalimbali vya ada za leseni za biashara kwa kutumia Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972. Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972 ili kuipa Serikali mamlaka ya kutoza ada za leseni za biashara kwa viwango vilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yamo katika Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Katika kikao cha maandalizi ya Bajeti cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *Pre-Budget Consultations of EAC Ministers for Finance* kilichofanyika tarehe 3 Mei, 2014 Jijini Nairobi, Kenya kilipendekeza marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa forodha yaani *EAC Common External Tariff (CET)* kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 kama ifuatavyo: -

(i) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mabasi ya kubeba abiria yanayotambuliwa katika *HS Code 8702.10.99* ambayo yana uwezo wa kubeba abiria 25 na zaidi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuboresha huduma ya usafirishaji wa abiria na kupunguza ajali;

Kwa hiyo, badala ya kutoza asilimia 25 ya mabasi yanayoletwa nchini sasa tutatoza asilimia 10. Lengo ni kuboresha huduma ya usafirishaji wa abiria na vilevile kupunguza ajali kunakotokana na kuingizwa kwa mabasi ambayo ni chakavu. Hii itawapa fursa wawekezaji vilevile kuingiza mabasi na kutoa huduma bora za usafiri nchini.

(ii) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano inayotambuliwa katika *HS Code 1001.99.10* na *HS Code 1001.99.90*. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda na wazalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumika ngano. Aidha, itaimarisha utulivu wa bei ya bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia ngano hiyo;

(iii) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri badala ya asilimia 10 kwenye malighafi inayotumika katika kutengeneza sabuni (*LABSA*) inayotambuliwa katika *HS Code 3402.11.00*; *HS Code 3402.12.00* na *HS Code 3402.19.00*, kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Hatua hii inalenga katika kuendelea kutoa unafuu kwa viwanda vidogo na vya kati vya kutengeneza sabuni, hivyo kuweza kuongeza uzalishaji na ajira;

(iv) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwenye kemikali za kuua wadudu zinazotengenezwa kwa kutumia petroli zinazotambuliwa katika HS Code 3808.91.39. Hatua hii inalenga katika kuwianisha kiwango cha ushuru unaotumika kwenye kemikali za kuulia wadudu zinazotengezwa kwa kutumia pareto ambazo nazo zinatozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 25. Aidha, hatua hii itahamasisha wazalishaji wa dawa za kuua wadudu kutumia pareto inayozalishwa hapa nchini na kuwezesha wakulima wa zao la pareto kuwa na soko la uhakika;

(v) Kupunguza Ushuru wa Forodha unaotozwa kwenye karatasi zinazotambuliwa katika HS Code 4805.11.00; HS Code 4805.12.00 na HS Code 4805.30.00 kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa za karatasi kwa kuwa karatasi hizo hazizalishwi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo karatasi zinazotambuliwa katika HS Code 4804.11.00; HS Code 4804.21.00; HS Code 4804.31.00 na HS Code 4804.41.00 zitaendelea kutozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 25. Karatasi za aina hii ni zile zinazozalishwa na kiwanda cha Mufindi pekee na lengo la kufanya hivyo ni kukilinda kiwanda hicho ambacho ndicho pekee kinachozalisha karatasi za aina hiyo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo, tunaweka ushuru wa asilimia 25 kwa karatasi kama hizo ambazo zinaingizwa nchini kukipa uwezo kiwanda chetu cha Mufindi kutengeneza karatasi na hivyo kwanza kuongeza kipato lakini vilevile kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC-Customs Management Act, 2004*) kama ifuatavyo: -

(i) Tanzania kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye mashine za kielektroniki za kukokotoa kodi (EFD) tutatoa msamaha wa ushuru kwa mashine za kielektroniki yaani EFD's kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii itapunguza gharama za kununua mashine hizi na hivyo kuhamasisha matumizi yake na kuboresha usimamizi wa kodi.

(ii) Kurekebisha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kufuta msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye vijiti vinavyotumika katika kutengeneza njiti za viberiti. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha matumizi ya vijiti vinavyotokana na malighafi zinazopatikana hapa nchini. Kwa hivyo, viwanda vyetu vya ndani sasa vitakuwa na uwezo wa kuzalisha njiti za kiberiti kwa malighafi zetu.

(iii) Kuendelea kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye migahawa ya majeshi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Katika kipindi hicho Serikali ya Tanzania imetakiwa kuangalia njia mbadala hususan za kibajeti katika kutoa unafuu wa gharama za maisha kwa majeshi ya ulinzi.

(iv) Kurekebisha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi za kutengeneza mitungi ya gesi. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uwekezaji kwenye utengenezaji wa mitungi ya gesi katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(v) Kurekebisha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye vifaa vya kuzalisha umeme unaotokana na nguvu za upepo na jua. Hatua hii inalenga katika kutoa unafuu wa gharama za uwekezaji katika kuzalisha na kuendeleza umeme unaotokana na nguvu ya upepo na jua na hivyo kuongeza upatikanaji wa nishati mbadala. Kwa hiyo, tutatoa msamaha wa ushuru wa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

forodha kwenye vifaa hivyo vya kuzalisha umeme unaotokana na nguvu za upepo pamoja na jua.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,456.1.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya ada na tozo mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea. Napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa kodi za mafuta ya petroli yanayoingizwa nchini, utaratibu wa utozaji wa kodi za mafuta ya petroli unaotumika hivi sasa ni wa kuchelewesha malipo ambapo kodi inakadiriwa na baada ya kukadiria malipo hufanyika katika siku 45. Tanzania ni nchi pekee inayotumia utaratibu huu katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, katika nchi hizo kodi zikishakadiriwa hukusanywa mara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kodi ambazo zinachangia mapato mengi kama vile kodi za mafuta ya petroli utaratibu huu unaathiri utekelezaji wa bajeti. Hivyo, ucheleweshaji wa malipo hayo hutoa mwanya wa ukwepaji kodi. Ili kuiwezesha Serikali kupata mapato yake kwa wakati na kuziba mianya ya ukwepaji kodi, napendekeza kodi inapokadiriwa, malipo yafanyike mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni marekebisho madogo madogo katika baadhi ya sheria za kodi na sheria nyingine mbalimbali. Napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo katika sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Mapendekezo haya yanaonekana katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya 2014.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe Mosi Julai, 2014, isipokuwa pale itakapokuwa imeelekezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, sura ya Bajeti kwa mwaka 2014/2015. Kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na shabaha ya bajeti, sura ya bajeti itakuwa kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali imepanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 19,853.3 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Mapato ya kodi na mapato yasiyo ya kodi yanatarajiwa kufikia shilingi trilioni 12,178.0 sawa na asilimia 19.2 ya Pato la Taifa. Aidha, mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 458.5 sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuendelea kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi trilioni 2,941.6. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 922 ni misaada na mikopo ya kibajeti, shilingi trilioni 1,745.3 ni mikopo na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 274.1 ni Mifuko ya Pamoja ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, ili kuziba nakisi ya bajeti, Serikali inatarajia kukopa kutoka katika vyanzo vya ndani na nje shilingi trilioni 4,275.2. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 2,265.7 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na mkopo wa ndani shilingi bilioni 689.6 ambao ni sawa na asilimia 1.1 ya Pato la Taifa na shilingi trilioni 1.320 ambazo ni mikopo yenye masharti ya kibiashara zitatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi, jumla ya shilingi trilioni 19,853.3 zimekadiriwa kutumika katika mwaka 2014/2015 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 13,408.2 ambayo yanajumuisha shilingi bilioni

Nakala ya Mtandao (Online Document)

5,317.6 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali, Wakala na Taasisi za Serikali, Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 4,354.7 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 3,735.9.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2014/2015 jumla ya shilingi bilioni 6,445.1 sawa na asilimia 33 ya bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Aidha, asilimia 69 ya fedha za maendeleo zitagharamiwa na fedha za ndani ambayo ni shilingi bilioni 4,425.7. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 689.6 zinatokana na mkopo kutoka vyanzo vya ndani, shilingi bilioni 1,320 ni mikopo ya masharti ya kibiashara, shilingi bilioni 375.5 ni mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 2,040.6 inatokana na mapato ya ndani. Kiasi cha shilingi bilioni 2,019.4 kitagharamiwa kwa fedha za nje, misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo ikijumuisha Mifuko ya Kisekta ambayo ni sawa na asilimia 31 ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo kimeendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2014/2015 fedha za ndani katika bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 4,425.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,952.9 zilizotengwa mwaka 2013/2014 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2014/2015 inazingatia pia mahitaji muhimu ya kitaifa ambayo hayawezi kuepukwa ikijumuisha gharama za uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Bunge Maalum la Katiba, upigaji kura ya maoni na uboreshaji wa daftari la wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama ulivyoielezwa hapo juu, mfumo wa bajeti kwa mwaka 2014/2015 unakuwa kama ifuatavyo, kuna jedwali ambalo ninaonekana.

(i) Mapato ya kodi ambayo yatakusanywa na TRA shilingi trilioni 11,318 (trilioni kumi na moja, milioni mia tatu kumi na nane);

(ii) Mapato yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 859,812 (bilioni mia nane hamsini na tisa, milioni mia nane kumi na mbili);

(iii) Mapato ya Halmashauri bilioni 458,471 (bilioni mia nne hamsini na nane, milioni mia nne sabini na moja);

(iv) Mikopo na misaada ya kibajeti shilingi milioni 922,168 (milioni laki tisa ishirini na mbili na mia moja sitini na nane);

(v) Mikopo na misaada ya miradi ya maendeleo shilingi trilioni 2,019,431 (trilioni mbili, bilioni kumi na tisa);

(vi) Mikopo ya ndani shilingi trilioni 2,955,227 (trilioni mbili milioni mia tisa hamsini na tano milioni mia mbili na ishirini na saba); na

(vii) Mikopo yenye masharti ya kibiashara ni shilingi trilioni 1,320,000 (trilioni moja milioni mia tatu ishirini elfu).

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo jumla ya mapato ni shilingi trilioni 19,853,331 (trilioni kumi na tisa, milioni mia nane hamsini na tatu, milioni mia tatu na thelathini na moja).

Mheshimiwa Spika, matumizi kwa Deni la Taifa. Matumizi ya Kawaida ikijumuisha Deni la Taifa ni shilingi trilioni 4,354,731 (trilioni nne milioni mia tatu hamsini na nne, milioni mia saba thelathini na moja); Mishahara shilingi trilioni 5,317,550 (trilioni tano, bilioni mia tatu kumi na saba,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

milioni mia tano hamsini); na Matumizi Mengineyo kwa upande wa Wizara ni shilingi trilioni 3,087,680 (trilioni tatu milioni themanini na saba, mia sita themanini); Mikoa ni bilioni 84,805 (bilioni themanini na nne, milioni mia nane na tano); na Halmashauri ni shilingi bilioni 563,452 (bilioni mia tano sitini na tatu, milioni mia nne hamsini na mbili).

Mheshimiwa Spika, hivyo, matumizi ya maendeleo jumla yake ni shilingi trilioni 6,445,115 (trilioni sita, milioni mia nne na arobaini na tano, milioni mia moja na kumi na tano) ambapo fedha za ndani ni shilingi trilioni 4,425,682 (trilioni nne, milioni mia nne na shirini na tano, mia sita na themanini na mbili) na fedha za nje ni shilingi trilioni 2,019,431 (trilioni mbili, milioni kumi na tisa, laki nne na thelathini na moja).

Mheshimiwa Spika, jumla ya matumizi yote ni shilingi trilioni 19,853,331 (trilioni kumi na tisa, bilioni mia nane na hamsini na tatu, milioni mia tatu thelathini na moja) sawa na mapato.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeeleza hapo awali, Bajeti ya mwaka 2014/2015 imelenga kuongeza makusanyo ya mapato, hasa ya ndani kwa kuanzisha vyanzo vipya, kuboresha vilivyopo na kupunguza misamaha ya kodi. Aidha, Bajeti hii imelenga kuongeza upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika, kuboresha elimu, kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miuondombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege. Hii itasaidia pia kutumia vyema fursa za kijiografia.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeeleza, Serikali imepanga kushughulikia kwa nguvu zaidi kero mbalimbali zinazowakabili wananchi zikiwemo kero ya upatikanaji wa maji, nishati ya uhakika, elimu juu ya umuhimu na faida za kulipa kodi kwa kutumia mitandao ya kielektroniki na kusimamia ulipaji kodi kwa hiari kupitia uhibitaji wa matumizi ya mfumo wa mashine za kielektroniki za kutoa risiti ulioboreshwa zaidi kuboresha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa kutumia TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa bajeti, Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti.

Kuhusu madai ya wakandarasi na wazabuni, Serikali inakamilisha utaratibu wa kusimamia na kuyalipa madai yaliyohakikiwa kupitia Hazina kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zinazohusika. Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza Wizara na Taasisi kuzingatia mfumo wa malipo (*IFMs*) ambao unamtaka kila Afisa Masuuli kutoingia mikataba bila kuwa na *LPO* inayotokana na mfumo wa malipo wa *IFMs*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo ya nje, Serikali itaendelea kufanya majadiliano mapema na wahisani pamoja na mabenzi ili kuhakikisha kwamba fedha za misaada na mikopo zinapatikana kama ilivyopangwa na kwa wakati. Hata hivyo, upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo kwa wakati inategemea umakini na usahihi wa kutekeleza miradi iliyokusudiwa kulingana na malengo na makubaliano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa Bajeti hii kunahitaji nidhamu ya hali ya juu ya wadau wote, ikiwemo Serikali na Taasisi zake, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla. Ili kufikia azma hii juhudi za pamoja kati ya Serikali na wadau wote zinahitajika ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi kwa kuwekeza zaidi katika maeneo ya kipaumbele. Natoa rai kwa kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake ili Bajeti hii iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, inawezekana, tutimize wajibu wetu!

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. Ahsante. (Makofi)

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja itolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante, Bajeti hii imeungwa mkono na wahusika.

HOTUBA YA BAJETI WA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2014/2015 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2014/2015. Pamoja na hotuba hii, nimewasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti. Kitabu cha **Kwanza** ni makisio ya mapato; Kitabu cha **Pili** ni makisio ya matumizi ya kawaida kwa wizara, idara za Serikali zinazojitegemea, wakala na taasisi za Serikali; Kitabu cha **Tatu** ni makisio ya matumizi ya kawaida kwa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na Kitabu cha **Nne** ni makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa wizara, idara za Serikali zinazojitegemea, wakala na taasisi za Serikali, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2014 ambao ni sehemu ya bajeti hii.

2. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema wakati nikiwasilisha mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Fedha, Wizara ilipata pigo kwa kuondokewa na aliyekuwa Waziri wa Fedha marehemu Dkt. William Augustao Mgimwa. Marehemu Dkt. Mgimwa alikuwa ni mtaalamu wa masuala ya fedha, hivyo kwa kipindi kifupi alichokaa Wizarani aliweza kutumia taaluma yake ipasavyo kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kusisitiza ukusanyaji wa mapato ya ndani na nidhamu ya matumizi kwa lengo la kupunguza utegemezi. Aidha, marehemu Dkt. Mgimwa alizingatia sheria, taratibu na kanuni katika kutekeleza majukumu yake ambayo ndio msingi mkuu aliotuachia ambao tunautumia na tutaendelea kuutumia. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amina.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na taadhima napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani kubwa aliyokuwa nayo kwangu kwa kuiteua kuwa Waziri wa Fedha. Naahidi kuwa nitatekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa umakini, weledi na uaminifu mkubwa. Aidha, napenda kuwashukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa miongozo yao ya kila wakati katika kufanikisha majukumu ya uandaaji wa bajeti.

Vilevile, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Adam Kighoma Malima (Mb) na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri wa Fedha. Kadhalika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano wake mkubwa aliotupa wakati wa matayarisho ya bajeti hii. Kadhalika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa vikao vya Bunge kwa kuongoza majadiliano vizuri bungeni.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukurani kwa wizara, idara za Serikali zinazojitegemea, wakala na taasisi za Serikali, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa na wadau mbalimbali kwa kushiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya bajeti hii. Kwa namna ya

pekee, ninaishukuru Kamati ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge (Mb) kwa kuchambua kwa kina bajeti za mafungu yote na kutoa mapendekezo na ushauri. Aidha, napenda kuwashukuru wenyeviti wa kamati za kisekta kwa ushauri na mapendekezo waliyotoa wakati wakichambua rasimu ya Bajeti hii.

5. **Mheshimiwa Spika**, ninawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha SMT; Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha SMZ; Naibu Makatibu Wakuu; Gavana wa Benki Kuu; Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Viongozi Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara; wakuu wa idara, vitengo na watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa waliyoifanya katika maandalizi ya Bajeti hii. Ninamshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2014 na nyaraka mbalimbali za kisheria ambazo ni sehemu ya Bajeti hii. Aidha, ninamshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha nyaraka zote za Bajeti kwa usahihi na kwa wakati.

6. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya mwaka 2014/15, imezingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano; na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Madhumuni ya mipango na mikakati hii ni kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

7. **Mheshimiwa Spika**, Awamu ya pili ya MKUKUTA inafikia tamati Juni 2015, hivyo Bajeti hii ni ya mwisho katika utekelezaji wa MKUKUTA II. Aidha, Malengo ya Maendeleo ya Milenia ambayo yametumika kama sehemu ya mikakati yetu ya kupunguza umaskini yanafikia tamati mwaka 2015. Hata hivyo, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 utafikia tamati Juni 2016. Hii inamaanisha kwamba MKUKUTA II utafikia ukomo mwaka mmoja kabla ya ukomo wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo. Kazi iliyo mbele yetu ni kutafuta jinsi masuala ya kupunguza umaskini yatakavyoanishwa katika mikakati na mipango yetu baada ya Juni 2015 wakati tunaielekea kuhitimisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2016. Hivyo basi, Serikali inafanya mapitio ya MKUKUTA II na kuandaa mapendekezo ya namna ya kuoanisha masuala muhimu ya kupambana na umaskini katika mipango yetu baada ya Juni 2015. Lengo ni kuwa na Mwongozo mmoja wa kuelekeza shughuli za maendeleo kwa Taifa letu.

8. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti hii imelenga kupunguza gharama za maisha ya wananchi kwa kuendelea na jitihada za kudhibiti na kupunguza mfumuko wa bei, kuendelea kuboresha huduma za jamii, kuboresha miundombinu ya barabara, umeme na umwagiliaji, kuongeza mishahara ya watumishi wa umma, kuendelea kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi, kuongeza fursa za ajira na kuimarisha utawala bora. Aidha, bajeti hii imezingatia pia maandalizi ya Katiba mpya; uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2014; na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

9. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti hii vilevile imelenga kupunguza misamaha ya kodi. Serikali imewasilisha kwenye Bunge hili Muswada wa Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Lengo la Muswada huu ni **kupunguza misamaha** ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kubakiza misamaha yenye tija kwa uchumi na ustawi wa jamii na kuleta usawa na haki katika ulipaji kodi. Aidha, Serikali imewasilisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi hapa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Katika Muswada wa Sheria ya Fedha 2014 nimependekeza pia mabadiliko kadhaa ya Sheria za Kodi, kama nitakavyoeleza baadae, kwa lengo la kupunguza misamaha ya kodi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge sote kwa pamoja tuunge mkono jitihada hizi za Serikali ambazo zitasaidia kupunguza misamaha ya kodi na kurahisisha usimamizi wa kodi nchini na hivyo kutoa unafuu kwa walipa kodi, na kuongeza mapato ya Serikali.

10. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na kupunguza misamaha ya kodi na kuongeza haki na usawa katika kutoa misamaha hii, kuanzia mwaka 2014/15, Serikali itachukuwa hatua kuu mbili muhimu. Kwanza, Serikali itakuwa inatoa taarifa ya misamaha ya kodi kila robo mwaka kwa kuwatangaza walionufaika na misamaha kwenye Tovuti ya Wizara ya Fedha. Taarifa hii itajumuisha majina ya watu, taasisi, asasi na makampuni yaliyonufaika na misamaha ya kodi, thamani na sheria iliyotumika kutoa misamaha hiyo. Zoezi hili litahusisha taarifa ya misamaha ya kodi kuanzia mwaka 2010 na kuendelea. Hatua hii itasaidia kuleta uwazi na uwajibikaji katika suala la misamaha ya kodi na kuwafanya wananchi wajue ni nani anayenufaika na misamaha hiyo. Pili, ni kutoa taarifa ya kina ya misamaha yote ya kodi iliyotolewa na kuiwasilisha Bungeni kila mwaka ili Waheshimiwa Wabunge mpate nafasi ya kujadili na kutoa maoni yenu.

11. **Mheshimiwa Spika**, bajeti hii imelenga pia kuimarisha zaidi usimamizi na udhhibiti wa matumizi ya fedha za umma. Ili kutekeleza azma hii, Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti na utakamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2014/15. Sheria hii inalenga kuongeza nidhamu ya matumizi na uwajibikaji kwa wadau wote wanaotekeleza Bajeti ya Serikali wakiwemo: viongozi na maafisa wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge, mashirika ya umma, wakala na taasisi za Serikali, wakandarasi na wazabuni. Katika kuandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti, wadau muhimu, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, watashirikishwa kupitia kamati za kudumu za Bunge.

12. **Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na tatizo la utekelezaji wa miradi chini ya viwango. Katika kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inawiana na uwekezaji katika miradi husika, Serikali imenunua vifaa vya kuhakiki ubora wa miradi ya maendeleo. Vifaa hivi vitatumika katika uhakiki wa miradi inayotekelezwa na wizara, idara, wakala na taasisi za Serikali na mamlaka za serikali za mitaa. Uhakiki huu utasaidia kuhakikisha kuwa, miradi ya maendeleo inayotekelezwa inakuwa ya ubora unaokidhi viwango.

Aidha, matumizi ya vifaa hivi yatasaidia kuwabaini wakandarasi dhaifu katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

13. **Mheshimiwa Spika**, ili kudhibiti matumizi na kupata thamani ya fedha katika ununuzi wa bidhaa na huduma, Serikali imeamua kuzingatia ununuzi wa pamoja (bulk procurement) kutoka kwa wazalishaji badala ya wakala kama ilivyo sasa na hatua imeanza kuchukuliwa ili ununuzi wa magari na vyombo vya TEHAMA ufuatae utaratibu huo.

Aidha, Kutokana na wingi wa mafuta yanayotumika kwenye magari na mitambo, Serikali itaanzisha mfumo mpya wa kielektroniki utakaotumika katika kununua, kutunza na kuuza bidhaa hiyo ili kuwezesha Serikali kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika katika ununuzi wa mafuta.

Vilevile, inaelekezwa kwamba vitabu vya kumbukumbu (diaries) na kalenda za kila mwaka, zitachapishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tu. Hii ni kwa wizara, idara zinazojitegemea, wakala na taasisi za Serikali, mikoa na mamlaka za Serikali za Mtaa badala ya utaratibu wa sasa ambapo kila taasisi ya Serikali inachapisha kwa utaratibu wake. Pia, ili kupunguza matumizi ya umeme katika ofisi za Serikali, Serikali inakusudia kutumia vifaa vya umeme vyenye matumizi kidogo ya umeme (Energy saving technology sensors).

14. **Mheshimiwa Spika**, hatua nyingine ya kudhibiti matumizi ya umma ni kuunganisha matumizi yote ya wizara, idara za Serikali zinazojitegemea, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na wakala na taasisi za Serikali chini ya mfumo mmoja wa udhhibiti wa fedha za Serikali unaosimamiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kuanzia sasa, hakuna taasisi yoyote ya umma

inayokusanya maduhuli itakayoruhusiwa kutumia fedha walizokusanya kabla ya bajeti yao kupitiwa na kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali na fedha zote zinazozidi bajeti iliyoidhinishwa zitawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Utaratibu huu unatumika na nchi nyingine duniani zikiwemo nchi jirani, na kwa hapa Tanzania utaratibu huu unatumika kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hivyo, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2014 una mapendekezo ya kurekebisha sheria zinazohusika ili kuwezesha utekelezaji wa utaratibu huo na ninaomba Waheshimiwa Wabunge muupitishie kwa kauli moja.

15. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kutoa taarifa kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwaka 2014/2015.

II. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA SERA ZA BAJETI YA MWAKA 2013/14

16. **Mheshimiwa Spika**, mipango na Bajeti ya Serikali mwaka 2013/14 iliandaliwa kwa kuzingatia mzunguko mpya wa bajeti na sera za uchumi jumla ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 18,249 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje na kiasi cha shilingi bilioni 12,604 kilipangwa kutumika kwenye matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 5,645 kwenye matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2014, Serikali imekusanya mapato halisi yenye jumla ya shilingi bilioni 12,882 sawa na asilimia 70 ya mapato yote ya mwaka.

Sera za Mapato

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, sera za mapato zililenga kupanua wigo wa kodi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ili kugharamia Bajeti ya Serikali. Sera hizo zilijumuisha: marekebisho ya sheria zinazoruhusu misamaha ya kodi kwa lengo la kuipunguza; kuanzisha kituo kimoja cha kutoa huduma za forodha katika bandari ya Dar es Salaam, kuendelea kuanzisha vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mipakani (*One Stop Border Posts*); na kupitia mfumo wa ukusanyaji wa kodi ya majengo na ardhi.

Mwenendo wa Mapato ya Ndani

18. **Mheshimiwa Spika**, sera za mapato zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 11,154. Tathmini inaonesha kuwa hadi Aprili 2014, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 7,771.5, sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 10,395.4. Sababu ya kutokufikia lengo ni kutokufanya vizuri kwa baadhi ya vyanzo vya kodi ambavyo vilitarajiwa kuchangia kiasi kikubwa cha mapato. Kutokana na mwenendo huu wa mapato, inategemewa kuwa hadi tarehe 30 Juni 2014, makusanyo ya mapato yanayotokana na kodi yatafikia asilimia 93 ya lengo la mwaka.

19. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mapato yasiyotokana na kodi, hadi Aprili 2014, yalifikia shilingi bilioni 425.5 ikiwa ni asilimia 57 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 741.1 kwa mwaka. Inakadiriwa kuwa, hadi Juni 2014, mapato yasiyo ya kodi yatafikia asilimia 65 ya lengo la mwaka.

20. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mapato ya halmashauri shilingi bilioni 252.8 zilikusanywa, sawa na asilimia 66 ya makadirio kwa mwaka ya shilingi bilioni 383.5. Sababu ya kutofikiwa kwa malengo hayo ni pamoja na kuchelewa kuanza ukusanyaji wa ada ya leseni za biashara na kuchelewa kwa zoezi la kuthamanisha majengo kwa mkupuo (mass valuation).

Misaada na Mikopo ya Nje yenye Masharti Nafuu

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Serikali ilitarajia kupata shilingi bilioni 3,855.2 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2014, misaada na mikopo ya kibajeti iliyopokelewa ni shilingi bilioni 734 sawa na asilimia 63 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Mifuko ya Kisekta, shilingi bilioni 368.6 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka. Aidha, kwa upande wa mikopo na misaada ya miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 1,200 zilipokelewa sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka.

Mikopo ya Kibiashara ya Ndani

22. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 1,699.9 kutoka soko la ndani kwa utaratibu wa kuuza hatifungani na dhamana za Serikali za muda mfupi kwa ajili ya kugharamia bajeti yake. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 552.3 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 1,147.6 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva. Katika kipindi cha Julai 2013 – Aprili, 2014, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 1,803.9. Kati ya hizo, shilingi bilioni 1,113.3 zilitumika kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zilizoiva (rollover) na shilingi bilioni 690.6 zilitumika kugharamia miradi ya maendeleo.

Mikopo ya Kibiashara kutoka Nje

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 1,156.4 sawa na Dola za Marekani milioni 700 kutoka kwenye masoko ya fedha ya nje ili kugharamia miradi ya maendeleo. Hadi sasa Serikali imepata jumla ya Dola za Marekani milioni 407.9 sawa na asilimia 58 ya makadirio. Dola za Marekani milioni 176.9 zimepatikana kutoka Benki ya Credit Suisse kwa ajili ya kugharamia miradi ya barabara, maji na reli na Dola za Marekani milioni 83 zimepatikana kutoka Benki ya Citi kwa ajili ya kugharamia miradi ya ufuaji umeme inayosimamiwa na TANESCO.

Aidha, Serikali itapata Dola za Marekani milioni 148 kutoka Benki ya HSBC kwa utaratibu wa *Export Credit Arrangement* kugharamia upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Majadiliano ya kupata kiasi kilichobaki cha Dola za Marekani milioni 292 kwa utaratibu huo huo yanaendelea na yako katika hatua za mwisho yakihusisha benki za Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC) na Japan Bank for International Cooperation (JBIC), kwa ajili ya mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi II wa Megawati 240.

Sera za Matumizi

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kutekeleza sera za matumizi zifuatazo: kuwianisha matumizi na mapato yaliyotarajiwa; kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 5 ya Pato la Taifa; mafungu kuzingatia viwango vya matumizi vilivyoidhinishwa na Bunge; kutenga fedha za kutosha katika kutekeleza miradi ya vipaumbele; na kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011.

Mwenendo wa Matumizi

25. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, Serikali imetoa ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 13,034.7 sawa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka. Serikali iliendelea kulipia mishahara ya watumishi wa umma, ambapo hadi Aprili 2014, shilingi bilioni 3,760 zililipwa sawa na asilimia 79 ya bajeti ya mishahara ya mwaka ya shilingi bilioni 4,763. Shilingi bilioni 1,098 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu, jumla ya shilingi bilioni 92 zilitolewa kwa ajili ya watumishi wa sekretarieti za mikoa na shilingi bilioni 2,097 kwa ajili ya halmashauri 161 za majiji, manispaa, miji na wilaya. Vilevile, Serikali ililipa mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma jumla ya shilingi bilioni 473.

26. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ilipanga kutumia shilingi bilioni 3,319.2 kulipa Deni la Taifa na madeni mengine. Hadi kufikia Aprili 2014, malipo ya riba kwa mikopo ya ndani na nje yalikuwa shilingi bilioni 782.7, sawa na asilimia 78 ya makadirio ya shilingi bilioni 998 kwa mwaka. Malipo ya deni halisi la mikopo ya nje yalikuwa shilingi bilioni 139, sawa na asilimia 36 ya makadirio ya mwaka. Malipo kwa madeni mengine (CFS others) yalikuwa shilingi bilioni 750 ikiwa ni asilimia 96 ya bajeti ya mwaka ya shilingi bilioni 783.

Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 1,113.3 kilipia hatifungani na dhamana za Serikali zilizoiva (rollover) sawa na asilimia 97 ya bajeti ya mwaka ya shilingi bilioni 1,148. Matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 3,374.7 ikiwa ni asilimia 69 ya makadirio ya shilingi bilioni 4,912 kwa mwaka.

27. **Mheshimiwa Spika**, hadi Aprili 2014, jumla ya shilingi bilioni 3,115 ziliidhinishwa na kutolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 5,645. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha zilizoidhinishwa na kutolewa, fedha za ndani zilikuwa shilingi bilioni 1,546 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka ya shilingi bilioni 2,953, sawa na asilimia 52. Aidha, fedha za nje zilikuwa shilingi bilioni 1,569 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi bilioni 2,692 sawa na asilimia 58 ya makadirio ya mwaka.

Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma

28. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wenye lengo la kuhakikisha kwamba Hesabu za Majumuisho za Serikali (Consolidated Financial Statements) zinaandaliwa kwa kuzingatia mfumo wa Viwango vya Kimataifa Vya Uhasibu (IPSAS Accrual Basis), hatua hizo zinalenga kuunganisha hesabu za Serikali Kuu, mamlaka za serikali za mitaa, mifuko ya hifadhi ya jamii, taasisi mbalimbali na mashirika ya umma.

29. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma hii ya Serikali ya kuandaa hesabu za majumuisho, Hesabu za mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 kwa Serikali kuu zimeandaliwa kwa kuzingatia mfumo wa *IPSAS Accrual Basis* kwa mara ya kwanza na kuziwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria. Lengo la kutumia mfumo huu ni kuboresha uwazi na uwajibikaji wa Serikali katika matumizi na usimamizi wa rasilimali zake. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kwa kupanua mtandao wa malipo ya moja kwa moja kwenye benki – TISS katika mikoa 20 ya Tanzania Bara hadi kufikia Mei, 2014 na zoezi linaendelea kwenye mikoa iliyosalia ambapo hadi mwishoni mwa Juni 2014 mikoa yote itakuwa imeunganishwa kwenye Mfumo huu.

30. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza nidhamu na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma, Serikali imeanza kufanya ukaguzi wa ndani kwa kuzingatia mwongozo wa ukaguzi wa ndani wenye viwango vya kimataifa ambao ulianza kutumika Julai 2013. Serikali pia imeandaa Mwongozo wa Kamati za Ukaguzi katika Sekta ya Umma kwa lengo la kuboresha utendaji wa Kamati za Ukaguzi na hivyo kuongeza uwazi na uwajibikaji katika mapato na matumizi ya Serikali. Aidha, Serikali imeendelea kuhakiki madai ya wakandarasi, wazabuni na watumishi, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 58 kimeokolewa katika zoezi hilo.

Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II)

31. **Mheshimiwa Spika**, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini umeainisha mikakati katika nguzo kuu tatu, ambazo ni Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato, Kuboresha Maisha na Ustawi wa Jamii na Kuimarisha Utawala Bora na Uwajibikaji. Mwaka 2013/14 ulikuwa mwaka wa tatu wa utekelezaji wa MKUKUTA II. Mwenendo wa viashiria vya

Nakala ya Mtandao (Online Document)

kupima matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA II katika nguzo kuu tatu nilizozitaja unaonesha mafanikio na changamoto. Nitaeleza matokeo kwa baadhi ya viashiria.

32. **Mheshimiwa Spika**, katika nguzo ya kwanza ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato, uchumi umeendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha. Ukuaji huu umeongeza pato halisi la wastani la kila Mtanzania hadi kufikia shilingi 1,186,200 mwaka 2013 kutoka shilingi 1,025,038 mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 14. Aidha, umaskini wa kipato umeendelea kupungua ambapo kwa mujibu wa takwimu mpya za Utafiti wa Mapato na Matumizi katika Kaya Binafsi uliofanyika Mwaka 2012, umeonesha kuwa umaskini wa kipato umepungua kwa wastani wa asilimia 6.2 kati ya mwaka 2007 na 2012 kutoka asilimia 34.4 hadi asilimia 28.2. Vilevile, umaskini wa chakula umepungua kwa asilimia 2.1 kati ya mwaka 2007 na 2012 kutoka asilimia 11.8 hadi asilimia 9.7.

33. **Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa utekelezaji katika eneo la kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii, unaridhisha. Aidha, uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi elimu ya msingi umeimarishwa kutoka 1:47 mwaka 2012 na kufikia 1:43 mwaka 2013 ikilinganishwa na lengo la uwiano wa 1:40.

Katika elimu ya sekondari uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi ulifikia lengo la MKUKUTA II la 1:28 mwaka 2013. Jitihada za kuboresha huduma za afya, lishe na upatikanaji wa maji safi na salama zimeendelea kuimarisha ubora wa maisha na ustawi wa jamii. Kwa mujibu wa takwimu mpya za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, vifo vya watoto wachanga vimeendelea kupungua kutoka vifo 51 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2010 hadi vifo 45 mwaka 2012. Umri wa kuishi kwa Mtanzania umeongezeka kutoka wastani wa miaka 51 mwaka 2002 hadi miaka 61 mwaka 2012.

34. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utawala bora na uwajibikaji, Serikali imeendelea kutekeleza programu za maboresho. Kupitia programu hizi, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuboresha mfumo wa usimamizi wa mali na fedha za umma, mfumo wa sheria na usimamizi wa haki, demokrasia, na utoaji huduma za umma kwa jamii. Hatua hizi zimeboresha upatikanaji wa huduma kwa umma, kupanua demokrasia na kuongeza kasi ya utoaji maamuzi ya mashauri katika mahakama za mwanzo na wilaya.

Tathmini ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs)

35. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Malengo ya Maendeleo ya Milenia, nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa ikiwemo Tanzania ziliahidhi kutekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia na shabaha ziliwekwa kwa viashiria mbalimbali kwamba ifikapo mwaka 2015, malengo hayo yawe yamefikwa. Mapitio ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia yanaonesha kuwa, Tanzania imefanya vizuri na inaweza kufikia malengo yafuatayo: Elimu ya Msingi kwa Wote; Usawa wa Kijinsia na Fursa Sawa kwa Wanawake; Kupunguza vifo vya kina mama na watoto wachanga na kupunguza maambukizi ya UKIMWI. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea na jitihada za kuhakikisha malengo yaliyobakia yanafikiwa.

Sekta ya Fedha

36. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza programu ya maboresho ya sekta ya fedha ili kuhakikisha inachangia kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na hivyo kukuza Pato la Taifa. Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma Jumuishi za Kifedha (National Financial Inclusion Framework) ulizinduliwa na Serikali Desemba, 2013 kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanafikiwa na huduma za kifedha zilizo rasmi. Aidha, Serikali ilikamilisha mwongozo wa uwakala wa huduma za kibenki ambao umeiwezesha Benki Kuu ya Tanzania kutoa leseni za

uwakala kwa benki za CRDB, Posta, Equity na DCB. Utaratibu huu wa uwakala umepanua wigo wa huduma za kibenki na hivyo kuwafikia walengwa wengi zaidi na kwa gharama nafuu.

37. **Mheshimiwa Spika**, katika kuangalia vikwazo vya upatikanaji wa huduma za fedha nchini, Serikali ilifanya utafiti mwaka 2013. Matokeo ya utafiti huo yalionesha mafanikio yafuatayo: asilimia 13.9 ya wananchi wanatumia huduma za kibenki ikilinganishwa na asilimia 9.2 mwaka 2009. Aidha, asilimia 43.5 ya wananchi wanatumia huduma zisizo za kibenki (Bima, SACCOS na taasisi ndogo za huduma za kifedha, malipo kwa njia ya simu) ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2009. Asilimia 15.8 ya wananchi wanatumia huduma za kifedha za sekta isiyo rasmi mfano VICOBA, ROSCA (Rotating Saving and Credit Association), VSLA (Village Saving and Lending Association) ikiwa imepungua ikilinganishwa na asilimia 28.9 mwaka 2009. Kwa ujumla utafiti huu unaonesha kuwa asilimia 57.4 ya wananchi wanapata huduma rasmi za kifedha.

Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

38. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua kuwa sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi. Ili kutimiza azma hiyo, Serikali imewasilisha Bungeni muswada wa kurekebisha Sheria ya Ubia Na. 18 ya mwaka 2010 ili kuwezesha utekelezaji wa haraka wa miradi ya PPP. Aidha, Serikali inaazimia kuanzisha Mfuko maalumu wa miradi ya ubia (PPP Facilitation Fund) na kuunda Kamati ya Kitaifa ya PPP (PPP Technical Committee) pamoja na Kituo cha Miradi ya Ubia (PPP Centre).

Deni la Taifa

39. **Mheshimiwa Spika**, Deni la Taifa linasimamiwa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 kama ilivyorekebisha mwaka 2004 na Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Madeni.

Hadi kufikia Machi 2014, Deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na deni la nje la sekta binafsi lilifikia shilingi bilioni 30,563 ikilinganishwa na shilingi bilioni 23,673.5 la Machi 2013. Kati ya kiasi hicho, deni la Serikali ni shilingi bilioni 26,832.4 na deni la sekta binafsi la nje ni shilingi bilioni 3,730.6. Deni la Serikali la nje linajumuisha mikopo ya nje kutoka mashirika ya fedha ya kimataifa, nchi wahisani na mabanki ya kibashara ambapo hadi kufikia Machi 2014 lilikuwa shilingi bilioni 18,997.6 wakati deni la ndani ni shilingi bilioni 7,834.8. Ongezeko la Deni la Taifa linatokana na kupatikana kwa mikopo mipya, kupokelewa kwa fedha za mikopo ya nyuma kwa kipindi husika pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi.

Uhimilivu wa Deni la Taifa

40. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha Deni la Taifa linaendelea kuhimilika Serikali imekuwa ikikopa na kuwekeza katika miradi ya kuchochea ukuaji wa uchumi ili kuwa na uwezo wa kuyalipa madeni hayo pindi yanapoiva. Aidha, Serikali imejiwekea utaratibu wa kufanya tathmini ya uhimilivu wa deni kila mwaka kwa mujibu wa sheria ili kubainisha hali halisi ya deni na uwezo wa nchi kulipa madeni hayo katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Kufuatia utaratibu huo mwezi Septemba, 2013 Serikali ilifanya tathmini ya uhimilivu wa deni kwa kutumia viashiria vilivyokubalika kimataifa. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa Deni la Taifa ilibainisha kuwa Deni la Taifa ni himilivu.

41. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa tathmini hiyo, viashiria vyote vya kupima uhimilivu wa deni viko katika wigo unaokubalika kimataifa (debt sustainability thresholds). Baadhi ya viashiria hivyo ni uwiano wa thamani ya sasa ya Deni la Taifa la nje (Present Value of External Debt) kwa uwiano wa Pato la Taifa ni asilimia 24.8 ikilinganishwa na ukomo wa wa asilimia 50. Uwiano wa thamani ya sasa ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 121.2 ikilinganishwa na ukomo

wa asilimia 300, Uwiano wa thamani ya ulipaji wa deni la nje kwa thamani ya mapato ya mauzo nje ya nchi ni asilimia 3.34 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 25, Uwiano kati ya ulipaji wa deni kwa mapato ya ndani ni asilimia 4.32 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 22 na uwiano wa deni la Serikali likijumuisha dhamana za serikali kwa taasisi mbalimbali kwa Pato la Taifa ni asilimia 35.58 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 74.

42. **Mheshimiwa Spika**, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa deni la Taifa linaendelea kuwa himilivu kwa kuendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukopa mikopo yenye masharti nafuu na kuhakikisha kuwa fedha zitokanazo na mikopo hiyo zinaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Serikali pia inaweka ukomo wa mikopo yenye masharti ya kibiashara bila kuathiri uhimilivu wa deni.

Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza uamuzi wake wa kusitisha utoaji wa dhamana kwa taasisi, mashirika, idara na wakala wa Serikali zinazopata ruzuku kutoka Serikalini.

Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa

43. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, Serikali ilianzisha utaratibu madhubuti wa kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi iliyo katika mpango wa maendeleo ujulikanao kama Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now - BRN*). Lengo la kuanzisha utaratibu huu ni kuongeza kasi katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambapo Tanzania inatarajia kuwa nchi ya kipato cha kati. Ili kuleta tija na ufanisi utekelezaji wa BRN unahusisha maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni:-Kilimo, Elimu, Maji, Nishati, Miundombinu na Utafutaji wa Rasilimali Fedha.

44. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza maamuzi yaliyofanyika kwenye maabara ya utafutaji wa rasilimali fedha, Wizara ya Fedha ilipewa lengo la kuongeza mapato mapya kwa jumla ya shilingi bilioni 1,160 kwa mwaka 2013/14; kupunguza nakisi ya bajeti kutoka asilimia 6.8 hadi asilimia 5.5 ya Pato la Taifa; kudhibiti matumizi; na kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi ya BRN katika sekta nyingine. Katika mwaka 2013/14, jumla ya shilingi bilioni 1,700 zilitengwa kwenye bajeti kupitia miradi mbalimbali ya sekta zinazotekeleza miradi ya BRN.

45. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2014, mafungu yanayotekeleza miradi ya BRN yamepatiwa jumla ya shilingi bilioni 1,566.7 sawa na asilimia 92 ya bajeti ya miradi ya BRN kwa mwaka 2013/14. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya maji viijini shilingi bilioni 226.1; Elimu shilingi bilioni 48.4; Nishati shilingi bilioni 577.5; Uchukuzi ikijumuisha miundombinu ya barabara na reli shilingi bilioni 663.6; na Kilimo shilingi bilioni 51.1.

Mafanikio na Changamoto katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2013/14

46. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miezi kumi ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/14, Serikali imefanikiwa kutekeleza shughuli muhimu za bajeti licha ya kukabiliwa na changamoto kama ilivyoielezwa katika hotuba za mipango na bajeti za wizara, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa husika ambazo Bunge lako tukufu limejadili kwa kina na kuzipitisha.

Aidha, Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu imeelezea mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa kuzingatia hatua hiyo, nitaeleza kwa kifupi baadhi ya mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

Mafanikio

Ukuaji wa Uchumi

47. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013 Pato halisi la Taifa limekua kwa asilimia 7.0 ambayo ni sawa na lengo lililowekwa. Aidha, kwa mwaka 2012 ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 6.9 na asilimia 6.4 mwaka 2011. Mafanikio haya yanatokana na juhudi za Serikali katika kuimarisha uchumi tulivu na utawala bora ambazo ni nguzo muhimu katika kuvutia uwekezaji nchini. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya mwezi Aprili 2014, Tanzania ni nchi ya 8 katika ukuaji wa uchumi katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, na ya kwanza katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ukuzaji wa ajira

48. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili 2014, jumla ya ajira mpya 630,616 zilikuwa zimezalishwa nchini katika sekta ya umma na sekta binafsi. Kati ya ajira hizo zilizozalishwa, sekta ya elimu ilizalisha ajira 36,073; Afya ajira 11,221; Kilimo ajira 130,974; Ujenzi wa miundombinu ajira 32,132; Nishati na Madini ajira 453; na Mawasiliano ajira 13,619. Aidha, kati ya ajira hizo, Serikali kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliajiri watu 3,055. Nafasi hizi ni nje ya nafasi zinazohusu sekta ya afya na elimu. Ajira zilizozalishwa katika sekta binafsi zilikuwa 211,970.

Mfumuko wa Bei

49. **Mheshimiwa Spika**, mfumuko wa bei nchini umeendelea kushuka kutoka asilimia 9.4 Aprili 2013 hadi kufikia asilimia 6.3 Aprili 2014. Lengo lililowekwa la mfumuko wa bei hadi Juni 2014 ni asilimia 6.0, ambalo kuna uwezekano wa kulifikia. Kupungua kwa kasi ya upandaji bei kulitokana hasa na sera madhubuti za fedha, hali nzuri ya hewa; jitihada za Serikali kuongeza ruzuku ya pembejeo za kilimo na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao; kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika nchi jirani; pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme.

Akiba ya Fedha za Kigeni

50. **Mheshimiwa Spika**, hali ya akiba ya fedha za kigeni mpaka mwisho wa mwezi Aprili 2014 iliendelea kuwa ya kuridhisha. Katika kipindi kilichoishia Aprili 2014, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 4,647.5 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 4,380.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka 2014 kinatosheleza uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje kwa zaidi ya miezi 4.6 ikilinganishwa la lengo la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma la miezi 4.0 hadi Juni, 2014.

51. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine ni pamoja na Serikali kugharamia shughuli za Tume ya Mabadiliko ya Katiba pamoja na uendeshaji wa Bunge Maalum la Katiba; kulipa mishahara ya watumishi kwa wakati; Ujenzi na utandazaji wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam umeendelea kutekelezwa kama ilivyopangwa; ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali unaendelea kufanyika; fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu iliitolewa kwa wakati; kugharamia ununuzi wa chakula cha hifadhi ya Taifa; kuendelea kugharamia huduma za jamii; na ununuzi wa pembejeo za kilimo.

Changamoto

52. **Mheshimiwa Spika**, licha ya mafanikio hayo, changamoto mbalimbali zimejitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/14. Changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji kwa wakati wa mikopo ya nje yenye masharti ya kibiashara; kuwepo kwa mahitaji makubwa ya fedha ikilinganishwa na upatikanaji wa mapato; ukusanyaji usioridhisha wa mapato yasiyo ya

kodi; gharama kubwa za uendeshaji wa mitambo ya kufua umeme wa dharura; kuongezeka kwa madai ya wakandarasi, wazabuni na watumishi; na kutokamilika kwa urasimishaji wa sekta isiyo rasmi na hivyo kusababisha ugumu wa kutoza kodi.

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto nilizoieleza, Serikali itaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu na faida za kulipa kodi kwa kutumia mitandao ya kielektroniki na kusimamia ulipaji kodi kwa hiari kupitia udhibiti wa matumizi ya mfumo wa Mashine za Kielektroniki za Kutoa risiti (*Electronic Fiscal Devices*) ulioboreshwa zaidi; na kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kutumia TEHAMA.

54. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa bajeti, Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti. Kuhusu madai ya Wakandarasi na Wazabuni, Serikali inakamilisha utaratibu wa kusimamia na kuyalipa madai yaliyohakikiwa kupitia Hazina kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zinazohusika. Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza Wizara na Taasisi kuzingatia mfumo wa malipo (IFMS) ambao unamtaka kila Afisa Masuuli kutoingia mikataba bila kuwa na LPO inayotokana na mfumo wa IFMS.

55. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa misaada na mikopo ya nje, Serikali itaendelea kufanya majadiliano mapema na wahisani pamoja na mabenki ili kuhakikisha kwamba fedha za misaada na mikopo zinapatikana kama ilivyopangwa na kwa wakati.

Aidha, Serikali itahakikisha inazingatia na kutekeleza kwa haraka masharti ya fedha za wahisani kulingana na makubaliano.

III. BAJETI YA MWAKA 2014/15

56. **Mheshimiwa Spika**, bajeti ya mwaka 2014/15 itaendelea kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye: Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010; Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/15 na Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now – BRN*); Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; na Programu za Maboresho katika Sekta ya Umma. Lengo likiwa ni kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

SHABAHA NA MISINGI YA BAJETI KWA MWAKA 2014/15

57. **Mheshimiwa Spika**, shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2014/15 ni kama ifuatavyo:-

(i) Pato halisi la Taifa linatarajia kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2014 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 7.7 kwa mwaka katika kipindi cha muda wa kati;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya upandaji bei ili ibaki kwenye viwango vya tarakimu moja, ambapo maoteo kwa kipindi kinachoishia Juni 2014 ni asilimia 6.0 na asilimia 5.0 Juni 2015;

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano wa asilimia 18.9 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2014/15;

(iv) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 4.9 ya Pato la Taifa mwaka 2014/15;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(v) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) katika wigo wa asilimia 15.5 kwa mwaka unaoishia Juni 2015 utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei;

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne kwa mwaka unaoishia Juni 2015; na

(vii) Kuimarisha thamani ya shilingi na kuwa na kiwango imara cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha.

58. Mheshimiwa Spika, ili kufikia shabaha na malengo yaliyoainishwa, misingi ya Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2014/15 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, utulivu na utengamano nchini, kikanda na Duniani;

(ii) Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, biashara ya nje na huduma za kifedha;

(iii) Mapato ya ndani yataongezeka kwa kuimarisha vyanzo vilivyopo na kubuni vyanzo vipya vya mapato na kupunguza misamaha ya kodi na kuongeza usimamizi;

(iv) Kuimarisha mfumo wa usimamizi na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma;

(v) Mfumo wa IFMS utaimarishwa na kuhakikisha unatumika kuweka mihadi ya huduma na bidhaa kabla ya malipo kuzingatia vipaumbele vilivyopo katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, MKUKUTA II pamoja na miradi itakayokuwepo katika "Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa";

(vi) Sera za fedha zitaendelea kuimarishwa ili ziendane na sera za bajeti zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei na tofauti ya riba za amana na za mikopo;

(vii) Mtengamano wa kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC utaendelezwa na kutumia vizuri fursa zilizopo; na

(viii) Mazingira ya biashara na uwekezaji yataendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vya utekelezaji wa sheria ya PPP ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi.

Sera za Mapato

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/15, Serikali itaendelea na juhudi za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali za kiseru na kiutawala kwa kupanua wigo wa kodi, kubuni vyanzo vipya vya mapato, kuimarisha usimamizi wa kodi, kupunguza misamaha ya kodi inayotolewa kupitia sheria mbalimbali za kodi ikiwemo sheria ya VAT. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na wadau mbalimbali ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bajeti ya Bunge, kikosi cha wataalam (*Lab*) cha kubuni vyanzo vya mapato katika mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa.

60. Mheshimiwa Spika, hatua za kiseru za kuongeza mapato zitakazozingatiwa kwenye Bajeti ya mwaka 2014/15 ni pamoja na:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(i) Kuimarisha taratibu za kukusanya mapato pamoja na kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi kwa kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi kwa lengo la kudhibiti na kupunguza misamaha hiyo;

(ii) Kuongeza usajili wa walipa kodi wapya na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;

(iii) Mamlaka ya Mapato Tanzania itaongeza siku za kufanya kazi ili kutoa muda wa ziada wa kuwahudumia walipa kodi bandarini na baadhi ya vituo vya mpakani ;

(iv) Kukamilisha utungwaji na kuanza kutekeleza Sheria Mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT);

(v) Kukamilisha utungwaji wa Sheria ya Usimamizi wa kodi (Tax Administration Act);

(vi) Kuendelea kuimarisha na kusisitiza matumizi ya mashine za elektroniki za kutoa stakabadhi za kodi (Electronic Fiscal Devices-EFDs) na kutoa elimu zaidi kwa walipa kodi na wafanya biashara kuhusu matumizi ya mashine hizo;

(vii) Kufuatia kukamilika kwa utafiti wa kuwianisha mifumo ya ukuanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, Serikali itaandaa mfumo wa usimamizi na utaratibu wa kukusanya;

(viii) Kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iingie kwenye mfumo rasmi wa kodi;

(ix) Taasisi, wakala na mamlaka za serikali kuwasilisha maduhuli yote kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia mfumo wa *retention*;

(x) Ili kukabiliana na ukwepaji kodi, Wizara ya Fedha itatoa namba maalum ya simu na anwani ya barua pepe ili kuwawezesha raia wema kutoa taarifa mbalimbali kuhusu ukwepaji kodi; na

(xi) Wizara, idara zinazojitegemea, mikoa, manispaa, majiji, halmashauri, wakala na taasisi, mamlaka zinazokusanya maduhuli na malipo mengine zinaagizwa kutumia mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha ukusanyaji na kupunguza upotevu wa mapato.

61. **Mheshimiwa Spika**, Sera za mapato katika mwaka 2014/15, zinalenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 12,178.0 sawa na asilimia 19.2 ya Pato la Taifa. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi ni shilingi bilioni 11,318.2 na mapato yasiyo ya kodi ni shilingi bilioni 859.8. Mapato yanayotokana na vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 458.5 sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

Misaada na Mikopo ya Masharti Nafuu

62. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na jitihada za kupata misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ili kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Kwa mwaka 2014/15, Serikali inatarajia kupokea misaada na mikopo ya masharti nafuu ya kiasi cha shilingi bilioni 2,941.5. Kati ya fedha hizo misaada na mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 922.1, Mifuko ya Kisekta shilingi bilioni 274.1 na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,745.3

63. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali itakamilisha na kuanza kutumia mwongozo mpya wa Ushirikiano katika Maendeleo. Mwongozo huu unalenga kuendeleza mafanikio yaliyopatikana chini ya MPAMITA na uwekaji wa misingi mipya hususan ufanisi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii (Development Effectiveness). Aidha, mwongozo huu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

unaainisha misingi ya majadiliano baina ya Serikali na wadau wa maendeleo ili misaada na mikopo inayotolewa iweze kuleta tija na matokeo yanayokusudiwa.

64. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na juhudi zao za kuchangia maendeleo yetu, naomba kuwatambua na kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kama ifuatavyo: Nchi za Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, India, Ireland, Italia, Japani, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, na Uswisi, pia taasisi mbalimbali za Kimataifa ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, BADEA, Global Fund, OPEC Fund, Saudi Fund, Umoja wa Ulaya, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Mbali na michango yao ya kifedha, Serikali pia inanufaika kutokana na ushauri na mawazo yao katika kutekeleza programu mbalimbali. Tunawashukuru na kuthamini mchango wao.

Mikopo ya Kibiashara ya Ndani na Nje

65. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya kuendeleza miradi ya miundombinu nchini, Serikali itaendelea kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kugharamia bajeti ya maendeleo. Katika mwaka 2014/15, Serikali inategemea kukopa katika soko la ndani jumla ya shilingi bilioni 2,955.2. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 689.56 sawa na asilimia 1.1 ya Pato la Taifa ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 2,265.7 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva kwa utaratibu wa *rollover*.

66. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 1,320.0 kutoka masoko ya fedha ya nje kwa masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Uamuzi wa kuendelea kukopa kwa masharti nafuu na ya kibiashara umezingatia tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa na umuhimu wa kuendeleza miradi ya kipaumbele hususan miundombinu ambayo itafungua fursa za kiuchumi na kuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi.

Sera za Matumizi

67. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Serikali imekadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 19,853.3 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Katika kipindi hiki mgawanyo wa matumizi ya Serikali utakuwa kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi bilioni 13,408.2 na matumizi ya maendeleo jumla ya shilingi bilioni 6,445.1.

68. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Serikali itatekeleza sera za matumizi zifuatazo:-

(i) Utoaji wa fedha kwa Mafungu utazingatia maombi na uwasilishwaji wa taarifa za matumizi (performance based disbursement) katika matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kila robo ya mwaka;

(ii) Kuwianisha matumizi na mapato yanayotarajiwa;

(iii) Kuimarisha zaidi usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, ikiwa ni pamoja na kuandaa Sheria ya Bajeti;

(iv) Taasisi zitumie wakala wa Serikali mtandao katika kuweka mifumo ya TEHAMA kwenye Taasisi zao ili kupunguza gharama za washauri kutoka nje;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(v) Wizara, idara zinazojitegemea, mikoa, halmashauri, wakala na Taasisi za Serikali zitafanya manunuzi yote kupitia Mfumo wa EFDs hivyo kuambatisha risiti zinazotokana na mashine za kielektroniki (EFDs);

(vi) Malipo yote ya Serikali yatalipwa kupitia akaunti moja ya Serikali iliyopo Benki Kuu ya Tanzania (Single Treasury Account);

(vii) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haitazidi asilimia 4.9 ya Pato la Taifa;

(viii) Mafungu yatazingatia matumizi yaliyokusudiwa pamoja na viwango vilivyoidhinishwa na Bunge;

(ix) Kutenga fedha za kutosha katika kutekeleza miradi ya vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo;

(x) Bajeti za Taasisi, wakala na mamlaka za Serikali zitawasilishwa na kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali;

(xi) Madai ya wakandarasi, wazabuni na watumishi yatahakikiwa na kulipwa na Wizara ya Fedha kwa kuzingatia bajeti za mafungu husika;

(xii) Serikali itazingatia ununuzi wa pamoja (bulk procurement) kutoka kwa wazalishaji badala ya wakala; na

(xiii) Matumizi yatazingatia Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2004 na manunuzi yatazingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake.

Mgawanyo wa fedha katika Sekta

69. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15 mgawanyo wa bajeti kwa sekta ni kama ifuatavyo:-

(i) Nishati na Madini: jumla ya shilingi bilioni 1,090.6 zimetengwa. Shilingi bilioni 290.2 zimetengwa kwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini; shilingi bilioni 151 kukamilisha ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam; na shilingi bilioni 90 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia Gesi wa Kinyerezi I. Hatua hii inalenga kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na kupunguza gharama zake na hivyo kuvutia uwekezaji na kuongeza ajira.

(ii) Miundombinu ya usafirishaji: jumla ya shilingi bilioni 2,109.0 zimetengwa, ambapo shilingi bilioni 179.0 kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa na ukarabati wa reli ya kati na shilingi bilioni 1,414.8 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja. Azma hii inalenga kupunguza msongamano wa magari mijini, gharama za usafiri na usafirishaji wa bidhaa na huduma, na hivyo kupunguza mfumuko wa bei.

(iii) Kilimo: jumla ya shilingi bilioni 1,084.7 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya SAGCOT; ujenzi wa maghala na masoko; na upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kukuza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Serikali itaendelea kuwekeza kwenye ugani kwa kuimarisha vyo vya utafiti katika kilimo na kuhakikisha kunakuwa na maofisa ugani wa kutosha na mbegu bora. Hatua hii itaimarisha uzalishaji wa mazao, usalama wa chakula na kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(iv) Elimu: jumla ya shilingi bilioni 3,465.1 zimetengwa, ambapo shilingi bilioni 307.3 zimetengwa kugharamia mikopo ya elimu ya juu. Aidha Serikali itaendelea kuimarisha ubora wa elimu ikijumuisha miundombinu ya elimu. Hatua hii itasaidia upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, kuimarisha na kujenga madarasa na maabara. Ili kuhakikisha vijana wetu wanapata fursa za ajira, juhudi zitawekwa pia kwenye kuimarisha vyuo vya ufundi stadi – VETA;

(v) Maji: jumla ya shilingi bilioni 665.1 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa visima katika vijiji 10 kwa kila Halmashauri na kukamilisha ujenzi wa bomba la maji kutoka Ruvu Chini hadi Dar es Salaam. Hatua hii itawaondolea wananchi kero ya kufuata maji mbali na makazi yao na hivyo kupata muda wa shughuli nyingine za uzalishaji, na kuwaondolea hatari ya kupata magonjwa kwa kutumia maji yasiyo salama;

(vi) Afya: jumla ya shilingi bilioni 1,588.2 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa madawa, kuzuia magonjwa ya mlipuko, chanjo za watoto, ujenzi wa zahanati na kudhibiti UKIMWI na Malaria;

(vii) Utawala Bora: jumla ya shilingi bilioni 579.4 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha utawala bora ikijumuisha kugharamia Bunge Maalum la Katiba; vitambulisho vya Taifa; uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2014; kuhuisha daftari la wapiga kura; maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015; mapambano dhidi ya rushwa na utoaji wa haki kwa wakati.

70. **Mheshimiwa Spika**, mgawanyo huu wa kisekta haujumuishi madeni ya kisekta yanayolipwa kupitia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS).

Masuala yanayohusu Mamlaka ya Serikali za Mitaa

71. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, mikoa na halmashauri zimetengewa shilingi bilioni 4,499 ikiwa ni nyongeza ya shilingi bilioni 685.87 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2013/14 ya shilingi bilioni 3,813. Nyongeza hii ni sawa na asilimia 18. Aidha, mapato ya ndani ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka kwa shilingi bilioni 85.9 kutoka shilingi bilioni 372.6 mwaka 2013/14 hadi shilingi bilioni 458.5 katika mwaka 2014/15. Ongezeko hili la mapato ya ndani ni sawa na asilimia 23.

72. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, shilingi bilioni 46.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya halmashauri mpya ambapo kila Halmashauri imetengewa shilingi bilioni 1.5. Aidha, shilingi bilioni 9.5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za wakuu wa wilaya katika maeneo hayo. Serikali itaendelea kuziwezesha Halmashauri hizo kupata nyenzo muhimu za utendaji kazi katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha, mwaka 2014/15, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa Halmashauri zenye mazingira magumu katika ujenzi wa nyumba za watumishi, ofisi, hospitali, hosteli, madaraja, barabara pamoja na miradi mingine maalum yenye kulenga kutoa huduma za haraka kwa wananchi ikiwamo maji, elimu na afya. Shilingi bilioni 53.99 zimetengwa katika mwaka ujao wa fedha kwa Halmashauri hizo.

73. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, shilingi bilioni 8.7 zimetengwa kwa ajili ya kazi za ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Mikoa 9 nchini. Mikoa hiyo ni Katavi, Simiyu, Njombe, Geita, Arusha, Pwani, Kilimanjaro, Singida na Tabora. Ni matumaini yangu kuwa kukamilika kwa kazi hizi kutaimarisha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Matumizi kwa Makundi Maalum

74. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua kero mbalimbali zinazowakabili walimu hususan walimu wa shule za msingi. Ili kukabiliana na kero hizo, Serikali imejipanga kuziondoa kero hizo kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) **Ujenzi wa nyumba za Walimu:** Serikali inaendelea na utaratibu wa ujenzi wa nyumba za walimu kwa awamu. Katika mwaka 2013/14, Halmashauri 40 zilipewa kila moja shilingi milioni 500 ili zianze ujenzi wa nyumba za walimu na kiasi kama hicho kitatolewa kwa Halmashauri hizo kwa mwaka 2014/15.

Aidha, shilingi milioni 500 zitatolewa kwa Halmashauri 80 zaidi, hivyo kufanya jumla ya Halmashauri 120 kunufaika na utaratibu huo, lengo likiwa ni kuzifikia Halmashauri zote mwaka 2015/16. Viongozi wa Serikali katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Kata wanahimizwa kusimamia kikamilifu fedha hizo ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa; na

(ii) **Malipo ya madai ya walimu:** Serikali inaendelea na utaratibu wa kulipa madai ya walimu yaliyohakikiwa, ambapo katika mwaka 2013/14, kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kimelipwa. Aidha, kwa mwaka 2014/15, madai ya walimu ambayo yatakuwa yamehakikiwa yataendelea kulipwa.

75. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Serikali itaendelea kuboresha huduma kwa wanafunzi katika shule na vyuo mbalimbali ili kuhakikisha vijana wetu wanasoma katika mazingira tulivu na bora. Ili kutekeleza hili, Serikali imepanga yafuatayo:-

(i) Kujenga maabara katika shule na vyuo na kuzipatia vifaa muhimu ikiwa ni pamoja na kutumia maabara zinazotembea ili kuwafikia wanafunzi wengi zaidi;

(ii) Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi waliopo vyuoni na watakojiunga na vyuo vya elimu ya juu; na

(iii) Kujenga maktaba mpya, kukarabati na kuimarisha zilizopo kwa kuzipatia vitabu zaidi vya kiada na ziada.

76. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazovikabili vyombo vya ulinzi na usalama, ikiwa ni pamoja na makazi na mahitaji mengine. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imepanga kutekeleza yafuatayo katika mwaka 2014/15:

(i) kuendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za askari katika maeneo mbalimbali nchini ambapo jumla ya shilingi bilioni 27.13 zimetengwa kwa ajili hiyo;

(ii) Kuendelea kuwapatia vitendea kazi; na

(iii) Kuendelea kuongeza mishahara ya askari na stahili nyingine kwa awamu kulingana na uwezo wa kibajeti katika kipindi husika.

77. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na kuongeza mishahara. Katika kuendelea na jitihada hizo, katika mwaka 2014/15, Serikali imepanga yafuatayo:-

(i) Kuongeza kima cha chini cha mishahara kwa watumishi wa umma; na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(ii) Kufanya marekebisho katika mfumo wa kodi ya mishahara (PAYE) kwa kupunguza kiwango cha kodi hadi kufikia kima cha chini cha kodi cha asilimia 12, kutoka asilimia 13 ambapo kiwango hicho kilikuwa asilimia 18.5 mwaka 2005/06 na kupunguzwa hadi asilimia 13 mwaka 2013/14.

78. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua umuhimu wa wastaafu ambao walitoa mchango mkubwa kwa Taifa hili. Kwa sasa wastaafu hawa wapo katika makundi mawili ambayo ni wastaafu wa Serikali ambao hawakuchangia katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanaolipwa shilingi 50,000 kwa mwezi na aina ya pili ni wastaafu ambao pensheni zao zinategemea michango yao katika mfuko husika.

79. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua kuwa viwango vinavyolipwa kwa sasa haviendani na uhalisia. Katika kutatua changamoto hii Serikali inapitia viwango hivyo ili kuongeza viwango kutegemeana na mapato ya Serikali na kuhakikisha malipo yanafanyika kwa wakati.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaendelea kuhuisha kanuni za ukokotoaji wa mafao ili kuweka ulinganifu wa mafao katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Ununuzi wa Umma

80. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali kupitia taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma nchini, itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na.7 ya Mwaka, 2011 ambayo imeanza kutumika Desemba, 2013 baada ya kanuni kukamilika. Sheria hiyo itaondoa changamoto mbalimbali zilizokuwepo katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 zikiwemo bei kubwa ya bidhaa ikilinganishwa na bei halisi ya soko pamoja na mchakato mrefu wa zabuni.

Hivyo, nitoe wito kwa wizara, idara zinazojitegemea, wakala na taasisi za Serikali na halmashauri zote na wadau wote kwa ujumla kuitumia Sheria hii kikamilifu. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuondokana na kasoro na malalamiko yaliyokuwepo hapo awali.

Sekta ya Fedha

81. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Serikali itakamilisha Sera na Mkakati wa Sekta ya Bima ili kutoa mwongozo wa kufidia hasara zinazotokana na majanga mbalimbali.

Aidha, Serikali itakamilisha Sera ya Taifa ya Taasisi Ndogo za Huduma za Kifedha na kutunga Sheria ya Taasisi hizo. Vilevile, Serikali inaandaa mapendekezo ya kutunga sheria ya mifumo ya malipo ili kuboresha matumizi ya kieletroniki kufanya malipo kwa kutumia simu za mkononi, huduma za benki kwa njia ya mtandao, vituo vya mauzo na mashine za kutolea fedha.

82. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua athari za riba kubwa zinazotozwa na benki na taasisi za fedha kwa mikopo itolewayo ambazo zinasababisha asilimia kubwa ya Watanzania kushindwa kufaidika na huduma za kifedha. Serikali imeanza kuchukua hatua za kutatua changamoto hizo kama ifuatavyo: kutekeleza programu ya kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge, kuanzisha taasisi inayotoa mikopo ya nyumba, kuendelea na zoezi la kutoa vitambulisho vya Taifa na anwani za makazi, kuchochea utumiaji wa Taasisi ya Kuhakiki Ukweli wa Taarifa za Waombaji Mikopo (Credit Reference Bureau), na kuimarisha mifuko ya dhamana ya mikopo inayosimamiwa na Benki Kuu.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu pamoja na wadau wengine itafanya tathmini ya viwango vya riba ili kuweza kubainisha sababu za viwango kuendelea kuwa juu na kuchukua hatua zinazostahili.

Ushirikiano wa Kikanda

83. **Mheshimiwa Spika**, Ushiriki wa nchi yetu katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika unazidi kuimarika, hasa baada ya kusainiwa, kuridhiwa na kutekelezwa kwa itifaki muhimu za biashara na uchumi. Hatua hizi zitaongeza fursa za uwekezaji na hivyo kukuza uchumi na kuongeza upatikanaji wa ajira.

Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, naomba kutoa taarifa kwamba mtangamano umefikia hatua ya kuanzishwa kwa Umoja wa Fedha ambapo Itifaki ya kuanzisha Umoja huo ilisainiwa na Wakuu wa nchi za Jumuiya mnamo tarehe 30 Novemba 2013. Ili kuimarisha ushirikiano katika hatua zilizofikiwa, Benki Kuu za nchi wanachama zimekubaliana kurahisisha taratibu za kufanya malipo kati ya nchi zetu (cross border payments), hivyo kuwezesha malipo kati ya nchi zetu kuwa rahisi na hivyo kuhamasisha utumaji wa fedha na biashara.

84. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha, naomba kutoa taarifa kwamba Serikali inakamilisha maandalizi ambapo kuanzia tarehe 1 Julai, 2014 mizigo inayokwenda nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki itakaguliwa mara moja katika bandari ya Dar es Salaam na kuruhusiwa baada ya nchi husika kuthibitisha kwa Mamlaka ya Mapato kwamba kodi imelipwa.

Hatua hii itapunguza muda wa mizigo hiyo kukaa bandarini, hivyo kupunguza gharama kwa wafanyabiashara na kuhamasisha ukusanyaji wa mapato na ukuaji wa uchumi wa nchi zetu. Kwa upande wa Itifaki ya Soko la Pamoja, naomba kutoa taarifa kwamba utekelezaji unaendelea na Serikali imetoa tangazo la kupunguza masharti ya uwekezaji wa mitaji baina ya nchi wanachama.

Kuhusu kuwianisha kodi za ndani, majadiliano ya kupata mfumo bora wa kuwianisha kodi hizo yanaendelea na yatakapokamilika Bunge lako Tukufu litajulishwa. Lengo ni kuhamasisha biashara sawia baina ya nchi wanachama kwa kuwa na taratibu za kodi na viwango vya kodi za ndani visivyotofautiana sana.

Kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), naomba kutoa taarifa kwamba Serikali inaendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara.

Aidha, napenda kulishukuru Bunge lako tukufu kwa kuridhia Itifaki ya Fedha na Uwekezaji ya nchi za SADC.

Uhusiano Kati ya Tanzania na Shirika la Fedha la Kimataifa kupitia Mpango wa Ushauri wa Kisera (Policy Support Instrument-PSI)

85. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kupitia mpango wa Ushauri wa Kisera ujulikanao kama Policy Support Instrument-PSI. Tanzania ilifanikiwa kujiunga na Mpango huu kutokana na juhudi zinazofanyika za kuimarisha uchumi tulivu na utawala bora. Mpango wa kwanza wa PSI ulianza kutekelezwa Februari 2007 hadi Juni 2010, na mpango wa pili ulianza Julai 2010 na kuishia Juni 2013. Mpango huu umekuwa chanzo kikuu cha kutoa ishara kwa wawekezaji na washirika wa maendeleo duniani juu ya ubora wa sera na mikakati, mipango na uwezo wa serikali katika kusimamia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ukuzaji uchumi, na upunguzaji umaskini nchini. Kutokana na mpango huu, nchi yetu imeendelea kupokea misaada na mikopo mbalimbali ikiwemo ya

kibajeti, miradi ya maendeleo pamoja na mifuko ya kisekta. Aidha, IMF imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukabiliana na misukosuko ya urari wa malipo ya nje kwa kuziba nakisi ya mapato ya fedha za kigeni.

86. **Mheshimiwa Spika**, Kutokana na mafanikio hayo, Serikali imeridhia kutekeleza Awamu ya Tatu ya Mpango wa PSI ambapo utekelezaji wake utanza Julai 2014 kwa kipindi cha miaka mitatu. Awamu hii itaendelea kuijengea nchi yetu uwezo wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia sera kwa lengo la kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika awamu mbili zilizotangulia pamoja na kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa na uchumi tulivu na endelevu na hivyo kuvutia zaidi uwekezaji na kuongeza fursa za ajira nchini.

Tathmini ya Uwezo wa nchi Kukopa na Kulipa Madeni

87. **Mheshimiwa Spika**, hatua ambazo zimefikwa hadi sasa ni kwa kupatikana kwa mshauri mwelekezi wa kuishauri Serikali ambapo Mkataba ulishasainiwa, Serikali pia imekamilisha hatua ya kumpata Mshauri wa Sheria wa Kimataifa (International Legal Adviser).

Aidha, Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kupata Kampuni za kufanya tathmini (Rating Agencies). Zoezi hili lilichelewa kutokana na kampuni za tathmini kutokubaliana na aina ya fomu za mikataba zinazoandaliwa na Serikali pamoja na kuleta nyongeza ya gharama nje ya makubaliano yaliosainiwa awali ambapo imeilazimu Serikali kuanza zoezi hilo upya. Kukamilika kwa zoezi hilo siyo tu kutawezesha Serikali kupata mikopo nafuu ya kibiashara kuliko ilivyo sasa, bali kutawezesha makampuni na taasisi binafsi za Tanzania kupata mitaji kwa urahisi kutoka soko la mitaji la kimataifa na kurahisisha uwekezaji wa sekta binafsi ambao ni muhimili wa uchumi. Aidha, zoezi hili ni muhimu katika kuiweka nchi kwenye ramani ya dunia hususan kiuchumi na kutambulika zaidi kwa wawekezaji.

IV. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA, TOZO NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO

88. **Mheshimiwa Spika**, Ili kuongeza mapato ya Serikali na kufikia malengo ya kiuchumi katika mwaka 2014/15, napendekeza kufanya marekebisha ya mfumo wa kodi na tozo, ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi na tozo nyingine zisizo za kodi chini ya sheria mbali mbali na pia taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali. Marekebisha hayo yanahusu sheria zifuatazo:-

- a. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;
- b. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147;
- c. Sheria ya Ushuru wa Mafuta, SURA 220;
- d. Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, SURA 124,
- e. Sheria ya Ushuru wa Mauzo Nje, SURA 196;
- f. Sheria ya Uwekezaji Tanzania, SURA 38;
- g. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82;
- h. Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya Mwaka 1972;
- i. Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

j. Marekebisho ya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na wizara, mikoa na idara zinazojitegemea;

k. Usimamizi wa kodi zinazotozwa kwenye mafuta ya petroli yanapoingizwa nchini.

l. Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya sheria za kodi na sheria nyingine mbali mbali;

m. Kurekebisha Sheria ya Fedha za Umma, SURA 348, Sheria ya Msajili wa Hazina SURA 418 na Sheria ya Wakala wa Serikali SURA 245 kwa minajili ya kuelekea kwenye kuunganisha fedha zote za umma chini ya Mfuko Mkuu unaodhibitiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

(a) Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332

89. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332 kama ifuatavyo: -

(i) Kutoa msamaha wa kodi kwenye mapato yanayotokana na mauzo ya hatifungani zitakazotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (African Development Bank) katika Soko la Mitaji la Tanzania. Hatua hii itawezesha Benki hiyo kuongeza uwezo wa kutoa mikopo nafuu ya uwekezaji kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile kuendeleza miundo mbinu n.k.

(ii) Kutoza Kodi ya Zuio ya asilimia 15 kwenye ada wanayolipwa wakurugenzi wa bodi kila mwisho wa mwaka;

(iii) Kufuta msamaha wa kodi ya makampuni kwenye mapato ya michezo ya kubahatisha;

(iv) Kufuta msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye ukodishaji wa ndege kwa walipa kodi wasio wakazi (non-resident). Hatua hii inalenga katika kupunguza misamaha ya kodi na kuongeza mapato ya Serikali;

(v) Kuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha ya kutoa misamaha ya kodi kwa miradi inayohusu upanuzi na ukarabati (expansion and rehabilitation) inayofanywa na wawekezaji. Msamaha huo hivi sasa unatolewa kwa utaratibu ambapo wawekezaji hupewa vyeti vya Kituo cha Uwekezaji (TIC Certificates);

(vi) Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka asilimia 13 hadi asilimia 12. Hatua hii inalenga katika kutoa unafuu wa kodi kwa wafanyakazi. Aidha, Serikali itaendelea kuangalia uwezekano wa kupunguza kiwango hiki hatua kwa hatua ili kuwapa nafuu wafanyakazi;

(vii) Kuongeza kiwango cha kutozwa kodi kwenye mapato ghafi ya wafanyabiashara wadogo yanayozidi shilingi 4,000,000 kwa mwaka na yasiyozidi shilingi 7,500,000 kwa mwaka, kutoka asilimia 2 hadi asilimia 4 kwa mauzo, kwa wanaoweka kumbukumbu za mauzo na kuongeza kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 200,000 kwa wasiokuwa na kumbukumbu za mauzo;

Hatua hizi za Kodi ya Mapato zitaongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 31,504**

(b) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147

Nakala ya Mtandao (Online Document)

90. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kufuta Ushuru wa Bidhaa wa asilima 0.15 unaotozwa kwenye uhawilishaji wa fedha (money transfer) ili kuwapa unafuu watu wanaotuma fedha kwa kutumia mabanki na kwa kutumia njia za simu. Badala yake napendekeza kuweka ushuru wa asilimia kumi kwa mabanki na mawakala kwenye mapato wanayopata kwenye tozo na ada wanazokusanya kwenye shughuli za uhawilishaji wa fedha;

(ii) Kuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha ya kutoa msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya petroli isipokuwa tu misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (Development Partners) ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji nk.

Lengo la hatua hii ni kupunguza matumizi mabaya ya msamaha huu na kuelekeza misamaha ya aina hii kwenye miradi ya maendeleo na yenye manufaa kwa umma. Aidha, hatua hii ina lengo la kuifanya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 iwe sanjari na Sheria ya TIC SURA 38 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2013 ambazo zilifanyiwa marekebisho ili kuondoa msamaha wa kodi kwenye mafuta ya petroli;

(iii) Kubadilisha ukomo wa umri wa magari yasiyo ya uzalishaji (non-utility vehicles) yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilimia 25 hivi sasa kutoka miaka kumi na zaidi kwenda miaka minane na zaidi. Lengo la hatua hii ni kulinda mazingira na kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu ambayo yanasababisha ajali, vifo na kuongeza gharama kwa kutumia fedha za kigeni kuagiza vipuri mara kwa mara;

(iv) Kubadilisha ukomo wa umri wa magari ya uzalishaji na yasiyobeba abiria (non-passenger utility vehicles) yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilimia 5 hivi sasa kutoka miaka kumi na zaidi kwenda miaka minane na zaidi. Aidha, kubadilisha ukomo wa umri wa magari ya kubeba abiria (passenger carrying vehicle) yanayotozwa ushuru wa uchakavu wa asilimia 5 sasa kutoka miaka kumi na zaidi kwenda miaka mitano na zaidi. Lengo la hatua hii pia ni kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu yanayoharibu mazingira, kusababisha ajali na vifo na kuongeza mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza vipuri mara kwa mara. Hata hivyo hatua hii haitahusisha matrekta ambayo yote yataendelea kuingizwa nchini bila kutozwa ushuru wowote;

(v) Kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika katika HS CODE 94.01. Aidha mwaka 2013/14 Serikali ilianza kutoza Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 15 kwenye samani zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zinazotambulika katika HS CODE 94.03. Lengo la hatua hizi ni kuhamasisha matumizi ya samani zinazotengenezwa kwa kutumia mbao zinazozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira na teknolojia katika kuzalisha bidhaa hii hapa nchini na kuongeza mapato ya Serikali;

(vi) Kurekebisha viwango maalum (specific rates) vya Ushuru wa Bidhaa zisizokuwa za mafuta (*Non-petroleum products*) kwa asilimia 10. Bidhaa hizo ni pamoja na vinywaji baridi, mvinyo, pombe, vinywaji vikali, n.k. Aidha, bidhaa za sigara zitatozwa Ushuru wa Bidhaa wa asilimia 25 ili kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Udhidhi wa Matumizi ya Tumbaku (Framework Convention on Tobacco Control) wa Shirika la Afya Duniani. Tanzania ni miongoni mwa nchi zililoridhia mkataba huu kwa kuwa unalingana na azma ya Serikali ya kulinda afya za wananchi wetu. Mabadiliko ninayopendekeza ni kama ifuatavyo:-

Nakala ya Mtandao (Online Document)

a. Ushuru wa vinywaji baridi, kutoka shilingi 91 kwa lita hadi shilingi 100 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 9 tu kwa lita;

b. Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (juisi) iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini kutoka shilingi 9 kwa lita hadi shilingi 10 kwa lita, ikiwa ni ongezeko la shilingi 1 tu kwa lita;

c. Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda (juisi) iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini kutoka shilingi 110 kwa lita hadi shilingi 121 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 11 tu kwa lita;

d. Ushuru wa bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa (unmalted), mfano kibuku, kutoka shilingi 341 kwa lita hadi shilingi 375 Kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 34 tu kwa lita;

e. Ushuru wa bia nyingine zote kutoka shilingi 578 kwa lita hadi shilingi 635 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 57 tu kwa lita;

f. Ushuru wa mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75 kutoka shilingi 160 kwa lita hadi shilingi 176 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 16 tu kwa lita;

g. Ushuru wa mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25 kutoka shilingi 1,775 kwa lita hadi shilingi 1,953 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 178 kwa lita;

h. Ushuru wa vinywaji vikali kutoka shilingi 2,631 kwa lita hadi shilingi 2,894 kwa lita, ikiwa ni ongezeko la shilingi 263 kwa lita;

i. Ushuru wa bidhaa kwenye maji yanayozalishwa viwandani hautaongezeka.

Marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara ni kama ifuatavyo: -

j. Sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 9,031 hadi shilingi 11,289 kwa sigara elfu moja. Hii ni sawa na ongezeko la shilingi 2,258 kwa sigara elfu moja au shilingi 2.25 kwa sigara moja;

k. Sigara zenye kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 21,351 hadi shilingi 26,689 kwa sigara elfu moja, ikiwa ni ongezeko la shilingi 5,338 au shilingi 5.30 kwa sigara moja;

l. Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 38,628 hadi shilingi 48,285 kwa sigara elfu moja, ikiwa ni ongezeko la shilingi 9,657 sawa na shilingi 9.65 kwa sigara moja;

m. Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara (cut filler) kutoka shilingi 19,510 hadi shilingi 24,388 kwa kilo, ikiwa ni ongezeko la shilingi 4,878 kwa kilo; na

n. Ushuru wa "cigar" unabaki kuwa asilimia 30.

Hatua hizi katika Ushuru wa Bidhaa kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 124,292.0**

(c) Sheria ya Ushuru wa Mafuta, SURA 220;

91. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Mafuta, SURA 220, ili kuondoa mamlaka ya Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa Ushuru wa Mafuta kupitia Sheria ya Ushuru wa Mafuta, SURA 220, isipokuwa misamaha inayotolewa kwenye mikataba iliyosainiwa baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ili kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile miundombinu ya barabara, maji, n.k.

(d) Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, SURA 124,

92. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usajili na Uhamishaji wa Magari SURA 124 kwa nia ya kutofautisha **mfumo** wa usajili wa magari na ule wa pikipiki kwa kuweka namba zinazoanzia na TZ kwa pikipiki badala ya T. Lengo la hatua hii ni kudhibiti uhalifu unaofanyika kwa kubadilisha namba za magari na kuweka kwenye pikipiki. Hatua hii haitaongeza mapato ya Serikali

(e) Sheria ya Ushuru wa Mauzo Nje, SURA 196;

93. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kupunguza kiwango cha Ushuru wa Mauzo ya Nje (Export Levy) unaotozwa kwenye ngozi ghafi zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi kutoka asilimia 90 au Shilingi 900 kwa kilo moja hadi asilimia 60 au Shilingi 600 kwa kilo moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Lengo la hatua hii ni kuzuia biashara ya magendo ya ngozi ghafi. Uchambuzi unaonyesha kuwa hivi sasa hakuna ngozi ghafi zinazosafirishwa nje kupitia vituo vya forodha na badala yake hupelekwa nje ya nchi kwa magendo. Aidha, lengo la kuongeza usindikaji wa ngozi hapa nchini ili kuongeza thamani na ajira bado halijafanikiwa. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 5,778.7**

(f) Sheria ya Uwekezaji Tanzania, SURA 38

94. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya mabadiliko yafuatayo kuhusu kodi na uwekezaji:-

i. Napendekeza kuondoa saruji katika orodha ya bidhaa zinazofikiriwa kuwa za mtaji (deemed capital goods) ambazo hupata msamaha wa kodi hivi sasa kupitia TIC. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa saruji hapa nchini na kulinda viwanda vya saruji kutokana na ushindani wa saruji inayoagizwa nje;

ii. Napendekeza kufuta misamaha ya kodi iliyokuwa inatolewa kwa makampuni ya simu (telecommunication operators) pale wanapoingiza nchini au kununua bidhaa za mtaji (deemed capital goods). Misamaha hii ni ile inayotolewa kwenye vifaa kama; minara ya mawasiliano, jenereta, uzio wa minara, magari, *base station*, vifaa vya kujikinga na radi na kadhalika.

iii. Napendekeza kutoa tafsiri mpya ya wawekezaji mahiri (strategic investors) kwa kufanya marekebisho ya kiwango cha chini cha mtaji kinachotumika katika kuwatambua wawekezaji mahiri. Napendekeza kiwango cha chini cha mtaji wa wawekezaji mahiri wanaotoka nje ya nchi kiongezeke kutoka Dola za Kimarekani milioni ishirini kufikia Dola za Kimarekani milioni hamsini. Lengo la hatua hii ni kuelekeza vivutio vya misamaha ya kodi kwa wawekezaji ambao wanaleta mitaji mikubwa. Hata hivyo, napendekeza kiwango cha mtaji kinachomtambulisha mwekezaji wa Kitanzania kuwa mahiri kibakie pale pale, cha Dola za Kimarekani milioni 20, ili kuwanufaisha wawekezaji wazalendo. Serikali inakusudia kuendelea na

Nakala ya Mtandao (Online Document)

uchambuzi wa kubaini namna bora zaidi ya kuvutia wawekezaji wakubwa kwenye miradi mikubwa na ya kimkakati ambayo itakuwa na msukumo mkubwa na wa haraka wa ukuaji wa uchumi, upanuaji ajira na uongezaji mapato ya wananchi.

Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 43,703.4**

(g) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82

95. **Mheshimiwa Spika**, katika marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Elimu na Mafunzo Stadi SURA 82 kupitia Mswada wa Sheria ya Fedha 2013 yaliingizwa maudhui mapya katika sheria hiyo ambapo taasisi zinazonufaika na msamaha wa tozo ya ufundi stadi zilipunguzwa na kubaki Idara za Serikali au Taasisi za Umma tu na ambazo zinapata fedha kwa asilimia 100 kutoka Serikalini.

96. **Mheshimiwa Spika**, kwa uzoefu wa utekelezaji wa mabadiliko haya tumeona kuwa baadhi ya taasisi ziliachwa katika msamaha huu kimakosa. Kwa mfano, mashirika ya umoja wa mataifa na ofisi za kibalazi hazitozwi kodi wala tozo kama hizi kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa. Hivyo basi, napendekeza kufanya marekebisho ili kuongeza taasisi zifuatazo katika msamaha wa tozo hii: (i) Ofisi za Kidiplomasia, (ii) Mashirika ya Umoja wa Mataifa na taasisi za nje zinazotoa misaada ambazo hazijihusishi na biashara kwa namna yoyote ile, (iii) Taasisi za kidini kwa wajiriwa wake ambao ni mahsus kwa kuendesha ibada tu, (iv) Mashirika yanayotoa misaada ya hiari yasiyohusisha na biashara kwa namna yoyote ile, (v) Serikali za mitaa, na (vi) Taasisi za elimu na mafunzo zinazotoa huduma bure na hazijihusishi na biashara katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo kwa namna yoyote ile.

(h) Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya Mwaka 1972

97. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Viwanda na Biashara wamewasilisha mapendekezo ya kutoza viwango mbalimbali vya ada za leseni za Biashara kwa kutumia Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972.

Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya mwaka 1972, ili kuipa Serikali mamlaka ya kutoza ada za leseni za biashara kwa viwango vilivyopendekezwa.

(i) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004

98. **Mheshimiwa Spika**, kikao cha maandalizi ya Bajeti cha Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Pre-Budget Consultations of EAC Ministers for Finance) kilichofanyika tarehe 3 Mei 2014 jijini Nairobi, Kenya, kilipendekeza marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa forodha (EAC Common External Tariff "CET") kwa mwaka wa fedha wa 2014/15 Kama ifuatavyo: -

(i) Kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 mabasi ya kubeba abiria yanayotambuliwa katika HS CODE 8702.10.99 ambayo yana uwezo wa kubeba abiria 25 na zaidi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuboresha huduma ya usafirishaji wa abiria na kupunguza ajali;

(ii) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano inayotambuliwa katika HS CODE 1001.99.10 na HS CODE 1001.99.90. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda na wazalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano. Aidha, itaimarisha utulivu wa bei ya bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia ngano hiyo;

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(iii) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri badala ya asilimia 10 kwenye malighafi inayotumika katika kutengeneza sabuni (LABSA) inayotambuliwa katika HS CODE 3402.11.00; HS CODE 3402.12.00 na HS CODE 3402.19.00, kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuendelea kutoa unafuu kwa viwanda vidogo na vya kati vya kutengeneza sabuni, hivyo kuweza kuongeza uzalishaji na ajira;

(iv) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 kwenye kemikali za kuuwa wadudu zinazotengenezwa kwa kutumia petroli zinazotambuliwa katika HS CODE 3808.91.39. Hatua hii inalenga katika kuwianisha kiwango cha ushuru unaotumika kwenye kemikali za kuulia wadudu zinazotengenezwa kwa kutumia pareto ambazo nazo zinatozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 25.

Aidha, hatua hii itahamasisha wazalishaji wa dawa za kuuwa wadudu kutumia pareto inayozalishwa hapa nchini na kuwezesha wakulima wa zao la pareto kuwa na soko la uhakika;

(v) Kupunguza Ushuru wa Forodha unaotozwa kwenye karatasi zinazotambuliwa katika HS CODE 4805.11.00; HS CODE 4805.12.00 na HS CODE 4805.30.00; kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10. Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa za karatasi kwa kuwa karatasi hizo hazizalishwi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo karatasi zinazotambuliwa katika HS CODE 4804.11.00, HS CODE 4804.21.00, HS CODE 4804.31.00 na HS CODE 4804.41.00 zitaendelea kutozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 25. Karatasi za aina hii ni zile zinazozalishwa na kiwanda cha Mufindi na lengo la kufanya hivyo ni kukilinda kiwanda hicho ambacho ndicho pekee kinachozalisha karatasi za aina hiyo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

99. Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, (EAC-Customs Management Act, 2004) kama ifuatavyo: -

(vi) Tanzania kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye mashine za kielektroniki za kukokotoa kodi (EFD) kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii itapunguza gharama za kununua mashine hizi na hivyo kuhamasisha matumizi yake na kuboresha usimamizi wa kodi.

(vii) Kurekebisha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kufuta msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye vijiti vinavyotumika katika kutengeneza njiti za viberiti. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha matumizi ya vijiti vinavyotokana na malighafi zinazopatikana hapa nchini.

(viii) Kuendelea kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye migahawa ya majeshi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Katika kipindi hicho Serikali ya Tanzania imetakiwa kuangalia njia mbadala hususan za kibajeti katika kutoa unafuu wa gharama za maisha kwa majeshi ya ulinzi.

(ix) Kurekebisha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye malighafi za kutengeneza mitungi ya gesi. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uwekezaji kwenye utengenezaji wa mitungi ya gesi katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(x) Kurekebisha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ili kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye vifaa vya kuzalisha umeme unaotokana na nguvu za upepo na jua. Hatua hii inalenga katika kutoa unafuu wa gharama za

Nakala ya Mtandao (Online Document)

uwekezaji katika kuzalisha na kuendeleza umeme unaotokana na nguvu ya upepo na jua na hivyo kuongeza upatikanaji wa nishati mbadala.

Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **milioni 1,456.1**

(j) Marekebisho ya Ada na Tozo Mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea

100. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbali mbali zinazotowazwa na wizara, mikoa na idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi.

(k) Usimamizi wa Kodi za Mafuta ya Petroli yanayoingizwa nchini

101. **Mheshimiwa Spika**, utaratibu wa utozaji wa kodi za mafuta ya Petroli unaotumika hivi sasa ni wa kuchelewesha malipo ambapo kodi inakadiriwa na baada ya kukadiriwa malipo hufanyika katika siku 45. Tanzania ni nchi pekee inayotumia utaratibu huu katika Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika Nchi hizo kodi zikishakadiriwa hukusanywa mara moja.

102. **Mheshimiwa Spika**, kwa kodi ambazo zinachangia mapato mengi kama vile kodi za mafuta ya petroli utaratibu huu unaathiri utekelezaji wa bajeti.

Aidha, ucheleweshaji wa malipo hayo hutoa mwanya wa ukwepaji kodi. Ili kuiwezesha Serikali kupata mapato yake kwa wakati na kuziba mianya ya ukwepaji kodi, napendekeza kodi inapokadiriwa, malipo yafanyike mara moja.

(l) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na sheria nyingine mbalimbali

103. **Mheshimiwa Spika**, napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo katika sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Mapendekezo haya yanaonekana katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya 2014.

Tarehe ya Kuanza Kutekeleza Hatua Mpya za Kodi

104. **Mheshimiwa Spika**, Hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2014, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

V. SURA YA BAJETI KWA MWAKA 2014/15

105. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na shabaha ya bajeti, sura ya bajeti itakuwa kama ifuatavyo; Serikali imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 19,853.3 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Mapato ya kodi na mapato yasiyo ya kodi yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 12,178.0 sawa na asilimia 19.2 ya Pato la Taifa. Aidha, mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 458.5 sawa na asilimia 0.7 ya Pato la Taifa.

106. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/15, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuendelea kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 2,941.6. Kati ya fedha hizo,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

shilingi bilioni 922.2 ni misaada na mikopo ya kibajeti, shilingi bilioni 1,745.3 ni mikopo na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 274.1 ni Mifuko ya Pamoja ya Kisekta.

107. **Mheshimiwa Spika**, ili kuziba nakisi ya bajeti, Serikali inatarajia kukopa kutoka katika vyanzo vya ndani na nje shilingi bilioni 4,275.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 2,265.7 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na mkopo wa ndani shilingi bilioni 689.6 ambao ni asilimia 1.1 ya Pato la Taifa na shilingi bilioni 1,320 ambazo ni mikopo yenye masharti ya kibiashara zitatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

108. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu matumizi, jumla ya shilingi bilioni 19,853.3 zimekadiriwa kutumika katika mwaka 2014/15, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 13,408.2 ambayo yanajumuisha shilingi bilioni 5,317.6 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Serikali, Wakala na Taasisi za Serikali; Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi bilioni 4,354.7, na Matumizi Mengineyo shilingi bilioni 3,735.9.

109. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2014/15, jumla ya shilingi bilioni 6,445.1 sawa na asilimia 33 ya bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Aidha, asilimia 69 ya fedha za maendeleo zitagharamiwa na fedha za ndani ambayo ni shilingi bilioni 4,425.7. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 689.6 zinatokana na mkopo kutoka vyanzo vya ndani, shilingi bilioni 1,320 ni mikopo ya masharti ya kibiashara, shilingi bilioni 375.5 ni mikopo ya kibajeti, na shilingi bilioni 2,040.6 inatokana na mapato ya ndani.

Kiasi cha shilingi bilioni 2,019.4 kitagharamiwa kwa fedha za nje, misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo ikijumuisha Mifuko ya Kisekta sawa na asilimia 31 ya bajeti ya maendeleo.

110. **Mheshimiwa Spika**, kiwango cha mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo kimeendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2014/15, fedha za ndani katika bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 4,425.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2,952.9 zilizotengwa mwaka 2013/14 sawa na ongezeko la asilimia 50.

111. **Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya mwaka 2014/15, inazingatia pia mahitaji muhimu ya kitaifa ambayo hayawezi kuepukwa ikijumuisha gharama za uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2014 na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, Bunge Maalum la Katiba, upigaji kura ya maoni na uboreshaji wa daftari la wapiga kura.

112. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama ulivyoielezwa hapo juu, mfumo wa bajeti kwa mwaka 2014/15 unakuwa kama ifuatavyo:-

HITIMISHO

113. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoieleza hapo awali, Bajeti ya mwaka 2014/15 imelenga kuongeza makusanyo ya mapato, hasa ya ndani kwa kuanzisha vyanzo vipya, kuboresha vilivyopo na kupunguza misamaha ya kodi. Aidha, Bajeti hii imelenga kuongeza upatikanaji wa nishati ya umeme wa uhakika, kuboresha elimu, kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miuondombinu ya barabara, reli na viwanja vya ndege. Hii itasaidia pia kutumia vyema fursa za kijiografia.

114. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoieleza, Serikali imepanga kushughulikia kwa nguvu zaidi kero mbalimbali zinazowakabili wananchi zikiwemo kero ya upatikanaji wa maji, nishati ya uhakika, elimu juu ya umuhimu na faida za kulipa kodi kwa kutumia mitandao ya kielektroniki na kusimamia ulipaji kodi kwa hiari kupitia udhibiti wa matumizi ya mfumo wa Mashine za Kielektroniki za Kutoa risiti (*Electronic Fiscal Devices*) ulioboreshwa zaidi; kuboresha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa kutumia TEHAMA.

115. **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa bajeti, Serikali inaandaa Muswada wa Sheria ya Bajeti. Kuhusu madai ya Wakandarasi na Wazabuni, Serikali inakamilisha utaratibu wa kusimamia na kuyalipa madai yaliyohakikiwa kupitia Hazina kwa kushirikiana na wizara na taasisi zinazohusika. Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza wizara na taasisi kuzingatia mfumo wa malipo (IFMS) ambao unamtaka kila Afisa Masuuli kutoingia mikataba bila kuwa na LPO inayotokana na mfumo wa malipo wa IFMS.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

116. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa misaada na mikopo ya nje, Serikali itaendelea kufanya majadiliano mapema na wahisani pamoja na mabenki ili kuhakikisha kwamba fedha za misaada na mikopo zinapatikana kama ilivyopangwa na kwa wakati. Hata hivyo, upatikanaji wa fedha za misaada na mikopo kwa wakati inategemea umakini na usahihi wa kutekeleza miradi iliyokusudiwa kulingana na malengo na makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

117. **Mheshimiwa Spika**, kufanikiwa kwa Bajeti hii kunahitaji nidhamu ya hali ya juu ya wadau wote ikiwemo Serikali na taasisi zake, Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla. Ili kufikia azma hii juhudi za pamoja kati ya Serikali na wadau wote zinahitajika ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi kwa kuwekeza zaidi katika maeneo ya kipaumbele. Natoa rai kwa kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake ili Bajeti hii iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa. Inawezekana, tutimize wajibu wetu.

118. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Jedwali Na 1: Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato ya Serikali: 2007/08 - 2014-15

Shilingi Milioni

	2007/08	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13	2013/14	2013/14	2014/15
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Bajeti	Matarajo	Bajeti
Jumla ya Mapato (Yakijumuishwa Halmashauri)	3,634,580.6	4,240,074.3	4,661,540.3	5,736,266.1	7,221,408.6	8,442,610.8	11,537,522.6	10,580,149.9	12,636,504.6
A. Mapato yanayotokana na Kodi	3,359,249.8	4,043,673.0	4,427,833.7	5,293,277.3	6,480,477.8	7,729,985.9	10,395,439.8	9,682,642.3	11,318,222.0
1. Ushuru wa Forodha	289,275.6	359,255.3	367,070.1	448,650.2	497,686.8	584,136.9	852,199.0	796,355.0	941,904.5
2. Ushuru wa Bidhaa	660,888.2	762,092.7	837,622.3	1,052,152.2	1,028,883.8	1,258,242.1	1,908,857.0	1,666,831.2	1,953,287.7
3. Kodi ya Ongezeko la Thamani	1,042,489.7	1,231,135.4	1,389,624.3	1,530,641.3	1,974,820.2	2,146,336.7	2,590,291.0	2,442,887.2	2,869,214.9
4. Kodi ya Mapato	983,804.3	1,228,645.8	1,334,019.7	1,660,385.2	2,246,783.7	3,034,359.9	3,656,505.6	3,691,175.8	4,299,715.4
5. Kodi Nyingine	382,792.0	462,543.8	499,497.2	601,448.4	732,303.2	706,910.4	1,387,587.3	1,085,393.1	1,254,099.5
B. Mapato yasiyotokana na Kodi	275,330.8	196,401.3	233,706.6	442,988.8	740,930.9	712,624.9	1,142,082.7	897,507.6	1,318,282.6
1. Gawio la Mashirika	58,253.5	25,865.9	18,630.7	26,154.6	207,352.0	47,602.4	122,047.1	87,012.0	142,393.3
2. Wizara Nyingine na Mikoa	172,797.3	155,334.5	177,841.2	231,839.4	311,317.7	414,925.0	614,654.1	499,551.6	717,418.3
3. Mapato Mengine yasiyo ya Kodi	44,280.0	15,200.9	37,234.7	26,714.9	26,736.7	29,262.6	21,929.7		
5. Mapato ya Halmashauri	0.0	0.0	0.0	158,280.0	195,524.5	220,835.0	383,451.8	310,944.0	458,471.0

Chanzo: Wizara ya Fedha

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Jedwali 2a: Mfumo wa Bajeti 2007/08-2014/15

	Shilingi Milioni								
	2007/08	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12	2012/13	2013/14	2013/14	2014/15
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Bajeti	Matarajio	Bajeti
apato									
ote	5,269,042	6,839,106	8,965,856	10,202,603	12,171,877	15,404,216	18,248,982	17,096,772	19,853,331
apato									
a dani/l	3,634,581	4,043,673	4,645,213	5,577,986	7,025,884	8,221,776	11,154,071	10,098,696	12,178,034
apato									
a alma-									
a iauri	0	0	0	158,280	195,525	220,835	383,452	268,416	458,471
isaada									
a ikopo									
a Bajeti	990,452	936,422	1,224,096	900,825	967,163	894,955	1,163,131	988,661	922,168
isaada									
a ikopo									
a iradi	844,970	797,376	1,134,708	1,013,078	1,207,445	1,423,579	1,796,874	922,255	1,745,344
ikopo									
a sekta									
a iasket									
a ans)	200,628	151,370	194,071	220,681	172,212	186,336	234,352	199,199	84,975
isaada									
a Kisekta									
a iasket									
a rants)	197,953	263,866	258,067	334,609	301,152	280,936	266,070	266,070	189,112
DRI									
MF)	114,200	67,997	22,403	0	0	0	0	0	0
CA (T)									
SA	0	11,733	19,930	196,114	221,601	220,350	394,773	335,557	0
ikopo									
lyo ya									
enki	-19,795	1,108	714,315	720,249	1,326,852	1,734,535	1,147,576	1,973,677	2,265,665
ikopo									
a Benki	-316,755	212,567	559,769	1,244,330	334,864	1,069,321	552,284	552,284	689,562
areke-									
isho	-377,192	307,994	164,625	-317,498	-382,101	88,588	0	335,557	0
apato									
ito-									
ina na									
binafsi-									
raji	0	45,000	9,659	0	0	0	0	0	0
ikopo									
a kibia-									
ara				153,948	801,282	1,063,006	1,156,400	1,156,400	1,320,000
areje-									
vo ya									
idha			19,000	0					
a EPA									
atumi-									
Yote	5,269,042	6,839,106	8,956,395	10,202,602	12,171,877	15,404,216	18,248,983	17,096,772	19,853,331
atumi-									
ya									
awa-									
a	3,458,070	4,708,737	6,345,089	7,453,565	8,397,155	10,904,521	12,574,949	12,085,214	13,408,218
FS	583,799	682,183	1,464,318	1,625,883	2,518,207	3,383,124	3,319,156	4,251,539	4,354,731
ulipa									
adeni	324,880	269,947	1,031,536	1,116,572	1,843,666	2,627,946	2,535,700	3,223,083	3,653,790
alipo									
engli-									
e	258,919	412,237	432,782	509,311	674,541	755,178	783,456	1,028,456	700,941
atumizi									
a awaida	2,874,271	4,026,554	4,880,770	5,827,682	5,878,949	7,521,397	9,255,792	7,833,675	9,053,487

Nakala ya Mtandao (Online Document)

o/w Malipo ya Mishahara	1,134,709	1,608,591	1,723,414	2,346,378	2,722,084	3,349,959	4,246,239	4,336,239	5,317,550
Mishahara ya Mashirika	216,762	303,290	349,188	457,665	455,006	518,755	516,957	546,957	627,204
Fedha ya Halimashauri	0	0	0	158,280	195,525	362,206	383,452	268,416	458,471
Matumizi Mengi	1,522,800	2,141,950	3,600,274	3,628,554	2,506,333	3,290,477	4,109,144	2,682,063	2,650,263
Matumizi ya Maendeleo	1,810,972	2,130,368	2,611,306	2,749,037	3,774,722	4,499,695	5,674,034	5,011,559	6,445,113
Fedha za Ndani	567,421	906,023	1,004,530	984,555	1,872,312	2,314,718	2,981,965	2,952,920	4,425,682
Fedha za Nje	1,243,551	1,224,345	1,606,776	1,764,482	1,902,410	2,184,977	2,692,069	2,058,638	2,019,431
Pata la Taifa	22,865,041	26,497,163	30,253,063	34,913,220	41,125,481	48,385,096	55,228,402	55,559,000	63,262,582

Chanzo: Wizara ya Fedha

Jedwali Na. 3 Misaada na Mikopo kutoka Nje 2011/12 - 2014/15


		Shilingi Milioni			
		2011/12	2012/13	2013/14	2014/15
		Halisi	Halisi	Bajeti	Bajeti
Misaada ya Kibajeti	Misaada	720,313	537,474	776,910	546,709
	Mikopo yenye Masharti Nafuu	246,850	357,481	386,221	375,459
	Jumla	967,163	894,955	1,163,131	922,168
Mifuko ya Kisekta	Misaada	301,152	280,936	266,070	189,112
	Mikopo yenye Masharti Nafuu	172,212	186,336	234,352	84,975
	Jumla	473,364	467,272	500,422	274,087
Miradi ya Maendeleo	Misaada	612,031	689,190	952,413	745,344
	Mikopo yenye Masharti Nafuu	595,414	734,389	844,461	1,000,000
	Miradi ya MCC	221,601	220,350	394,773	-
	Jumla	1,429,046	1,643,928	2,191,647	1,745,344
Jumla Kuu		2,869,573	3,006,155	3,855,199	2,941,599

Chanzo: Wizara ya Fedha



Nakala ya Mtandao (Online Document)



Jedwali 4: Mwenendo wa Deni la Taifa


KIWANGO CHA MIKOPO MIPYA YA NDANI NA NJE (MILIONI SHILINGI)			
	2012/13	2013/14	2014/15
1. Jumla ya Mikopo mipya ya Ndani na nje (a-b)	4,034,257.0	4,321,293.7	5,735,661.7
(a) Mikopo Mipya ya Ndani	1,631,958.0	1,699,860.0	2,955,227.5
(i) Mikopo mipya ya Ndani (Kulipia dhamana za Serikali zilizoiva)	1,148,107.0	1,147,576.0	2,265,665.3
(ii) Mikopo mipya ya Ndani (Kuziba nakisi ya Bajeti)	483,851.0	552,284.0	689,562.1
(b) Mikopo Mipya ya Nje	2,402,299.0	2,621,433.7	2,780,434.2
(i) Mikopo yenye Masharti nafuu (Miradi ya Maendeleo)	928,223.0	1,078,812.7	1,084,975.0
(ii) Mikopo yenye Masharti nafuu (Bajeti)	219,984.0	386,221.0	375,459.2
(iii) Mikopo yenye masharti ya Kibiashara	1,254,092.0	1,156,400.0	1,320,000.0
(c) Malipo ya Madeni ya Ndani	1,543,276.0	1,767,840.8	2,921,270.2
(i) Mtaji -Kulipia Dhamana za Serikali zilizoiva (Rollover)	1,148,107.0	1,147,576.0	2,265,665.3
(ii) Riba	395,169.0	617,087.8	652,427.8
(vi) Madeni Mengineyo-contingent Liability (Lakilaki)		3,177.0	3,177.0
(d) Malipo ya Madeni ya Nje	321,255.9	767,859.5	732,519.5
(i) Riba	220,047.4	377,426.0	342,086.00
(ii) Mtaji	101,208.5	390,433.5	390,433.47
(e) Ongezeko Halisi la Mikopo ya Ndani (a-c(i))	483,851.0	549,107.0	686,385.1
(f) Ongezeko Halisi la Mikopo ya nje (b-d(ii))	2,301,090.5	2,231,000.2	2,390,000.7
2. Ongezeko Halisi la Mikopo ya Ndani na Nje (e+f)	2,784,941.5	2,780,107.2	3,076,385.8



Nakala ya Mtandao (Online Document)







SPIKA: Kwanza naomba nimpongeze Meshimiwa Waziri kwanza kwa kuwasilisha vizuri bajeti yake. Kweli umewakilisha vizuri, habari ya ndani mimi sijui. Lakini kuwakilisha imekuwa vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo naomba niwatambue kwa sababu nina wageni wengi, kwa hiyo basi naomba nitangaze matangazo machache ya mwanzo kwanza.

Waheshimiwa Wabunge tumekaribishwa katika siku ya uzinduzi wa video ya wimbo maalum wa miaka 50 ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, tarehe si ndiyo naendelea.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete atakuwa mgeni rasmi katika tamasha hilo ambalo litafundisha watu kuhamasisha uzalendo na hivyo uzinduzi wa video ya wimbo maalum wa miaka 50 ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar. *(Makofi)*

Tamasha hilo limeandaliwa na muungano wa Wasanii nchini, wanaitwa TZ 50. Tamasha la uzinduzi huo utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 14 Juni, 2014 katika Uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma kuanzia saa 9 alasiri. Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kuhudhuria katika uzinduzi huo. Ni burudani tosha maana yake ni wasanii wote wapo hapo. Kwa hiyo mnakaribishwa sana.

Lakini tangazo lingine ni kwamba kwa Wabunge wote ni kwamba tarehe 15 Juni, siku ya Jumapili kutakuwa na mchezo wa mpira wa miguu na pete kati ya timu ya Bunge na timu ya NMB kuanzia saa 9.30 alasiri katika Uwanja wa Jamhuri na baadaye kutakuwa na tafrija fupi ya kukabidhi zawadi kwa washindi itakayofanyika Dodoma Hoteli kuanzia saa moja jioni. Kwa hiyo mnakaribishwa, hiyo ni tarehe 15 Juni na nyingine ni tarehe 14 Juni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitambue wageni tulio nao, wapo wengi lakini nitawataja hawa wageni, maana yake niliwaalika mimi mwenyewe.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwanza kabisa tunaye Katibu Mkuu Kiongozi, yeye ni kiongozi wa watumishi wote na Serikali nzima Ndugu Balozi Ombeni Sefue, nadhani yupo pale, ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu tuna Kamishna Mkuu wa TRA Ndugu Rished Bade, mtanisamehe kwa kutamka hovyoy.

Pia tunae Gavana wa Benki Kuu, Profesa Benno Ndulu, tunae Naibu Gavana wa Benki Kuu, Dkt. Natu Mwamba, tunae Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, nafikiri leo hakuja.

Pia tunae Naibu Inspekta Jenerali wa Polisi nchini, Ndugu Abdulrahman Kaniki, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunae Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Raphael Muhuga, tunae Kamishna Mkuu wa Magereza nchini, Ndugu John, samahani majina yao wameandika, John Casmir Minja, wana vyeo vyao ninyi mmeandika tu. *(Makofi)*

Tunae Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Ndugu Rashid Othman, pia tunae Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, Dkt. Philip Mpango nilimwona asubuhi. Pia yupo mwakilishi wa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Ndugu Paniel Mgonja. *(Makofi)*

Wengine ni Naibu Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Jaspa Mero, Mkuu wa Polisi Mkoa wa Dodoma wote wanaitwa ndugu lakini wana vyeo vyao Ndugu David Misime. Pia tuna Mkuu wa Usalama wa Mkoa wa Dodoma, Ndugu Prudenciana Amos. *(Makofi)*

Halafu nina Wabunge wa Afrika Mashariki, yupo Mheshimiwa Adam Kimbisa, Mheshimiwa Shy-Rose Bhanji, Mheshimiwa Angela Kizigha, Mheshimiwa Twaha Takrima, Mheshimiwa Mariam Ussi, Mheshimiwa Benard Murunya, Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, Mheshimiwa Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Dkt. Nderakindo Kessy. *(Makofi)*

Wanashangilia wanasema mmeonyesha mfano wa kutokuleta malumbano yasiyokuwa na maana na Spika wenu. *(Makofi)*

Wageni wengine nina Dkt. Servacius Likwelile - Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Profesa Adolf Mkenda, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Ndugu Dorothy Mwanyika, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha - Ndugu Elizabeth Nyambibo, Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa John Samwel Malecela, nafikiri yupo somewhere. Ahaa, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia yupo Spika Mstaafu Mheshimiwa Pius Msekwa, yupo mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mama Tunu Pinda, yupo mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mama Asha Seleman Iddi, yupo mama mzazi wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha Mama Mvita Kibendera. Mama mzaa chema, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia mdogo wa Waziri wa Fedha, Ndugu Lubna Salum, yupo mke wa Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Naibu Waziri wa Fedha pamoja na watoto wake, Mama Neema Mchemba, ahsante. *(Makofi)*

Pia yupo mke wa Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wa Fedha, Mama Naima Malima. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tuna wageni wetu wengine Mabalazi, tuna Waheshimiwa Mabalazi. Yupo Balozi wa Jamhuri ya Watu wa Congo na Mkuu wa Mabalazi nchini Mheshimiwa Juma Alfani Mpango, ahsante, yeye ndiye Dean wa Mabalazi wote.

Pia yupo Balozi wa Namibia nchini Tanzania Ndugu Japhet Isaack, yupo Balozi wa Mozambique nchini Tanzania, Mheshimiwa Pedro Joao de Azevedo Davane, yupo Balozi wa Afrika ya Kusini nchini Tanzania Mheshimiwa Thanduyise Henry Chiliza, ahsante. (Makofi)

Yupo Balozi wa Indonesia nchini Tanzania Mheshimiwa Zacharia Anshar, yupo Balozi wa Zimbabwe nchini Tanzania Mheshimiwa Edzai Chimonyo, yupo Kaimu Balozi wa Rwanda nchini Tanzania Mheshimiwa Labet Msanoo na yupo Mheshimiwa Mwakilishi wa Balozi wa Marekani, jina hawakuniandikia. Naomba asimame alipo. (Makofi)

Halafu tuna wengine ni Mabalazi lakini wahisani wanaochangia bajeti Kuu ya Serikali yaani *General Budget Support Development Partners*. *I am sure I am going to name mess up some of your names, but you will be bear with me.* Tunae Ambassador wa Finland na ndiyo GBS Chairperson Mheshimiwa Sinikka Antila. (Makofi)

Tunae Head of EU Delegation Honorable Filiberto Ceriani Sebregondi and there is Ambassador of Sweden, Honorable Leonard Head Maker. (Makofi)

Also Ambassador of Norway Honorable Ingunn Klepshvik. (Makofi)

There is Ambassador of Japan Honorable Masaki Okada, this one has got African name. Tuna-representatives, tuna Honorable Joan Kidera, representing the Ambassador of Canada. Thank you.(Makofi)

We have Claudia Melody, representing the Ambassador of Germany, we have the Head of DFID Honorable Marshaal Elliot, mwakilishi wa AFDB representative Honorable Tonia Kandiero. (Makofi)

We have the Country Director of World Bank, Honorable Philippe Dongier. The Head of Co-operation Finnish Embassy Mr. Kati Manner. We have the Economist of Finnish Embassy, Ndugu Lotta Voltonen.

Also we have the Program Officer, Finnish Embassy, Sebastian Gahnström. We have GDS Secretariat Finnish Embassy, Verena Knippel. We have GDS Secretary Finnish Embassy, Kalle Hellman and we have GDS Secretary Finnish Embassy, Paulina Mrosso. (Makofi)

Hawa Wafinland wamekuja wengi kwa sababu ndiyo Chairpersons wa GDS.

Halafu tuna Swedish Embassy, yupo Lars Johansson ni Economist, halafu tuna Emmanuel Mungunasi, Senior Economist World Bank.(Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunae Joram Rugemalila, Senior Economist Adviser, Embassy ya Japan. Yupo Joseph Nyamboha, Economist - JICA Tanzania. (Makofi)

Wengine ni Olivier Coupleux – Head Economic Section ya EU, yupo Vagine De Ruyt – Public Finance Manager Lead – EU, yupo Richard Moberly – Senior Economist – DFID, yupo Nick Highton – DFID – PFM Specialist, yupo Prosper Charles – Senior Economist African Development Bank na yupo Katrin Brandes, Senior Project Manager, KfW/Germany. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Halafu zipo taasisi nyingi zilizowakilishwa hapa, yupo *UN Resident Coordinator* wa UNDP, *Honorable Philippe Ponsoti*, halafu yupo *Deputy UN Resident Coordinator* na *UNICEF Country Representative* Dkt. Jama Gulaid, halafu na *Country Resident Representative* wa IMF - Thomas Baunsgaard. *(Makofi)*

Halafu nina Makatibu Wakuu, naomba waliofika hapa kuna Katibu Mkuu wa Utumishi, yupo Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, yupo Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (Katibu Mkuu), yupo Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

Halafu tuna wasaidizi wa Rais kama 15, sijui wako wapi? Kama wako ndani wasimame walipo, wengi tu 15. *(Makofi)*

Kuna Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi wa Mkoa wa Dodoma, yupo Mkuu wa Kikosi JWTZ – Msalato, siyo jina lake Msalato, anatokea Msalato. *(Kicheko)*

Yupo Mkuu wa Kikosi JWTZ Ihumwa, halafu yupo Mkuu wa Kikosi JKT Makutupora na yupo Mkuu wa Magereza Dodoma. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Halafu tuna Wakuu wa Mashirika, Taasisi za Umma na Fedha, hawa wapo wa NSSF, LAPF, GEPEF, NMB, CRDB, NBC, Benki ya Posta, TTCL, Shirika la Posta na Twiga Bancorp. *(Makofi)*

Halafu na viongozi wa Taasisi za Elimu ya Juu hapa Dodoma, tuna Kiongozi Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, nasikitika majina yenu hawakuniandikia. *(Makofi)*

Wengine ni kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu John, ahsante wako huku, Chuo Kikuu cha Mipango na Chuo kingine cha Biashara. Naona walishindwa kuandika. *(Makofi)*

Halafu tuna viongozi mbalimbali wa dini Mkoa wa Dodoma, tuna Kiongozi wa Madhehebu ya CCT sijui yuko wapi. Pia tuna Kiongozi wa Madhehebu TEC na halafu tuna Kiongozi wa BAKWATA. Ahsante sana, hawa wapo upande huu. *(Makofi)*

Halafu viongozi na watendaji waandamizi wa Mkoa wa Dodoma, yupo Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma (RAS). Yeye yuko wapi? Maana yake hawa ndiyo wenyeji wetu.

Pia wapo Wakuu wa Wilaya, yupo Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, yupo hapa, yupo Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, yupo kule na yupo Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Kuna Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma, amekaa wapi, naye yupo hapa. Wapo Waheshimiwa Madiwani wa Manispaa ya Dodoma wapo 15. Waheshimiwa Madiwani wako wapi? Ahaa wako hapa, tumekaa wachache wamewakilishwa na yupo Mkurugenzi wa CDA. Ahsante sana yupo pale. *(Makofi)*

Kuna Wazee wa Mkoa wa Dodoma, yupo Mwenyekiti wa Wazee wote wa Dodoma, yeye yupo wapi Mzee wetu? Yupo pale, amesimama pale. *(Makofi)*

Pia yupo Katibu wa Wazee, Katibu wetu, ahsante sana, bahati mbaya hatuna majina na yupo Mzee wetu Job Lusinde aah ahsante. Naomba asimame. *(Makofi)*

Pia yupo Mzee wetu naye Mbunge Mstaafu, Mzee William Kusila. *(Makofi)*

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Naomba pia niwakaribishe wageni wengine wote ambao sikuwataja. Lakini tumefurahi kwamba mmekuja kushirikiana na sisi na kama mlivyosikia bajeti yetu ndiyo hii iliyosomwa. Majadiliano kamili yataanza siku ya Jumatatu na kwa utaratibu wetu mpya tutaendelea na majadiliano hayo kwa siku saba. Halafu baada ya siku saba tutapitisha hii bajeti yetu kwa kupiga kura. Kwa hiyo kwa tarehe hizo Waheshimiwa lazima muwepo pale, kufa na kupona muwepo.

Halafu baada ya hapo tutaingia kwenye Muswada wa Fedha. Muswada wa Fedha una utaratibu wake pia na kwa sababu Waziri ameshauweka sasa, naomba mfanye bidii kuusoma, hata mkitafuta kwa sababu amesoma basi upo wazi sasa. Kabla ya kusoma usingekuwa wazi.

Kwa hiyo, muusome vizuri, kwa sababu Sheria yetu mpya ya kupitisha Muswada wa Sheria inasema kama unataka kufanya *amendment* katika ule Muswada, unajiandaa mapema, unapeleka kwenye *Budget Committee*, pale patakuwa na wataalam wengi kabisa, watajaribu kufikiria hayo mawazo yako unayoyafanyia kama yanaweza kutekelezeka au sivyo. Kama yanatekelezeka yanakubalika, kama hayatekelezeki watakuambia sababu gani hayatekelezeki na yatakaliwa. Naomba mufanye hivyo. Msifanye uvivu unakuja unasema kutoa *amendment* zako hapa, hazitakubalika.

Waheshimiwa Wabunge, nimewaambia mapema kusudi muweze kujiandaa vizuri zaidi siku siyo nyingi, zinakwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hivyo, kesho hatutakuwa na Bunge. Lakini kuna shughuli mbalimbali ambazo zimeandaliwa pamoja na Kamati ya Uongozi ambayo itahudhuriwa na Waziri Mkuu, itahudhuriwa na Waziri wa Fedha, itahudhuriwa na Wenyeviti wote mtakuwepo pale saa 3 asubuhi.

Baada ya kusema hayo, sina matangazo mengine, niwatakie jioni njema.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Wageni wote mnanafanya mwongozo ahaa.

Baada ya kusema hivyo naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho, ooh mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.20 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu,
Tarehe 16 Juni, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*